YALIYOMO

VIFUPISHO VYA MANENO.....iii - iv

1.0 UTANGULIZI 1

1.1 Hoja ya Kuunda Kamati Teule 1
1.2 Wajumbe na Hadidu za Rejea..... 2
1.3 Utekelezaji wa Majukumu 4

2.0 UKAME NA TATIZO LA UZALISHAJI UMEME NCHINI 10

2.1 Taarifa za Awali na Hatua za Serikali 10
2.2 Maandalizi ya Zabuni 15
2.3 Mchakato wa Zabuni ndani ya TANESCO 18
2.3.1 Vigezo vya Tathmini (*Preliminary Evaluation***)**..... 19
2.4 Mchakato wa Zabuni Ndani ya Wizara 25

3.0 MKATABA KATI YA TANESCO NA RICHMOND DEVELOPMENT40

3.1 Madhumuni, Muundo na Muda wa Mkataba..... 40
3.2 Malipo ya Kodi..... 43
3.3 Malipo mengine 45
3.4 Kuhaulisha Mkataba..... 46
3.5 Fidia kwa Kuchelewa kutekeleza Mkataba..... 46
3.6 Ulinganisho na Mikataba Mingine..... 48
3.7 Uzingatiaji wa Mkataba huu katika kutekeleza Sheria ya CRB na ERB 57

4.0 UTEKELEZAJI WA MKATABA 59

4.1 **Barua ya Dhamana ya Benki (Letter of Credit)** 59
4.2 Majadiliano na Makubaliano kuhusu Masharti ya Barua ya Dhamana ya Benki 63
4.2.1 Maombi ya Masharti ya Barua ya Dhamana ya Benki (Awamu ya Kwanza)..... 63
4.2.2 Mapendekezo ya Richmond Development Company LLC kutaka Masharti mengine mapya ya Barua ya Dhamana ya Benki (Awamu ya Pili)...... 67
4.3 Mchakato wa Kufungua Barua ya Dhamana ya Benki..... 70

4.4 Maombi ya Richmond Development Company LLC kubadilisha tena Masharti ya Barua ya Dhamana ya Benki (Awamu ya Tatu). 74
4.5 Kushindwa kwa Richmond Development Company LLC kutimiza masharti ya Mkataba 84
4.6 Mwelekeo Mpya wa Mkataba wa Umeme wa Dharura 89
4.7 Uhaulishaji wa Mkataba kati ya TANESCO, Richmond na Dowans 95
4.8 Mchakato wa Malipo kwa Dowans Holdings S.A 97
4.9 Madai na malipo ya Dowans Holdings S.A ya *Capacity* na *Interim Energy* Januari 2006 hadi Oktoba, 2007 101

5.0 TAARIFA ZA TAKURU/PPRA 104

5.1 **Chimbuko la Uchunguzi** 104
5.2 **Taarifa ya Mamlaka ya Udhibiti na Ununuzi wa Umma (PPRA)** 109
5.3 **Taarifa ya TAKURU** 114
5.4 **Vyombo vya Habari – Magazeti** 122

6.0 RICHMOND DEVELOPMENT COMPANY LLC NI KINA NANI? . 125

6.1 **Utambulisho wake Kisheria** 125
6.2 **Hadhi ya Richmond kisheria/kikampuni Marekani** 126
6.3 **Hadhi ya Richmond kisheria/ kikampuni Tanzania** 132
6.4 **Uwezo wa Richmond Kifedha, Kitaalamu, Kiutendaji** 138

7.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 142

7.1 **Hitimisho.....** 142
7.2 **Mapendekezo ya Kamati Teule .....** 149
7.3 **Shukrani.....** 164

VIFUPISHO VYA MANENO

$	Alama ya Dola ya Kimarekani
Aggreko	Aggreko International Projects Limited
Alstom	Alstom Power Rentals
BoT	Bank of Tanzania
BRELA	Business Registration and Licensing Authority
CNG	Compressed Natural Gas
COD	Commercial Operating Date
CRB	Contractors Registration Board
CTI	Confederation of Trade and Industries
Dba	Doing business as
Dk	Daktari
Eng.	Injinia
ERB	Engineers Registration Board
GN	Government Notice
GNT	Government Negotiation Team
ICC	International Chamber of Commerce
IPTL	Independent Power Transmission Limited
kWh	kilo Watt hour
LC	Letter of Credit
LLC	Limited Liability Company
Ltd	Limited
Mb	Mbunge
MDRI	Multilateral Debt Relief Initiative

Mhe.	Mheshimiwa
MoF	Ministry of Finance
MW	Mega Watt
PPA	Public Procurement Act
PPRA	Public Procurement Regulatory Authority
t/a	Trading as
TAKUKURU	Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa
TAKURU	Taasisi ya Kuzuia Rushwa
TANESCO	Tanzania Electric Supply Company Limited
TPDC	Tanzania Petroleum Development Corporation
TRA	Tanzania Revenue Authority
UCP	Uniform Customs Practice
US$	United State Dollar
USc	United States cents

TAARIFA YA KAMATI TEULE ILIYOUNDWA NA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA TAREHE 13 NOVEMBA, 2007 KUCHUNGUZA MCHAKATO WA ZABUNI YA UZALISHAJI UMEME WA DHARURA ULIOIPA USHINDI RICHMOND DEVELOPMENT COMPANY LLC YA HOUSTON, TEXAS, MAREKANI MWAKA 2006

1.0 UTANGULIZI

1.1 Hoja ya Kuunda Kamati Teule

Tarehe 13 Novemba, 2007 wakati Bunge likijadili Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara kwa Mwaka 2006, Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa William H. Shellukindo (Mb), alitoa hoja ya kuunda Kamati Teule ya kuchunguza mchakato ulioendeshwa nchini mapema mwaka 2006 wa kumpata mzabuni wa kuzalisha umeme wa dharura wa MW 100 na kutathmini mkataba baina ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na mshindi wa zabuni hiyo Richmond Development Company LLC.

Hoja hiyo iliwasilishwa Bungeni kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni ya 104 (1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2004 inayotamka kwamba:-

"Kamati Teule yaweza kuundwa na Bunge kwa madhumuni maalum, kwa hoja mahususi itakayotolewa kwa ajili hiyo na kuafikiwa".

1.2 Wajumbe na Hadidu za Rejea

Baada ya hoja hiyo kuafikiwa na Bunge, Spika wa Bunge Mheshimiwa Samuel J. Sitta, (Mb) aliteua Wabunge wafuatao, kuunda Kamati Teule kwa mujibu wa Kanuni ya 104 (3) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004:

(a) Mhe. Dk. Harrison George Mwakyembe, Mb
(b) Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya, Mb
(c) Mhe. Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mb
(d) Mhe. Lucas Lumambo Selelii, Mb
(e) Mhe. Herbert James Mntangi, Mb

Tarehe 15 Novemba, 2007 Mhe. Spika aliipa Kamati Teule siku thelathini kukamilisha kazi yake na Hadidu za Rejea zifuatazo kwa ajili ya kutekeleza kazi hiyo ya uchunguzi;

1. Kubainisha Richmond Development Company LLC ni kina nani, na ni kampuni ya shughuli zipi na hivyo kupima uwezo wake kupatiwa zabuni ya kuleta nchini na kujenga mtambo wa umeme wa gesi wa MW 100,

2. Kutathmini mchakato mzima wa jinsi zabuni waliyoshinda Richmond ilivyoshughulikiwa kuanzia Kamati ya Zabuni hadi mwisho ili kujiridhisha kuwa sheria, taratibu, miiko na maadili ya zabuni yanayotawala zabuni za aina hiyo vilifuatwa au vipi,

3. Kutathmini mkataba baina ya Richmond Development Company LLC na TANESCO ili kujiridhisha kuhusu uhalali wa masharti ya mkataba huo ukizingatia gharama na masharti mengine ukilinganisha na masharti yaliyomo katika mikataba ya aina hiyo iliyoafikiwa na TANESCO/Serikali,

4. Kubainisha huduma na misaada mbalimbali waliyopewa Richmond kama vile kufunguliwa *Letter of Credit* na kupima uhalali wake,

5. Kuziangalia na kuzitolea maoni taarifa za TAKUKURU, PPRA na taarifa zozote nyingine zilizoangalia utaratibu wa zabuni ya Richmond, na

6. Kuangalia mambo mengine yoyote yenye uhusiano na mchakato mzima wa Richmond ili kutoa mapendekezo ya kuboresha taratibu za zabuni kwa siku zijazo, kwa maslahi ya Taifa letu.

1.3 Utekelezaji wa Majukumu

Mara baada ya kuteuliwa, Wajumbe wa Kamati Teule walimchagua Mhe. Dk. Harrison George Mwakyembe, (Mb) kuwa Mwenyekiti kwa mujibu wa Kanuni ya 104 (3) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2004. Aidha, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 105(3) ya Kanuni hizo za Bunge, upana wa hadidu rejea na kipindi kifupi cha mwezi mmoja tu cha kukamilisha kazi hiyo, Kamati Teule ikaona umuhimu wa kumchagua mmoja wao kutekeleza wajibu wa Makamu Mwenyekiti kwa lengo la kuboresha ufanisi katika ufuatiliaji wa karibu wa masuala mbali mbali ndani na nje ya vikao vya Kamati Teule. Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya, (Mb) akachaguliwa kutekeleza wajibu huo. Vilevile, Mheshimiwa Spika alimteua Ndugu Anselm Lyatonga Mrema kuwa Katibu wa Kamati Teule akisaidiwa na Ndugu Emmanuel Mpanda, Lina Kitosi na Nenelwa Mwihambi.

Kamati Teule ilianza kazi yake mara moja kwa kukusanya na kusoma nyaraka mbalimbali za msingi kama vile Mkataba kati ya TANESCO na Richmond Development Company LLC, Sheria ya Ununuzi wa Umma (*Public Procurement Act*) ya Mwaka 2004 na Kanuni zake (*Public Procurement Act (Goods, Works, non-Consultant Services & Disposal of Public Assets by Tender) Regulations of 2005*), taarifa ya uchunguzi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)[1] na taarifa ya Mamlaka ya Udhibiti na Ununuzi wa Umma (*Public Procurement Regulatory Authority-PPRA*) kuhusu

[1] Wakati huo ikiitwa Taasisi ya Kuzuia Rushwa (TAKURU)

suala hilo. Vilevile, Kamati Teule ilianza kuandaa hati (*summons*) kwa mujibu wa vifungu 13 (1) na 14 (1) na (2) vya Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, 1988 (Sura ya 296) za kuita mashahidi mbalimbali waliohusika kwa njia moja au nyingine katika mchakato wa zabuni hiyo ya uzalishaji wa umeme wa dharura.

Hadi kufikia tarehe 15 Disemba jumla ya mashahidi 46 walihojiwa na maswali 2061 kuulizwa. Pamoja na taarifa zetu tulizozitoa kupitia vyombo vya habari na kuwataka wenye ushahidi wajitokeze na kuhakikishiwa kuwa Sheria itawalinda, hakuna shahidi hata mmoja aliyekuja kwa hiari yake mwenyewe bila kupelekewa hati ya kuitwa. Aidha, hakuna mtu yeyote aliyeweza kutoa ushahidi wa kimaandishi ulio wazi zaidi ya wale waliojifanya kuwa na uchungu kwa kutoa taarifa zisizo na majina, namba za simu wala anwani kwa madai ya kuogopa kuhatarisha maisha yao.[2] Matokeo haya yanaonesha hali ya uoga na kutojiamini inayowakumba Watanzania wengi wanapotakiwa kuelezea rasmi yaleyale wanayoyanong'ona kwa nguvu au kuyazungumza pembeni kwa hamasa kubwa. Kwa mtindo huu Taifa linaweza kuishia kuwa la walalamishi wasio na ujasiri wala dhamira ya dhati ya kukemea maovu pale inapobidi.

Mashahidi wengi walioitwa kwa hati hususan kutoka TANESCO, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha na Wizara ya Katiba na Sheria walionesha hofu, mashaka na hali ya kutojiamini kwa kutoa majibu yaliyofanana ya kiitifaki-itifaki na yaliyokosa mvuto na

[2] Mfano wa barua kama hizo unaambatanishwa.

ushawishi wa kawaida mithili ya watu walioketishwa pamoja na kukaririshwa hoja za kujibu. Kama itakavyoelezwa baadaye, baadhi ya wataalam wa TANESCO walioikataa Richmond Development Company LLC mara tatu wakati wa kutathmini zabuni ya umeme wa dharura, kwa hoja za kitaalam kuwa haifai kwa vigezo vyote muhimu, walifika mbele ya Kamati Teule wakiwa wapambe nambari moja wa kampuni hiyo!

Aidha, nyaraka nyingi ambazo Kamati Teule ilizipata toka Serikalini na taasisi mbali mbali, zilikuwa nakala zilizokosa mtiririko wa kimasijala. Kamati Teule ilipodai nyaraka halisi kulinganisha na nakala ilizokuwa nazo, ilipewa majalada yaliyoonesha dalili zote za kukarabatiwa.

Hali hii ilijitokeza zaidi kwa TANESCO na Wizara ya Nishati na Madini. Jalada halisi kutoka TANESCO lilichukua siku tatu kuifikia Ofisi Ndogo ya Bunge likiwa na nyaraka zenye namba zilizokosa mtiririko stahili. Wizara ya Nishati na Madini ndiyo iliyotia fora kwa kumtuma Msaidizi wa Katibu Mkuu, Ndugu Julius Sarota tarehe 18 Disemba 2007 akiwa na maagizo ya kuwafungulia Wajumbe wa Kamati Teule kurasa maalum tu na si nyinginezo hivyo kuinyima Kamati Teule mtiririko halisi wa mawasiliano. Kamati Teule haikuridhishwa na utaratibu huo, hivyo ilimtaka Msaidizi huyo wa Katibu Mkuu aondoke na majalada yake na kumpelekea hati ya kuitwa Katibu Mkuu, Ndugu Arthur Mwakapugi afike yeye mwenyewe na majalada hayo.

Tarehe 19 Disemba 2007 Katibu Mkuu huyo kwa maneno mengi na ya kuzunguka alithibitisha kuwa alichokifanya Msaidizi wake yalikuwa maelekezo ya Wizara.[3] Kwa kuzingatia uhaba wa muda wa kukamilisha kazi ya Kamati Teule na kwamba suala hilo tayari lilikuwa limechukua siku tatu nzima za Kamati Teule, ugeni wa Katibu Mkuu huyo katika Wizara hiyo na katika masuala ya Bunge na uwezekano uliokuwepo kwa Kamati Teule kupata taarifa za ziada kupitia njia nyingine, Kamati Teule iliamua kusonga mbele na kumuacha Katibu Mkuu huyo na siri kubwa za Wizara yake.

Pamoja na changamoto hizo, Kamati Teule iliona kuwa ni vyema baadhi ya Wajumbe waende Houston, Texas, Marekani ili kupata taarifa za kina na za ziada kuhusu suala hilo. Kamati Teule inamshukuru sana Mhe. Spika kwa kuzielewa changamoto zilizokuwa zinaikabili Kamati Teule na kuwawezesha Wajumbe watatu kwenda Washington DC kukutana na maafisa wa Ubalozi wetu, na Houston Texas kukutana na wamiliki wa Richmond Development Company LLC. Wajumbe hao walioondoka Dar-es Salaam kwenda Marekani tarehe 10 Disemba 2007 ni:

(a) Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya, Mb
(b) Mhe. Lucas Lumambo Selelii, Mb
(c) Mhe. Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mb, na
(d) Ndugu Anselm L. Mrema (Katibu wa Kamati)

[3] Taarifa Rasmi za Bunge, HANSARD ya tarehe 19/12/ 2007 – Mahojiano na Ndugu Mwakapugi.

Tarehe 12 Disemba 2007 Kamati Teule ilimwandikia barua Mhe. Spika kumuomba aiongezee muda kwa sababu kuu mbili: Kwanza, Wajumbe watatu kati ya watano na Katibu wa Kamati Teule walikuwa nchini Marekani kuanzia tarehe 10 Disemba 2007 kujiridhisha na taarifa mbalimbali ambazo Kamati Teule imekuwa ikizipata kuhusu Richmond Development Company LLC. Kwa kuwa Wajumbe hao walikuwa wanategemea kurejea nchini tarehe 15 Disemba 2007 siku ambayo Kamati Teule ilitakiwa kuwasilisha taarifa yake kwa Mhe. Spika, na pia taarifa ambazo wangezipata Marekani zingetakiwa kuingizwa kwenye taarifa ya Kamati Teule na hata kubadilisha baadhi ya masuala katika taarifa hiyo.

Pili, baada ya uchambuzi wa kina wa ushahidi wa maandishi na wa mdomo uliotolewa mbele ya Kamati Teule chini ya kiapo, Kamati Teule iligundua kuwepo kwa mgongano wa ushahidi, hivyo kutia mashaka juu ya dhamira ya baadhi ya mashahidi. Kamati Teule iliona umuhimu wa kuwaita tena baadhi ya mashahidi kuthibitisha kauli zao, na hata kuwachukulia hatua za kisheria baadhi yao ambao wangeendelea kusema uongo chini ya kiapo ili kulinda heshima ya Bunge.

Mhe. Spika aliona umuhimu wa kuiongezea Kamati Teule muda, hivyo tarehe 13 Disemba 2007 akaridhia ombi la Kamati Teule na kuweka tarehe 31 Disemba 2007 kuwa tarehe ya kuwasilisha taarifa ya uchunguzi. Hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2007 siku

ilipowasilisha taarifa yake kwa Mhe. Spika, Kamati Teule ilikuwa imewahoji jumla ya mashahidi 75 na kuuliza maswali 2717 na kuzipitia nyaraka na kumbukumbu 104. Mashahidi 4 kati ya hao walikuja kwa hiari yao bila kupelekewa hati za kuitwa. Mashahidi 7 waliitwa mara mbili. Mashahidi wawili, Ndugu Daniel Yona na Mhe. Rostam Aziz, (Mb) walipelekewa hati za kuitwa mbele ya Kamati Teule lakini hawakufika kwa maelezo kwamba walikuwa nje ya nchi. Ndugu Daniel Yona alitakiwa na Kamati Teule atoe maelezo kuhusu msingi wa uamuzi wake wa kuipa Richmond Development Company LLC, haki maalum ya kipekee *(exclusive right)* ya miezi 18 kuhusu mradi wa Bomba la Mafuta kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza mwaka 2004 wakati huo akiwa Waziri wa Nishati na Madini. Maelezo ya kina ya mradi huu yako sehemu ya sita ya taarifa hii. Mhe. Rostam Aziz alitakiwa atoe maelezo kuhusu uhusiano wake na Kampuni za Richmond Development Company LLC na Dowans Holdings S.A baada ya mashahidi zaidi ya watano kumtaja kuwa ana uhusiano nazo. Aidha, alitakiwa na Kamati Teule aeleze kwanini anwani ya posta na anwani ya barua pepe ya kampuni yake ya Caspian Construction Company Ltd inatumiwa na Dowans Holdings S.A. Kamati Teule ilipata majina ya baadhi ya wafanyakazi wa Caspian ambao pia wanaitumikia Dowans Holdings S.A.

2.0 UKAME NA TATIZO LA UZALISHAJI UMEME NCHINI

2.1 Taarifa za Awali na Hatua za Serikali

Kwa takribani miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2002 nchi yetu ilikumbwa na tatizo la ukosefu wa mvua za kutosha. Athari za tatizo hilo hasa katika uzalishaji umeme, zilianza kuonekana mwaka 2004, na kufikia mwishoni mwa mwaka 2005 ikawa dhahiri kwamba nchi ilikuwa inaelekea kwenye janga kubwa la upungufu wa umeme. Mahitaji ya mitambo ya gesi ya kuzalishia umeme wa dharura yakajitokeza.

Kutokana na hali hiyo, mwezi Disemba 2005, TANESCO iliiomba Serikali kufikiria na kuidhinisha mpango wa kukodisha mitambo ya kuzalisha umeme wa dharura kwa kutumia gesi kutoka kwenye makampuni yanayofahamika kwa biashara hiyo chini ya Mikataba ya kuuziana umeme kwa muda usiopungua miezi kumi na mbili.

Tarehe 28 Disemba 2005 Serikali ilikubali ombi hilo na kuiruhusu TANESCO kuwasiliana moja kwa moja na kampuni ya Songas kuhusu mahitaji hayo ya dharura ya nchi. Bila kuchelewa TANESCO wakawasiliana na Songas ambayo ikaanza mara moja kuandaa makisio ya mradi huo. Tarehe 11 Januari 2006, CDC Globeleq, kampuni mama ya Songas, iliwasilisha TANESCO makisio ya kukodisha mitambo ya gesi ya kuzalisha umeme wa MW 74 ambayo ingefungwa Ubungo na kuanza kuzalisha umeme katikati ya mwezi Aprili 2006.

Tarehe 13 Januari 2006 Bodi ya Zabuni ya TANESCO ilianza kujadili zabuni hiyo ya CDC Globeleq na siku sita baadaye, yaani tarehe 19 Januari 2006, Bodi hiyo ikathibitisha mapendekezo ya zabuni hiyo na kuingia katika majadiliano na CDC Globeleq. Tarehe 30 Januari, 2006 Bodi ya Zabuni ya TANESCO iliyakubali mapendekezo ya Kamati ya Tathmini ya kuingia mkataba wa uzalishaji umeme kwa miaka mitano au mitatu kama ifuatavyo: (i) miaka mitano kwa bei ya senti za Kimarekani 3.2/kWh; au (ii) miaka mitatu kwa bei ya senti za Kimarekani 5.3/kWh. Chini ya mpango huo, mitambo hiyo ya kuzalisha umeme ingekuwa mali ya TANESCO baada ya kipindi cha kukodi kumalizika.[4]

Taarifa hizi pamoja na mapendekezo ya Wizara ya Nishati na Madini yaliwasilishwa na kujadiliwa katika Kikao cha Baraza la Mawaziri cha tarehe 10 Februari 2006, yaani siku nne baada ya kuanza mgao wa umeme kwa mikoa yote ya Tanzania Bara inayounganishwa na Gridi ya Taifa.

Pamoja na mambo mengine, Baraza la Mawaziri liliiagiza Timu ya Wataalamu (*Technical, Financial and Legal Experts Team*) iliyokuwa inaundwa na Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali chini ya uenyekiti wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, ishugulikie masuala makuu manne:

[4] Waraka wa Baraza la Mawaziri Na. 2/2006

(i) ununuzi wa mitambo ya MW 60-100 ambao ungefungwa Ubungo pamoja na jenereta za mafuta za MW 40 ambazo zingefungwa Mwanza, Arusha na Moshi kwa kutumia fedha zilizotegemewa kutoka Mifuko ya Pensheni nchini;

(ii) ukaguzi wa mitambo ya kutoka CDC Globeleq ili kujiridhisha na hali na ubora wa mitambo hiyo;

(iii) kuitaka CDC Globeleq ikubali kuiuzia Serikali mitambo hiyo moja kwa moja tangu mwanzo au iikodishe Serikali kwa bei ambayo Serikali ingeridhika nayo na siyo kwa kipindi cha miaka mitano bali kipindi kile tu cha matatizo ya umeme kutokana na ukame;

(iv) kutafuta na kukagua mitambo ya kuzalisha umeme wa MW 60-100 Ubungo ikiwa ni pamoja na mitambo ya CDC Globeleq kwa muda mfupi iwezekanavyo ili ipatikane na kufungwa mara moja kupunguza tatizo la umeme nchini.

Ni dhahiri kuwa kwa maamuzi hayo, Serikali haikutaka kufanya makosa kwa kuweka mayai yote kwenye kikapu kimoja kutokana na hali ya kutisha ya upungufu wa nishati ya umeme nchini. Lakini Kamati Teule imebaini kuwa utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri haukuwa makini kama inavyoelezwa hapa chini.

Siku hiyo hiyo ya tarehe 10 Februari 2006, Wizara ya Nishati na Madini, badala ya kuwatumia ujumbe sahihi CDC Globeleq kuwa Serikali inataka wapunguze kipindi cha ukodishaji mitambo, washushe zaidi bei yao ya umeme na wawe tayari kuzalisha umeme

ifikapo Mei 2006, ilipeleka ujumbe tofauti kabisa kuwa Serikali inafuta mpango wa kukodisha mitambo kutoka kwao. Sehemu ya barua hiyo iliyoandikwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ndugu Arthur Mwakapugi, ikijibu barua iliyoandikwa na CDC Globeleq kwenda kwa Waziri Mkuu, inasema:

> *"I wish to inform you that despite the progress you have so far made in effecting the project, the Government has decided to cancel the leasing of the plant and instead will be provide (sic) funds to TANESCO to procure, install and commission a similar plant".*[5] (Napenda kukufahamisha kuwa licha ya maendeleo mazuri mliyoyafanya katika kutekeleza mradi, Serikali imeamua kufuta ukodishaji wa mtambo na badala yake itaipatia TANESCO fedha za kununulia, kufunga na kuzindua mtambo wa aina hiyo hiyo).

Pamoja na kumhoji aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini kipindi hicho Mhe. Dk. Ibrahim Msabaha, (Mb) na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Ndugu Arthur Mwakapugi kwa muda mrefu na katika siku nne tofauti, Kamati Teule imeshindwa kupata majibu ya uhakika kwa maswali yake manne:

(i) Je, kulikuwa na kikao kingine cha Baraza la Mawaziri siku hiyo hiyo ya tarehe 10 Februari, 2006 kilichotengua maamuzi yake ya awali ya siku hiyo hiyo?

[5] Barua kutoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini Kumb. Na. CBD.286/397/01 ya tarehe 10/02/06.

(ii) Ikiwa jibu ni hapana, kwa nini Wizara ilipeleka CDC Globeleq ujumbe tofauti na ule ilioagizwa na Baraza la Mawaziri?

(iii) Kwa nini Wizara isitume barua hiyo baada ya kushindwa kuwashawishi CDC Globeleq kubadilisha masharti yao?

(iv) Maamuzi kama hayo, siku nne ndani ya mgao wa umeme wa nchi nzima na katika kipindi ambacho Serikali haikuwa na mkakati mbadala uliokuwa umeiva kama wa CDC Globeleq, yalikuwa kweli maamuzi makini ya kunufaisha Taifa?[6]

Kutokana na msimamo huo mpya wa Wizara, TANESCO ikaachana na mpango wa kukodisha mitambo na kuelekeza nguvu zake kwenye kununua mitambo mipya ya kuzalishia umeme. Hivyo, tarehe 20 Februari 2006, TANESCO iliwasilisha kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini mpango wa ununuzi wa moja kwa moja kutoka kwa watengenezaji wa mitambo ya kuzalishia umeme wanaofahamika duniani chini ya utaratibu unaotambuliwa kama *international shopping* chini ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 na Kanuni zake.

Hatua hiyo ikafuatiwa na kikao cha Waziri wa Nishati na Madini na watendaji wa Wizara na TANESCO tarehe 21 Februari 2006 ambacho Waziri alikitumia kusisitiza kuwa mpango wa Serikali si kukodisha mitambo bali kununua. Hivyo akaiagiza TANESCO kutangaza mara moja zabuni ya kununua mitambo mipya au iliyotumika ya kuzalishia

[6] Taarifa Rasmi za Bunge, HANSARD za tarehe 4, 7, 10 na 19/12/07.

umeme ama sivyo hatua kali za kinidhamu zingechukuliwa dhidi ya viongozi wa shirika.[7]

Waziri alitaka tangazo la zabuni lichapishwe magazetini siku ya Alhamisi tarehe 23 Februari 2006 na kuwapa TANESCO masharti yafuatayo kwa zabuni hiyo: (i) ifunguliwe baada ya siku 10 (yaani tarehe 6 Machi 2006); (ii) tathmini ya zabuni ifanyike kwa siku mbili (tarehe 7 - 8 Machi 2006). Aidha, Waziri alitaka Kamati ya Kutathmini Zabuni iongozwe na TANESCO lakini iwe na wajumbe wengine kutoka Hazina, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mifuko ya Pensheni na Wizara ya Nishati na Madini.[8]

2.2 Maandalizi ya Zabuni

Tarehe 22 Februari 2006 TANESCO iliomba idhini ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kutangaza zabuni hiyo kwa muda wa siku 10 badala ya siku 45 zinazoainishwa katika Kanuni za Ununuzi.[9] Tarehe hiyo hiyo ya 22 Februari 2006, PPRA ikaijibu TANESCO kwa kuitahadharisha kuwa utaratibu huo utakuwa kinyume cha taratibu na Kanuni za ununuzi. Muda wa siku 10 hautoshi kuitisha zabuni ya kimataifa na kuweza kupata wazabuni wenye sifa zinazohitajika.

[7] Muhtasari wa kikao cha tarehe 21/02/06.
[8] Angalia Na.7
[9] Barua Kumb. Na.DST/18/49 ya tarehe 22/02/06

Mamlaka ikaishauri TANESCO kuwa badala ya kutumia njia ya kutangaza zabuni ya kimataifa (*international competitive tendering*) itumie njia mbadala ya ununuzi wa kimataifa (*international shopping)* ambapo makampuni mengi yanayotengeneza mitambo ya kuzalisha umeme yanaalikwa na "kuyashindanisha kwa kuyaomba yawasilishe zabuni zao badala ya kutangaza kwani utaratibu huo ungesaidia kuondoa makampuni ya kati yasiyohusika na uzalishaji umeme".[10]

Tarehe hiyo hiyo 22 Februari, 2006 TANESCO ikaiarifu Wizara kuhusu ushauri wa PPRA. Wizara iliukataa ushauri huu na kuiagiza TANESCO kutekeleza agizo la Waziri bila kukosa kwa kuitangaza zabuni hiyo. Zabuni hiyo ikatangazwa kwa utaratibu wa ndani tarehe 23 Februari 2006. Hatua hiyo iliishitua PPRA ambayo iliiandikia barua TANESCO kuelezea kushangazwa kwake na hatua ya shirika hilo kukaidi ushauri wa kitaalamu na wa kisheria. PPRA ikasisitiza kuwa, njia pekee kwa TANESCO kupata wazabuni wazuri na wenye sifa stahili katika kipindi kifupi ni kutumia utaratibu iliyoupendekeza wa *international shopping*.[11]

Hali ya uzalishaji umeme nchini iliendelea kuwa tete na kulazimu kikao cha Baraza la Mawaziri kufanyika tarehe 23 Februari 2006, na kuagiza utaratibu wa haraka *(fast track)* wa kukodi mitambo ya kuzalishia umeme wa dharura ufanyike. Baraza liliagiza kuwa,

[10] Barua Kumb. Na. PPRA/TANESCO/41/16 22/02/06
[11] Barua Kumb. Na. PPRA/TANESCO/41/18 ya 23/02/06

katika kutekeleza maamuzi haya, Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005 zizingatiwe. Pamoja na msisitizo huo wa Baraza la Mawaziri, Wizara ya Nishati na Madini ikaendelea kuishinikiza TANESCO kufuata maagizo ya Wizara na si vinginevyo.

Jumapili tarehe 26 Februari 2006 TANESCO ikionyesha dhahiri kusukumwa tu na Wizara, ikaiandikia tena barua PPRA kuelezea kuwa sasa imeagizwa na Serikali kuitangaza zabuni hiyo magazetini, hivyo mamlaka hiyo ya udhibiti wa ununuzi wa umma itoe idhini ya kutangaza zabuni ya kimataifa kwa siku chache kuliko zilizowekwa na sheria.[12] TANESCO huku ikijua kabisa kuwa PPRA isingeweza kuipata na kuijibu barua hiyo Jumapili, ikatangaza zabuni hiyo magazetini tarehe 27 Februari 2006[13] na kuwataka wazabuni wawasilishe zabuni zao tarehe 6 Machi 2006 yaani siku 10 baada ya kuchukua nyaraka za zabuni tarehe 24 Februari 2006.

Tarehe 1 Machi 2006 PPRA ikaijibu TANESCO kuwa pamoja na kuendelea na zabuni hiyo, isingekuwa rahisi kwa Shirika hilo la umeme la Taifa kupata mzabuni anayefaa katika kipindi hicho kifupi cha siku 10. Hata hivyo PPRA ikaitaka TANESCO kuufuatilia utaratibu mzima wa zabuni hiyo kwa karibu ili kuhakikisha kuwa taratibu

[12] Barua Kumb. Na.DST/18/50 ya tarehe 26/02/06
[13] Gazeti la DAILY NEWS tarehe 27/02/06

zinafuatwa, ili kuepusha malamiko yasiyo ya msingi kutoka kwa wazabuni.[14]

Pamoja na kuipongeza PPRA kwa kuonesha subira ya hali ya juu, uwazi na ukweli wa kitaaluma, Kamati Teule ilishindwa kubaini chanzo cha ujasiri wa kiburi ndani ya Wizara ya Nishati na Madini kiasi cha kupindisha maamuzi ya Baraza la Mawaziri kama tulivyoona pamoja na kukaidi ushauri wa Mamlaka zilizopo kisheria.

2.3 Mchakato wa Zabuni ndani ya TANESCO

Ili kupata muda zaidi wa zabuni ililazimu muda wa zabuni kuongezwa hadi tarehe 20 Machi 2006 ambapo jumla ya wazabuni ishirini na sita (26) walinunua nyaraka za zabuni zilizouzwa kwa fedha isiyorejesheka (*non refundable*) ya Dola za Kimarekani 100. Ni wazabuni wanane (8) tu ndio waliorudisha nyaraka za zabuni hiyo kama ifuatavyo:

(i) M/S Aggreko International Projects Ltd ya Uarabuni,
(ii) M/S Quantus ya Ujerumani,
(iii) M/S APGUM Co. Ltd ya Ujerumani,
(iv) M/S Globeleq Ltd ya Kanada,
(v) M/S Real Energy Projects ya Uingereza,
(vi) M/S Renco SPA ya Italia,
(vii) M/S Richmond Development Company LLC ya Marekani, na
(viii) M/S GAPCO(T) Ltd ya Tanzania.

[14] Barua Kumb. Na. PPRA/TANESCO/41/21 ya tarehe 01/03/06

Zabuni zikafunguliwa. Wazabuni wote waliorudisha nyaraka zao za zabuni waliwakilishwa kwenye ufunguzi. TANESCO ikaunda Kamati ya Kutathmini Zabuni iliyokuwa na wajumbe 12, kati yao wanane walitoka TANESCO, wawili kutoka kampuni ya ushauri ya Lahmeyer International, mmoja kutoka Wizara ya Fedha na mwingine Wizara ya Nishati na Madini. Kamati hiyo ilipewa wiki moja tu kumaliza kazi yake na kuiwasilisha taarifa ya tathmini kwenye Bodi ya Zabuni ya TANESCO tarehe 28 Machi, 2006.

2.3.1 Vigezo vya Tathmini (*Preliminary Evaluation*)

Kamati ya Tathmini ilitumia vigezo vifuatavyo kupima uwezo wa mzabuni:

(i) Muda wa kuleta mtambo na kuanza kazi,
(ii) Dhamana ya zabuni (*Tender Security*),
(iii) Kipindi cha mchakato wa Zabuni (*Tender Validity*),
(iv) Uwepo wa mitambo na uwezekano wa kusafirishwa,
(v) Uzoefu wa mzabuni kutekeleza na kuendesha mitambo ya aina hiyo,
(vi) Kibali cha mtengenezaji wa mitambo,
(vii) Uwezo wa kupata mkopo,
(viii) Mapato (*turnover*)
(ix) Uzoefu na sifa za kiufundi za mzabuni,

(x) Viambatisho vya idhini ya kisheria vya kuweza kutoa maamuzi ya mwisho (*Power of Attorney*)
(xi) Hati iliyotiwa saini ya mwakilishi wa kisheria wa mzabuni,
(xii) Hati iliyotiwa saini ya mwakilishi wa kisheria wa mtengenezaji wa mitambo,
(xiii) Hati ya nchi anayotoka mzalishaji wa mitambo,
(xiv) Uwepo wa maelezo ya lazima ya kiufundi,
(xv) Barua ya dhamana kwa ajili mahitaji ya kiufundi na ubora wa bidhaa inayotolewa na mtengenezaji wa mitambo,
(xvi) Ujazaji fomu ya zabuni kikamilifu,
(xvii) Mchanganuo wa bei/gharama ya umeme,
(xviii) Uhakika kuwa wakala/ kuwa na uwezo wa kufanya matengenezo na kuwa na vipuri, na
(xix) Muda wa kukodisha mitambo.

Matokeo ya uchambuzi wa zabuni zote nane yalionesha kuwa hakuna mzabuni hata mmoja aliyetimiza au kukidhi vigezo vya zabuni vilivyowekwa (*non responsive*). Kutokana na hali mbaya ya uzalishaji umeme nchini, Kamati ya Tathmini ikalazimika kuondoa zaidi ya nusu ya vigezo na kuvibakiza tisa tu ilivyoviona kuwa ni muhimu sana kwa ngazi ile ya uchambuzi ili kumpata mshindi katika kundi hilo la wazabuni wanane. Vigezo vilivyobakizwa ni:

(i) Muda wa kuleta mtambo na kuanza kazi,
(ii) Dhamana ya zabuni (*Tender Security*),

(iii) Uwepo wa mtambo tayari kuletwa Tanzania,

(iv) Uzoefu wa mzabuni kutekeleza miradi/ kuendesha mitambo ya aina hiyo,

(v) Uzoefu na sifa za kitaaluma/ kiufundi za mzabuni,

(vi) Viambatisho vya idhini ya kisheria kuweza kufanya maamuzi ya mwisho (*Power of Attorney*),

(vii) Uwepo wa maelezo ya lazima ya kiufundi,

(viii) Ujazaji fomu ya zabuni kikamilifu, na

(ix) Mchanganuo wa bei/ gharama ya umeme.

Wazabuni wote wanane walifanyiwa tena tathmini ya pili kwa kuzingatia vigezo hivyo tu. Hata hivyo matokeo yakawa yaleyale. Wazabuni wote wanane wakashindwa kukidhi vigezo hivyo vichache.

Nyaraka tulizozipata kutoka TANESCO zinaonesha maeneo mbalimbali ya udhaifu miongoni mwa wazabuni kama ifuatavyo:-

i) M/S Aggreko International Projects Ltd ya Uarabuni ilikutwa na maeneo 7 yenye mapungufu,

(ii) M/S Renco SPA ya Italia maeneo 9,

(iii) M/S APGUM Co. Ltd ya Ujerumani maeneo 12,

(iv) M/S GAPCO(T) Ltd ya Tanzania maeneo 13,

(v) M/S Globeleq Ltd ya Kanada maeneo 14,

(vi) M/S Real Energy Projects ya Uingereza maeneo 15,

(vii) M/S Quantus ya Ujerumani maeneo 16, na

(viii) M/S Richmond Development Company LLC ya Marekani ilikutwa na maeneo 17 yenye mapungufu.

Kamati ya Tathmini haikuona busara kutangaza kuwa imeshindikana kabisa kumpata mshindi. Hivyo, ikapunguza vigezo zaidi na kubakiza vitano tu kama ifuatavyo:

(i) muda ambao mtambo utaanza kazi,
(ii) uwepo wa mtambo tayari kuletwa Tanzania,
(iii) uzoefu wa mzabuni kutekeleza miradi/kuendesha mitambo ya aina hiyo,
(iv) uzoefu na sifa za kitaaluma/ kiufundi za mzabuni, na
(v) uwepo wa maelezo ya lazima ya kiufundi.

Katika hatua hii wazabuni wanne (4) wakashindwa kukidhi vigezo vichache vilivyobakizwa, hivyo kushindwa kufuzu kuingia hatua ya pili ya kufanyiwa tathmini ya kina (*detailed evaluation*). Wazabuni walioshindwa ni:

(i) M/S Aggreko International Projects Ltd ya Uarabuni,
(ii) M/S Quantus ya Ujerumani,
(iii) M/S APGUM Co. Ltd ya Ujerumani, na
(iv) M/S Globeleq Ltd ya Kanada.

Wazabuni walioonekana kuwa na afadhali kidogo na kuingia hatua ya pili ya kufanyiwa tathmini ya kina ni:

(i) M/S Real Energy Projects ya Uingereza,

(ii) M/S Renco SPA ya Italia,

(iii) M/S GAPCO(T) Ltd ya Tanzania, na

(iv) M/S Richmond Development Company LLC ya Marekani.

Tathmini ya kina ya wazabuni hao wanne walioonekana afadhali kidogo, ilionesha kuwa Richmond Development Company LLC ya Marekani bado ilikuwa na mapungufu mengi yaani 13 kupita wazabuni wengine watatu. M/s Renco SPA ya Italia ilifuatia kwa kuwa na mapungufu 10; M/s GAPCO (T) Ltd ya Tanzania mapungufu 9 na M/s Real Energy Project ya Uingereza mapungufu 8. Kamati ya Tathmini iliwasilisha matokeo ya tathmini kwa Bodi ya Zabuni ya TANESCO ikielezea kwamba hakuna mzabuni hata mmoja aliyetimiza masharti, na kwamba wote walikosa sifa za kupata zabuni. Hivyo Kamati ikashauri kuwa zabuni itangazwe upya. Bodi ya Zabuni ya TANESCO baada ya kuridhia mapendekezo hayo, iliyawasilisha kwenye Bodi ya Wakurugenzi wa TANESCO tarehe 30 Machi 2006.

Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO ilipitia tathmini nzima na kuamua kwa kauli moja kuishauri Serikali kurejea kwenye ushauri wa PPRA wa kutumia njia ya *international shopping* ili kupata *quotations* moja kwa moja kutoka kwa watengenezaji wa mitambo ya kuzalishia umeme kwa gesi.

Kesho yake, yaani tarehe 1 Aprili 2006 Waziri wa Nishati na Madini, wakati huo Mhe. Dk. Ibrahim Msabaha, (Mb.) akionesha dhahiri kutotaka njia ya *international shopping* kutumika, akawaita wajumbe wote wa Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO na kuwaagiza wahakikishe kuwa Bodi ya Zabuni ya shirika inawaita tena wazabuni wote waliojitokeza awali na makampuni mengine yoyote yenye uwezo wa kuingiza nchini mitambo hiyo. Aidha, Mhe. Dk. Ibrahim Msabaha, (Mb.) alisisitiza kwa barua kwamba:

> *"Mshindi wa tenda ya ununuzi wa mitambo mipya atajulikana baada ya idhini ya Serikali kutolewa. Composition ya wajumbe wa TANESCO Tender Board ibadilishwe na kuimarishwa kwa kuwa na wajumbe wenye uwezo na ni pro-active".*[15]

Ni dhahiri kuwa agizo hili la Waziri lilikuwa batili kwani Sheria ya Ununuzi wa Umma haimpi Waziri mamlaka ya kuteua Wajumbe wa Bodi za zabuni za Mashirika yaliyo chini ya Wizara yake.

Tarehe 10 Aprili 2006, wakati Menejimenti ya TANESCO iko kwenye zoezi la kutekeleza maagizo hayo ya Waziri, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO akasitisha mchakato huo kusubiri maelekezo ya ziada toka Wizarani. Siku mbili baadaye, yaani tarehe 12 Aprili 2006, Waziri akamwandikia barua Mwenyekiti wa Bodi

[15] Maagizo ya Waziri wa Nishati na Madini, Kumb. Na. CBD 88/286/01 ya tarehe 01/04/06

kuwa suala la zabuni hiyo haliko mikononi mwa TANESCO tena, na kusisitiza kwamba:

> *"Suala la kushugulikia gas turbines za kukodisha lilishashughulikiwa na Mhe. Waziri Mkuu, ambaye aliunda Kamati ya wataalamu watatu: KM Hazina, KM Nishati na AG. Nia ni kuliondoa suala zima kwenye mikono ya Menejimenti ya TANESCO ambayo imeshindwa kulishughulikia kwa ufanisi. Waachie Kamati iliyoteuliwa kufanya kazi hiyo … Pasiwe tena na picha kama vile Menejimenti ya TANESCO imerejeshewa kazi hiyo, maana huko kutakuwa ni kukiuka maagizo ya Mhe. Waziri Mkuu".*[16]

Kesho yake tarehe 13 Aprili 2006, Mkurugenzi Mwendeshaji wa TANESCO wakati huo, Bw. Adriaan Van De Merwe, akamtumia Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini nyaraka zote kuhusu zabuni yenyewe na uchambuzi wote kwa uamuzi na uteuzi wa mwisho wa mzabuni.[17]

2.4 Mchakato wa Zabuni Ndani ya Wizara

Tarehe 20 Aprili 2006, Wizara ya Nishati na Madini iliamua kuunda timu ya wataalamu ili ichague mzabuni mmoja kati ya wanane walioshiriki kwenye zabuni na kufanya naye majadiliano ya

[16] Barua Kumb. Na. CBD.88/286/01 ya tarehe 12/04/06
[17] Barua Kumb. Na. MD/010 ya tarehe 13Aprili, 2006

mkataba. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali ilikuwa tayari imejiandaa na kamati zake zifuatazo: Kamati ya Makatibu Wakuu, Kamati ya Watalaam na Kamati ya Serikali ya Majadiliano.

Kamati ya Makatibu Wakuu iliundwa katika kikao cha Baraza la Mawaziri cha tarehe 10 Februari 2006, ikiwajumuisha Makatibu Wakuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kamati hii ilipewa jukumu la kusimamia mchakato mzima wa zabuni. Ili kuharakisha zoezi hilo, Serikali iliunda Kamati ya Wataalam (*Team of Experts*) ili kuisaidia kwa karibu Kamati ya Makatibu Wakuu.[18]

Kamati Teule iligundua kuwa Kamati ya Wataalam ndiyo ilikuwa yenye maamuzi katika mchakato huu na ndiyo iliyokuwa na mawasiliano ya karibu na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, kwani Kamati ya Makatibu Wakuu ilikutana mara moja tu toka iundwe.[19]

Kazi ya kwanza ya Kamati ya Wataalam ilikuwa ni kupitia upya na kuichambua tathmini iliyofanywa na TANESCO. Kazi ya pili ya Kamati hiyo ilikuwa ni kumpata mzabuni ambaye angeweza kutekeleza mradi huo wa umeme wa dharura kwa haraka. Kamati hiyo ikatupilia mbali vigezo vya msingi vilivyotumika na Kamati ya Tathmini ya TANESCO na kuweka vipya ambavyo, kwa maoni ya

[18] Barua Kumb. Na CBD 214/324/01/13 ya tarehe 21/03/06
[19] Taarifa Rasmi za Bunge, HANSARD ya tarehe 05/12/07 – Mahojiano na Ndugu Gray Mgonja.

Kamati Teule, vilifanana na vigezo vya mchezo wa watoto wa sadakarawe: “mwenye kupata apate, mwenye kukosa akose”.
Vigezo hivyo vilikuwa:

(i) Uwepo wa mitambo yenyewe pamoja na mitambo ya akiba,
(ii) Uunganishwaji wake kwenye gridi ya Taifa,
(iii) Hali ya usalama wa mitambo yenyewe kwa kulinganisha na usalama wa gridi ya Taifa,
(iv) Muda wa kuleta mitambo, na
(v) Bei ya umeme.

Kwa maoni ya Kamati Teule, vigezo hivyo vilikuwa haviendani na uzito na utaalam wa kazi iliyokusudiwa. Pia viliweza kutoa mwanya hata kwa wazabuni dhaifu kupenyezwa.

Kamati ya Wataalamu ikawaalika wazabuni wote 8 kwa usaili wa kuwapima kufuatana na vigezo hivyo vipya. Mzabuni mmoja kati ya wazabuni wanane, M/S GAPCO (T) Ltd hakushiriki. Baada ya usaili huo, Kamati hiyo ikapata wazabuni wanne ambao walionesha kukidhi vigezo hivyo vipya. Wazabuni hao ni: Richmond Development Company LLC, Renco SPA, Aggreko International Projects Ltd na APGUM Co. Ltd.

Aggreko International Projects Ltd walidai kuwa na uwezo wa kuzalisha umeme wa MW 40 kwa senti za Kimarekani 6.0/kWh; Renco SPA walidai kuwa na uwezo wa kuzalisha umeme wa MW 60

kwa senti 10.0/kWh; Richmond Development Company LLC ilidai kuwa na uwezo wa kuzalisha umeme wa MW 100 kwa senti 4.99/kWh; na APGUM Co. Ltd ilidai kuwa na uwezo kuzalisha umeme wa MW 100 kwa senti za Kimarekani 5.4/kWh.

Kutokana na madai hayo yasiyo na uthibitisho Kamati ya Wataalamu ikaipendekeza Richmond Development Company LLC kuingia kwenye majadiliano ya mkataba na Serikali. Katika kuhalalisha ushindi huo wa Richmond Development Company LLC wajumbe wote wa Kamati hiyo ya wataalamu, Waziri wa Nishati na Madini aliyetangulia Mhe. Dk. Ibrahim Msabaha (Mb), Waziri wa sasa wa Wizara hiyo, Mhe. Nazir Karamagi (Mb), Katibu Mkuu wake, Ndugu Arthur Mwakapugi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Johnson Mwanyika, (Mb), Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Ndugu Gray Mgonja na maafisa wote waandamizi wa Serikali na TANESCO waliotoa ushahidi mbele ya Kamati Teule, walitoa kauli zilizofanana mithili ya wimbo maarufu kuhusu sifa za Richmond Development Company LLC zilizoifanya ishinde kuwa: kwanza, bei yake ya umeme ilikuwa chini kupita makampuni mengine; pili, kampuni hiyo ilikuwa na ubia na kampuni kubwa na maarufu duniani ya Pratt & Whitney ya Marekani inayotengeneza mitambo mbalimbali ya umeme; na tatu, iliwasilisha pendekezo lake kama mwendelezaji miradi.[20]

Pamoja na wimbo huo kunoga, Kamati Teule ilishangazwa na udhaifu mkubwa wa hoja hizo usiolingana hata kidogo na ujuzi na

[20] Taarifa Rasmi za Bunge HANSARD za tarehe 28, 29, 30/11/07 na 3,4,5,6,7,10,19,21/12/07

uzoefu walionao watendaji wa TANESCO na Serikali hivyo kujenga hisia kuwa Richmond Development Company LLC ilibebwa. Kwa mfano, kwanza, Hoja ya bei iliyopendekezwa na Richmond Development Company LLC kuwa ilikuwa ndogo haijitoshelezi. Je, Kamati hiyo ililinganisha bei hiyo na nini? Kwani katika kuangalia kumbukumbu za mchakato wa majadiliano, Kamati hiyo haikuwa na kiwango chochote cha makadirio ya bei ya umeme wa kukodi ambacho kingetumika kama kigezo cha kupima unafuu huo kama upo badala ya kulinganisha na bei za makampuni ambayo yalikwisha tubebesha mzigo mkubwa wa malipo hapo awali.

Aidha, Kamati Teule ilipata tetesi na baadaye ushahidi kuwa Richmond Development Company LLC ilikuwa na wapambe ndani ya Wizara ya Nishati na Madini na TANESCO waliokuwa wanaipa taarifa *(insider dealing).* Mfano mdogo tu ni kama vile aliyekuwa Mkurugenzi wa Usambazaji wa TANESCO Ndugu Mohamed Saleh, aliyeshiriki kwenye Kamati ya Wataalam, na vile vile Kamati ya Serikali ya Majadiliano, alipostaafu tu TANESCO akawa mmoja wa wahandisi waandamizi wa DOWANS HOLDINGS S.A iliyochukua majukumu ya Richmond Development Company LLC.[21]

Pili, ni hoja ya kwamba kampuni hiyo ilikuwa na ubia na kampuni kubwa ya Pratt & Whitney. Katika mchakato wote wa zabuni ndani ya TANESCO, moja ya masuala kadhaa yaliyoifanya Richmond Development Company LLC isitiliwe maanani, ni ukosefu wa

[21] Taarifa rasmi za Bunge HANSARD ya tarehe 04/12/06 - Mahojiano na Ndugu. Mohamed Saleh

ushahidi wa kisheria wa ubia (*consortium agreement*) kati yake na Pratt & Whitney. Baada ya kubanwa na Kamati Teule kuhusu ushahidi wa mahusiano wa kampuni hizo mbili, Wajumbe wa Kamati ya Wataalamu waliwasilisha mbele ya Kamati Teule *business card* ya mzungu mmoja Bwana John Perun[22] aliyejiita mwakilishi wa Pratt & Whitney, na kivuli cha mkataba wa kurasa nne kati ya Richmond Development Company LLC na Pratt & Whitney wa kubadilishana taarifa na siyo kuzalisha umeme, na uliokuwa haujathibitishwa na wakili au shahidi yeyote wa kuaminika kuwa ushahidi wa ubia.[23] Kamati Teule imesikitishwa na kushangazwa kwa kiwango cha chini cha umakini kilichoonyeshwa na wataalam wetu hususan Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kushughulikia suala hili.

Kamati Teule inaamini kuwa bila kujihusisha na Pratt & Whitney, kampuni hiyo ya Richmond Development Company LLC isingeweza kamwe kushinda zabuni hiyo. Hivyo ushahidi wa uhusiano wa kisheria wa Kampuni hizo mbili, ilikuwa suala la msingi ambalo wataalamu wetu waliwajibika kulipa uzito ili kulinda maslahi ya nchi.

Katika tovuti yake (www.rdevco.com) Richmond Development Company LLC ilikuwa inajitangaza kimataifa kuwa kampuni yenye miradi mikubwa Tanzania ya ujenzi wa kiwanja cha kisasa cha michezo, ujenzi wa bomba la mafuta la kilometa 1,150 na ukarabati

[22] *Business Card* ya John Perun

[23] Nakala ya Mkataba wa kubadilishana taarifa kati ya Richmond Development Company LLC na Pratt & Whitney.

wa viwanja kadhaa vya ndege.[24] Kamati Teule ilishindwa kuelewa kwa nini Kamati ya Wataalam haikuihoji Richmond Development Company LLC kuhusu uongo huo bayana ambao ulikuwa ushahidi wa kutosha kuipotezea sifa.

Hoja ya tatu kwamba Richmond Development Company LLC ni mwendelezaji miradi ilitakiwa vile vile ifanyiwe kazi badala ya kuiamini tu. Wizara ya Nishati na Madini haiwezi kukwepa lawama kwa kufumbia macho ukweli kuwa Richmond Development Company LLC ilishawahi kuwa na Mkataba na Wizara hiyo uliosainiwa tarehe 30 Juni 2004, na kuvunjika mwezi Januari 2006 kwa kampuni hiyo ya Kimarekani iliyojitambulisha kama mwendelezaji miradi kushindwa kutekeleza sehemu yake ya mkataba. Wizara inaelewa fika kuwa kampuni hiyo ilishindwa utekelezaji huo kutokana na kuyumba kifedha. Mwendelezaji miradi gani ambaye anashindwa kumudu hata fedha ya kununulia maafisa wake tiketi ya ndege kutoka Dar-es-Salaam hadi Afrika Kusini na kurejea?[25]

Kama tulivyodokeza hapo awali baada ya Kamati ya Wataalam kumaliza kazi yake na kuwasilisha taarifa Serikalini, Kamati ya Serikali ya Majadiliano *(Government Negotiation Team- GNT)* ikiwa na wajumbe kutoka TANESCO, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha, Benki Kuu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ikaanza mchakato wa majadiliano ya mkataba na mshindi wa

[24] Nakala ya kipeperushi cha Richmond Development Company LLC na nakala ya *company profile*
[25] Taarifa Rasmi ya Bunge HANSARD tarehe 19/12/07 – Mahojiano na Ndugu John Chaggama

zabuni. Kama ilivyotokea kwa Kamati ya Wataalam, *Government Negotiation Team* vile vile haikufanya kazi ya kuridhisha japokuwa ilikuwa na uwakilishi mpana. Kwa mfano, suala la kukosekana kwa *consortium agreement* kati ya Richmond Development Company LLC na Pratt & Whitney halikuwasumbua kabisa wajumbe wa Kamati ya Serikali ya Majadiliano. Wajumbe hao, akiwemo mwakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, waliichukulia *business card* ya Bwana John Perun na mkataba wa kubadilishana taarifa kati ya kampuni hizo mbili kuwa ndio ushahidi wa ubia. GNT ilishindwa hata kusisitiza kuwa ubia wa kampuni hizo uwekwe wazi katika mkataba.

Aidha, kwa kuelewa kuwa Richmond Development Company LLC haikufanyiwa uchunguzi wa awali *(due diligence)* GNT ilishindwa kupendekeza kwa Serikali umuhimu wa kuifanyia Kampuni hiyo uchunguzi baada ya kuiteua *(post-qualification)* kujua uwezo wake kifedha, kiutendaji, kiutalaam na kiuzoefu. Katika mahojiano na Wajumbe wa GNT, Kamati Teule iligundua kuwa walipitisha masuala mengi kwa mazoea tu, baadhi yao wakiamini kuwa mikataba ya aina hiyo inatoka Benki ya Dunia na vipengele vyake havibadiliki.[26] GNT ilifika mahali ikakubali bila vigezo vya kueleweka, faini ya mzabuni/mkandarasi ya Dola 10,000 kwa siku kwa kuchelewesha utekelezaji wa mradi.

[26] Taarifa Rasmi za Bunge HANSARD ya tarehe 28 na 30/11/07 – mahojiano na Ndugu G.Makia na Chidowu.

Tarehe 19 Juni, 2006, Bodi ya Zabuni ya TANESCO ilikutana na kupitisha uamuzi rasmi wa kufuta zabuni waliyokuwa wanashughulikia awali na kutangaza kuwa "TANESCO isihusishwe na mkataba wowote utakaotokana na nyaraka za zabuni waliyoifuta".[27]

Siku hiyo hiyo ya tarehe 19 Juni 2006, Waziri wa Nishati na Madini alimwandikia dokezo Waziri Mkuu Mhe. Edward Ngoyai Lowassa, (Mb) kuwa majadiliano ya awali na Richmond Development Company LLC yamekamilika hivyo Serikali iiteue Kampuni hiyo kwa lengo la kuingia mkataba na TANESCO wa kuzalisha umeme wa dharura kwa miaka miwili. Sehemu ya barua hiyo inasomeka:

> *"Kamati ya Serikali ya Majadiliano (GNT) inayojumuisha wataalam kutoka Wizara Fedha, Wizara ya Nishati na Madini, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Benki Kuu na TANESCO ilifanya majadiliano na Richmond Development Company LLC ya Houston, Marekani kutoka tarehe 8 hadi 16 Juni 2006, kwa kuzingatia maelekezo yako."*[28] *(msisitizo tumeongezea)*

Tarehe 21 Juni 2006, Katibu wa Waziri Mkuu Ndugu B. Olekuyan aliiandikia Wizara ya Nishati na Madini kuitaarifu kuwa Mhe. Waziri

[27] Kumbukumbu za kikao cha Bodi ya Zabuni ya TANESCO, tarehe19/06/06
[28] Dokezo Na. CDB 286/397/01 la tarehe 17/06/06

Mkuu amekubali mapendekezo na ushauri wa Waziri wa Nishati na Madini.[29]

Siku hiyo hiyo tarehe 21 Juni 2006, Waziri wa Nishati na Madini akamwandikia dokezo Katibu Mkuu wake aiagize TANESCO iingie mkataba mara moja na Richmond Development Company LLC baada ya Waziri Mkuu kuidhinisha mapendekezo ya Wizara.[30]

Muda mfupi baadaye, kwa kutekeleza agizo la Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini akamwandikia barua Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO Balozi Fulgence Kazaura kumwagiza ahakikishe kuwa TANESCO inasaini mkataba na Richmond Development Company LLC:

> *"Kwa barua hii Serikali inaiagiza TANESCO iingie mkataba na Kampuni ya Richmond ili mitambo iletwe na kuanza kuzalisha umeme haraka iwezekanavyo. TANESCO inawajibika kuzingatia makubaliano yaliyofikiwa kati ya Richmond na Kamati ya Majadiliano ya Serikali (GNT)."*[31]

Ijumaa ya tarehe 23 Juni 2006, Kaimu Mkurugenzi Mwendeshaji wa TANESCO, Bwana Johannes .G. Lottering, aliitwa Wizara ya Nishati na Madini na kuagizwa kusaini Mkataba huo kati ya TANESCO na

[29] Barua Kumb. Na. 1/CEA 136/444/01 ya tarehe 21/06/06
[30] Dokezo Na. CAB.286/397/01 la tarehe 21/06/06
[31] Barua Kumb. Na. CBD.88/286/01 ya tarehe 21/06/06

Richmond Development Company LLC. Pamoja na kusita kwake, hatimaye alisaini mkataba huo.[32]

Kamati Teule inaelewa hisia walizokuwa nazo viongozi wa ngazi mbalimbali wa TANESCO kutokana na uongozi wa kiimla wa Wizara. Tulichokiona hapo juu kwa maana ya mchakato wa Zabuni kuchukuliwa na Wizara, ulikuwa ni ukiukwaji wa sheria na utaratibu mzima wa uwajibikaji. Pamoja na dharura iliyokuwa inailikabili Taifa, Serikali haiwezi kuwa kinara wa kuvunja sheria za nchi. Ni maoni ya Kamati Teule kuwa Wizara ilikiuka siyo tu masharti ya sheria na kanuni za ununuzi wa umma, bali vilevile maagizo mbalimbali ya Baraza la Mawaziri. Kamati Teule isingelikerwa sana na matukio haya kama Wizara ambayo ni taasisi ya ununuzi (*procurement entity*) kama ilivyo TANESCO, ingemalizia mchakato wake kwa kusaini mkataba huo yenyewe. Kuishinikiza TANESCO kusaini mkataba ambao vyombo vyake halali vilikuwa havijaupitia, ni udhalilishaji wa vyombo vya maamuzi ndani ya TANESCO na upotoshaji wa hali ya juu wa taratibu za kazi na sheria. Inashangaza kuwa baada ya kudhalilishwa na Wizara kwa kiwango hicho, chombo kikuu cha maamuzi cha TANESCO, yaani Bodi ya Wakurugenzi, haikuchukua hatua ya heshima ya kujiuzulu.

Kamati Teule ilishindwa kujua chanzo halisi cha ubabe, ujeuri na kiburi cha Wizara ya Nishati na Madini kama tulivyoshuhudia, kiasi cha kupindisha hata maamuzi ya Baraza la Mawaziri bila wasiwasi

[32] Taarifa Rasmi za Bunge HANSARD ya tarehe 06/12/07 – mahojiano na Bwana J.G Lottering

wowote, kukaidi ushauri wa kitaalamu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma mara tatu mfululizo kinyume na maagizo ya Baraza la Mawaziri lililotaka Sheria ya Ununuzi wa Umma izingatiwe, kukiuka sheria kwa makusudi kwa kuingilia mchakato wa zabuni wa taasisi nyingine ya ununuzi, kuvipuuza vyombo vya ndani vya maamuzi vya TANESCO (Bodi ya Wakurugenzi, Bodi ya Zabuni n.k), kuilazimisha Bodi ya Menejimenti ya TANESCO kuridhia maamuzi yaliyofanywa na Wizara ya kuibeba Richmond Development Company LLC kinyume cha sheria na taratibu, n.k.

Baadhi ya mashahidi, wakiwemo waandishi wa habari mashuhuri nchini, waliinyooshea kidole Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa msingi wa ubabe uliokithiri wa Wizara ya Nishati na Madini katika kuibeba Richmond.[33] Aidha, baadhi ya nyaraka ambazo Kamati Teule ilizipata katika uchunguzi wake zinaonesha kuwa maelekezo na maamuzi mengi ya msingi yalikuwa yanafanywa na Waziri Mkuu badala ya Wizara. Mfano ni barua kutoka Wizara ya Nishati na Madini kwenda kwa Waziri Mkuu tuliyoinukuu ukurasa wa 33 wa taarifa hii, ikitamka wazi kuwa GNT ilifanya majadiliano na Richmond Development Company LLC tarehe 8 hadi 16 Juni 2006 "kwa kuzingatia maelekezo" ya Waziri Mkuu. Tarehe 13 Julai 2006 Waziri wa Nishati na Madini akamwandikia Katibu Mkuu wake kuwa, "Nimezungumza tena na Mheshimiwa Waziri Mkuu leo juu ya bei ya mitambo ya Aggreko. Msimamo ni ule ule niliokueleza awali na

[33] Taarifa Rasmi za Bunge HANSARD ya tarehe 15/12/2007 – Mahojiano na Saed Kubenea. Vilevile mazungumzo nje ya kiapo na waandishi wa habari Mbarak Islam na Zeno Mrina wa Ino Communication.

ameagiza tuulizie Richmond kama anaweza kutoa 40 MW kwa bei isiyozidi ile ile ya 4.99 cents per kWh na kama tunaweza kuipata basi achukuliwe Richmond".

Ushiriki huu wa karibu wa Waziri Mkuu katika kila hatua ya zabuni ya umeme wa dharura, si lazima uwe ushahidi wa kwamba kiongozi huyo wa kitaifa alihusika katika kuibeba Richmond. Unaweza pia ukawa ushahidi wa staili ya kawaida kabisa ya Waziri Mkuu katika kufuatilia masuala yote ya kitaifa kwa karibu sana tukizingatia kwamba nchi wakati huo ilikuwa katika kipindi kigumu sana cha ukosefu wa umeme. Watu pekee waliokuwa wanaujua ukweli wenyewe, ukweli ambao ungeipa Kamati Teule msingi wa kumhoji Waziri Mkuu kwa kiapo, walikuwa watatu: Waziri Dk. Msabaha (Mb), Katibu Mkuu Mwakapugi na Mwenyekiti wa Bodi Balozi Kazaura.

Kamati Teule ikawaita kwa mara ya pili Mhe. Dk. Ibrahim Msabaha (Mb) na Ndugu Arthur Mwakapugi kwa mahojiano zaidi. Wote wawili, wakiwa ndani ya kiapo, walikataa katakata kupokea maagizo kutoka kwa Waziri Mkuu ya kuipa Richmond upendeleo. Lakini Mhe. Dk. Ibrahim Msabaha (Mb), baada ya mahojiano chini ya kiapo, akaiuma sikio Kamati Teule kuwa katika suala hilo yeye atakuwa kondoo wa kafara tu au, kwa maneno yake mwenyewe, "Bangusilo" kwa lugha ya Kizaramo. Maelezo hayo ya ziada ya Mhe. Waziri nje ya kiapo yalioana na maelezo aliyoyatoa Balozi Kazaura nje ya kiapo tarehe 30 Novemba, 2007 ambapo mara baada ya

kumaliza mahojiano na Kamati Teule kwa kiapo, Balozi akatoa maelezo ya ziada kuwa Richmond ilikuwa mradi wa "Bwana Mkubwa" na "mshirika wake mkubwa kibiashara", akimaanisha Mhe. Waziri Mkuu na Mhe. Rostam Aziz (Mb). Hii haikuwa mara ya kwanza kwa Balozi Kazaura kuuhusisha uteuzi wa Richmond Development Company LLC na mkono wa Waziri Mkuu. Mara ya kwanza ilikuwa Januari 2007 mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara.

Tumelazimika kueleza hata mambo tuliyoelezwa kwa siri kiungwana *(in confidence)* kutokana na uzito wa suala lenyewe na dhamana kubwa tuliyopewa na Bunge ya kuelezea kilichotokea kwa uwazi na ukweli. Lakini ushahidi huu wa ziada na nje ya kiapo wa viongozi hawa wawili, haukutoa msaada stahili kwa Kamati Teule kwa kuwa msingi wa maamuzi yote ya Bunge si minong'ono au tetesi, bali taarifa zenye uthibitisho halisi.

Ni dhahiri kuwa, kwa watumishi hao "waaminifu" wa Serikali, isingelikuwa rahisi kumtaja Waziri Mkuu chini ya kiapo. Hatua hiyo inahitaji ujasiri mkubwa na uzalendo wa hali ya juu. Pamoja na woga uliokuwa dhahiri kwa watumishi hao, ushahidi wa maandishi, wa mdomo na wa kimazingira ambao Kamati Teule iliupata kutoka kwa mashahidi mbalimbali, unatosha kumuhusisha Waziri Mkuu katika suala hili la Richmond na haumweki mahali pazuri kisiasa na kimadaraka. Uvumi wa kuhusika kwa Waziri Mkuu mwenyewe moja kwa moja na baadhi ya washirika wake wa karibu umeenea nchini

kwa kiwango cha kushangaza. Kamati Teule inaelewa kuwa uvumi huo unaweza kuwa umechangiwa na mahasimu wake kisiasa, lakini uharaka, urahisi na wepesi wa wananchi kuziamini tetesi hizo, unazua maswali mengi kuhusu imani, heshima na staha aliyojijengea yeye mwenyewe katika jamii.

3.0 MKATABA KATI YA TANESCO NA RICHMOND DEVELOPMENT COMPANY LLC

3.1 Madhumuni, Muundo na Muda wa Mkataba

Kama tulivyoona awali, Mkataba kati ya TANESCO na Richmond Development Company LLC hatimaye ulisainiwa na pande zinazohusika Jijini Dar-es-Salaam tarehe 23 Juni 2006. Madhumuni ya Mkataba yameainishwa wazi katika Utangulizi wa Mkataba kuwa ni kusambaza umeme wa dharura kwa kutumia mitambo ya kukodi ya kuzalisha umeme wa MW 105.6 kutokana na gesi.

Wanasheria waliokuwa kwenye GNT Ndugu Godson Makia na Ndugu Donald Chidowu waliiambia Kamati Teule kuwa vifungu vya masharti ya Mkataba huo vimenukuliwa kutoka kwenye Rasimu ya Mikataba ya Benki ya Dunia.[34] Taarifa hiyo haikuipendeza Kamati Teule kwani matarajio ya Taifa kwa wataalam wetu wanaposhiriki kwenye majadiliano ya aina hiyo siyo tu kuhamisha vifungu kutoka kwenye tovuti za taasisi za kimataifa bila kujali na kutafakari masharti ya mikataba hiyo kwa kuzingatia hali halisi ya mazingira yalivyo kwa manufaa ya Taifa.

Kamati Teule imebaini kuwa upo udhaifu, ukosefu wa mbinu na uzoefu katika kujadili mikataba *(contract negotiation skills)*.

[34] Majadiliano rasmi ya Bunge HANSARD ya tarehe 28 – 29/11/07

Aidha, Kamati Teule imeshangazwa na msimamo wa wataalam wetu wa kuheshimu maelekezo ya taasisi za kimataifa wakati kanuni za ununuzi *(Public Procurement Regulations GN. 97)* zilizotungwa chini ya sheria za ununuzi wa umma zinaelekeza kufuata mifumo ya mikataba iliyoandaliwa na PPRA. Kanuni ya 115 inatamka kwamba kila juhudi itafanywa kuhakikisha kuwa sampuli za mikataba ya ununuzi zilizoandaliwa na mamlaka zinatumika na pale ambapo rasimu zingine za mikataba nje ya mamlaka zinatakiwa kutumika, basi idhini ya Mamlaka na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itahitajika.

Pamoja na kwamba madhumuni ya msingi ya Mkataba huu ni kuzalisha na kusambaza umeme wa dharura *(emergency power supply)* muda wa mkataba huo ni miezi ishirini na minne (24)!

Tukirejea kwenye tangazo la zabuni la TANESCO, muda wa kukodi mitambo hiyo ilikuwa ni miezi kumi na mbili tu na muda huo ungeweza kuongezwa kutegemea hali ya uzalishaji umeme nchini. Hata hivyo, muda huo uliongezwa na GNT na kuwa miezi ishirini na nne. Swali linalojitokeza ni kwamba, GNT ilikuwa inakimbilia wapi kuongeza muda wa kukodi mitambo hiyo kutoka miezi kumi na mbili mpaka ishirini na nne wakati kulikuwa na fursa ya kuongeza muda pale inapobidi?

Kwa kuwa madhumuni ya Mkataba huu ilikuwa ni kuzalisha umeme wa dharura, Serikali ilipaswa kutilia maanani hali ya kuongezeka

kwa maji katika mabwawa yaliyoko nchini ili kuona umuhimu wa kuongeza au kutoongeza muda wakati wa ukomo wake. Uamuzi wa kuongeza muda kabla ya kutathmini hali ya uzalishaji umeme kwa njia ya maji zaidi ya kipindi cha mwaka mmoja kilichokusudiwa awali, unatia mashaka. Ukweli ni kwamba maji katika mabwawa nchini yalikuwa yameshajaa mapema Januari, 2007 na muda wa awali wa kuisha Mkataba ungekuwa tarehe 11/9/2008; hivyo ingekuwepo nafasi ya kutosha kuamua kuongeza au kutoongeza muda wa mkataba.

Kamati Teule inasisitiza kuwa, udharura wa mradi huu ulimalizika pale mabwawa yetu yalipojaa maji mapema mwezi Februari 2007, hivyo kitendo cha TANESCO kukubali mkataba kuhaulishwa bila marekebisho kimewashangaza hata hao waliohaulishiwa mkataba huo.[35] Hii pia inaonyesha udhaifu kwa watendaji wetu kushindwa kuona fursa iliyokuwa wazi katika kifungu 12.3 cha mkataba ambacho kingeiwezesha TANESCO kuvunja mkataba bila ya kupata hasara. Matokeo yake TANESCO imeingia kwenye gharama kubwa ya kulipa *capacity charge* na gharama nyinginezo, wakati huo huo ikizingatiwa kuwa mitambo hiyo inatumika chini ya kiwango kilichokusudiwa au kutotumika kabisa *(under utilization)* kutokana na mabwawa yetu kuzalisha umeme wa bei nafuu ukilinganisha na bei ya umeme huo wa kukodi.

[35] Majadiliano rasmi ya Bunge HANSARD ya tarehe 27/12/07 – mahojiano na Mkurugenzi Mwendeshaji wa Dowans Holdings S.A Bwana Gui Picard

Kwa ujumla muda wa kumalizika kwa mkataba huu una utata mkubwa. Utata wenyewe unatokana na ukweli kwamba kwa mujibu wa kifungu cha 15.18 mkataba unaanza siku moja baada ya kufunguliwa Barua ya Dhamana ya Benki (Letter of Credit - LC) ambayo ni tarehe 12/09/2006 hivyo mkataba huu ungeisha muda wake tarehe 11/09/2008. Iwapo tarehe ya awali ya kuzindua mitambo hiyo (Commercial Operational Date - COD) yaani tarehe 2/2/2007 ingekuwa ndio msingi wa kuanza mkataba huu, basi mkataba huu ungeisha tarehe 2/2/2009. Aidha, kwa kufuata tarehe ya sasa ya COD yaani tarehe 4/10/2007 mkataba huo utaishia tarehe 4/10/2009. Kutokana na hali hiyo, kutakuwa na ongezeko la muda wa mkataba kwa miezi 13 ikizingatiwa mkataba ungeanza tarehe 12/09/2006. Kamati Teule imebaini kuwa ongezeko hilo linaliongezea Taifa mzigo wa kiasi cha Dola za Kimarekani 47.5 millioni au Tsh. 59.375 bilioni kutokana na malipo ya *capacity charge*.

3.2 Malipo ya Kodi

Kwa mujibu wa Kifungu cha 3.4 cha Mkataba, TANESCO inawajibika kulipia kodi zote zinazotakiwa kulipwa na Richmond Development Company LLC kwa mujibu wa Sheria, pamoja na malipo mengine yanayohusiana na uingizaji nchini na utoaji nje ya nchi mitambo husika, ikiwa ni pamoja na vifaa, vipuri n.k. vya mitambo hii.

Kifungu hicho kinasomeka kama ifuatavyo:

> "*All taxes and charges arising in relation to the importation and exportation of the plant, equipment, tools, spare parts, consumables, testing and monitoring equipment or in connection with the supplier's performance of its obligations under this Agreement generally that become due in accordance with the laws of Tanzania shall be paid for by TANESCO at its sole cost and expense".*

Tafsiri ya Kifungu hiki cha mkataba ni kwamba, Richmond Development Company LLC inalipiwa kodi zote zinazohusiana na utekelezaji wa wajibu wake chini ya Mkataba huo, hata pale ambapo itaamua kuihamishia mitambo yake nchi nyingine.

Kwa maoni ya Kamati Teule kifungu hiki cha Mkataba kinatoa unafuu usiostahili katika hali ya kawaida, au kwa namna yoyote ile, kwa Richmond Development Company LLC na kuibebesha TANESCO mzigo wa kulipia kodi isizostahili.

Vilevile, masharti ya Kifungu hiki yanaifanya TANESCO ibebe mzigo wa kulipia kodi zinazohusika na uendeshaji (*operations*) na matengenezo (*maintenance*) ya mitambo ya Richmond Development Company LLC kutokana na hoja kwamba, uendeshaji na matengenezo ya mitambo vimetafsiriwa kama shughuli ambazo zinahusiana na utekelezaji wa majukumu ya Richmond Development

Company LLC chini ya Mkataba *(in connection with the supplier's performance of its obligations under the Agreement).*

Kwa wigo wa tafsiri ya majukumu haya, TANESCO inawajibika kulipa hata gharama za Bima, ada za mawakili wa wawekezaji hawa, gharama ambazo TANESCO haina uwezo wa kuzisimamia wala kuzipunguza.

3.3 Malipo mengine

Kwa mujibu wa Mkataba, TANESCO ina wajibu wa kufanya malipo yafuatayo kwa Richmond Development Company LLC kuanzia tarehe ya kuanza uzalishaji (COD):

(i) Malipo ya umeme unaotumiwa *(energy purchase price)* – Dola za Kimarekani 0.0499 kwa kWh.[36] au Shilingi za Kitanzania 62.375 kwa kWh, na

(ii) Gharama za kudumu za uwezo wa mitambo (*capacity charge)* Dola za Marekani 34.60565 kwa kW kwa mwezi au Shilingi za Kitanzania 43,257.063 kwa kW. Malipo haya yanafanywa hata pale ambapo mitambo ya Richmond Development Company LLC haizalishi umeme.[37]

[36] Tafsiri ya Interim Energy Purchase Price ukurasa wa 3 wa Mkataba
[37] Kifungu 4.2 na Nyongeza C ya Mkataba

3.4 Kuhaulisha Mkataba

Mkataba huu una kifungu cha 15.12 kinachoruhusu wahusika wa Mkataba huu kuhaulisha haki na majukumu yao chini ya Mkataba kwa chombo kingine chochote walichokiteua lakini kwa makubaliano ya pande zote mbili.

Kitendo cha kuweka kipengele cha kuhaulisha Mkataba, kinadhihirisha moja kwa moja woga wa Wizara ilioujadili na kuuidhinisha mkataba huu wa kutokuwa na uhakika na utendaji wa wazabuni inaowachagua. Vilevile kinaruhusu biashara ndani ya mkataba, biashara ambayo Serikali haina udhibiti nayo kwa maana ya kujua hulka na usalama wa mrithi wa mzabuni. Kamati Teule haioni mantiki ya kuhaulisha mkataba wakati mtoa huduma ameshindwa kutekeleza masharti ya mkataba.

3.5 Fidia kwa Kuchelewa kutekeleza Mkataba

Kwa mujibu wa Kifungu cha 4.4 cha Mkataba, Richmond Development Company LLC inawajibika kuilipa TANESCO Dola za Kimarekani 10,000 (Tsh.12.5 milioni) kwa siku kwa ucheleweshaji wa kuanza kuzalisha umeme kulingana na tarehe iliyowekwa katika Mkataba.

Wataalam walipotakiwa kueleza jinsi walivyofikia kiwango hicho, walitoa maelezo kuwa walifuata viwango vya kimataifa kutoka kwa

wataalam wao *(Consultants)* bila kutumia vigezo vyovyote vinavyohalalisha kiwango hicho.[38]

Kamati Teule imebaini kuwa malipo ya Dola za Kimarekani 10,000 kwa siku ni kidogo sana ukilinganisha na *capacity charge* ambayo TANESCO inalipa kwa siku kwa mwekezaji huyo. TANESCO ingeweza kurejesha kiwango kile kile ambacho Richmond Development Company LLC inalipwa inapokuwa haizalishi umeme, au kiwango ambacho TANESCO ingepata kutokana na mauzo ya umeme unaozalishwa kwa siku kwa bei ya TANESCO, au wangeweza kutumia *formula* ya haki *(fair deal)* ya wastani wa bei zao kwa siku.

Kwa mfano, Richmond Development Company LLC imechelewesha mradi kwa siku 243 kuanzia tarehe 2/2/07 hadi tarehe 2/10/2007. Fidia tunayodai kufuatana na mkataba ni Dola za Kimarekani 10,000 x 243 = 2,430,000 ambazo ni sawa na Tsh.3.037 bilioni tu. Endapo mradi huo ungecheleweshwa kwa miaka miwili wangetakiwa kulipa Dola za Kimarekani 10,000 x siku 365 x miaka 2 = Dola za Kimarekani 7.3 milioni (Tsh 9.125 bilioni tu).

Kwa mujibu wa mkataba, Richmond Development Company LLC inalipwa Dola za Kimarekani 121,811 (Tsh 152.264 milioni) kwa siku kama gharama za kudumu za uwezo wa mitambo yao *(capacity charge)*. Fedha hizi zinalipwa kila siku bila kujali kama Richmond Development Company LLC imezalisha umeme au la. Kwa msisitizo

[38] Taarifa rasmi za Bunge HANSARD ya tarehe 23/11, 30/11, 3/12/07

ni kwamba wakati sisi tunawalipa shilingi milioni 152.264 kwa siku, wao wanatulipa Tsh. milioni 12.5 kwa siku pale wanapotupa hasara kwa kutokuzalisha umeme kwa wakati. Hasara ambayo TANESCO ilipata kwa kukosa umeme inaweza kutambuliwa kwa kuangalia wastani wa bei inayowauzia wateja wake ambayo ni sawa na Dola za Kimarekani 0.07 au Tsh 87.5. Hivyo, ingekuwa halali kabisa kwa TANESCO kuidai Richmond Development Company LLC Tsh. milioni 228.657 kwa siku. Kamati Teule inaona tatizo kuu linalotukabili ni ukosefu wa mbinu za kibiashara, kutojiamini, kukosa umakini wa kitaaluma na ubinafsi upande wa maafisa wetu wanaojadili mikataba kwa niaba yetu.

3.6 **Ulinganisho na Mikataba Mingine**

Mzigo mkubwa ambao TANESCO inabeba chini ya mkataba wake na Richmond Development Company LLC unajirudia katika mikataba mingine kati ya TANESCO na makampuni mengine ya umeme kama vile IPTL, AGGREKO, ALSTOM na SONGAS.

Katika kuchambua mikataba mbalimbali ya kuzalisha umeme wa dharura wa muda mfupi na ile ya muda mrefu, Kamati Teule imebaini kuwa baadhi ya miradi imeigharimu Serikali pesa nyingi mno kulinganisha na mradi wenye uwezo sawa inayotumia nishati ya aina nyingine. Mfano halisi ni mradi wa Alstom Power Rentals na Aggreko International Project Ltd, hii yote inazalisha umeme wa MW

40 lakini inatofautiana kwa aina ya nishati ya uzalishaji (Angalia Jedwali II).

Mradi wa Alstom Power Rentals wenye *capacity charge* ya Dola za Kimarekani milioni 21.9 (Tsh. 27.375 bilioni) umegharimu Serikali jumla ya Dola za Kimarekani milioni 130.181 (Tsh. 162.726 bilioni) kwa mwaka mmoja. Hii ni pamoja na gharama za dizeli kwa uendeshaji wa mtambo huo. Mradi wa AGGREKO wenye *capacity charge* ya Dola za Kimarekani milioni 17.437 (Tsh.21.796 bilioni) umeigharimu Serikali jumla ya Dola za Kimarekani milioni 28.860 (Tsh. 36.075 bilioni) pamoja na gharama ya gesi kwa mwaka mmoja.

Kwa kubaini mzigo mkubwa wa gharama hizo uliosababishwa hasa na nishati ya diesel na kwa kuzingatia utajiri wa nishati ya gesi tuliyobarikiwa kuwa nao, Kamati Teule inashauri njia mbadala ambayo inaweza kutumika ili kuokoa gharama hizo za dizeli hasa kwa vile sehemu nyingi za pembezoni mwa Tanzania zinatumia mitambo ya mafuta na haijaunganishwa na Gridi Kuu ya Taifa (Msongo Mkuu wa Umeme).

Kamati Teule imeshuhudia matumizi ya gesi asilia inayohifadhiwa katika visima vya gesi (gas wells). Gesi hiyo husafirishwa mahali husika kwa kutumia trailers maalum. (Angalia Jedwali Na I).

Kutokana na takwimu tulizozipata, mradi wa Mwanza wa Alstom endapo ungetumia gesi tungeweza kunusuru jumla ya Dola za

Kimarekani 68.294 (Tsh. Bilioni 85.4) kwa mwaka wa kwanza na tungeepukana na gharama za *capacity charge* ya kila mwezi. Wakati huo huo mitambo hiyo itabaki kuwa mali yetu. (Angalia uchambuzi wa kimahesabu baada ya Jedwali Na. I & II).

JEDWALI Na. I

	MAELEZO	**KIPIMO**	**BEI (US $)**
1	Mtambo wa kuzalisha umeme aina ya GPB180 kwa kutumia nishati ya gesi asilia	17.5 MW	7,500,000
2	Compressed Natural Gas tanks CNG Tank Trailer and Truck kwa matumizi ya siku 7 kwa mtambo wa GPB180 DOT 3AAX-2400 tubes	167000ceft	449,250
3	Tank ya kufukia ardhini OCTA Burying Tank No…	500PSI	2,500,000

JEDWALI Na. II

	KAMPUNI	**NISHATI**	**MW**	**CAPACITY CHARGE KWA MWAKA (US$)**	**GHARAMA ZA GESI KWA MWAKA (US$)**	**JUMLA YA GHARAMA KWA MWAKA (US$)**
1	Richmond Development Company LLC	Gesi	105.6	43,852,283	30.156,826	74,009,109
2	Aggreko International Projects	Gesi	40	17,437,055	11,423,040	28,860,095
3	Alstom Power Rentals	Dizeli	40	21,900,000	108,280,000	130,180,000

- Jedwali hili hapo juu limepatikana kutokana na *capacity charge* kwa mwaka kama inavyoonekana katika mikataba husika.
- Bei ya gesi ambayo mitambo ya Dowans inatumia kwa sasa ni Dola za Kimarekani 0.0326/kW (TANESCO,2007).

  Mfano: Matumizi ya gesi kwa mtambo wa 40 MW wa Aggreko kwa mwaka:

  US$ 0.0326 x 40 kW.10^3 x 24hrs x 365

  kWx hrs

  US$ 11.423.040

- Ili uzalishe 40 MW unahitaji kuwa na mitambo mitatu ya PBG180 ambayo kwa ujumla wake itazalisha (17.5 MW x 3) MW 52.5 sawa na US$ 22,500,000.
- Kwa matumizi ya mtambo mmoja kwa mwezi unahitaji kuwa na OCTA 4 na mitambo mitatu ya PBG180 utahitaji kuwa na OCTA 12 ambayo sawa na US$ 30,000,000.
- Ili kujaza gesi ya kutosha kwa mwezi unahitaji kuwa na CNG Trailer na Truck 12 kwa mwezi yaani DOT.3AAX - 2400(US$ 449,250 x 12) sawa na US$ 5,391,000

Jumla	57,891,000
Usafirishaji 15%	8,683,650
Gharama za Ufungaji 10%	5,789,100
Gharama bila gesi ya uendeshaji	**72,363,750**

Pamoja na gharama za gesi kwa mwaka mmoja mtambo ungegharimu:

US$ 72,363,750

US$ 11,423,040

US$ 83,786,790

Kwa maana hiyo mtambo wa dizeli uliofungwa Mwanza ungeweza kunusuru gharama zifuatazo kama ungetumia mitambo ya gesi kwa bei tulizozigundua:

US$ 130,180,000-US$ 83,786,790 = US$ 46,394,210

Pamoja na *capacity charge* tungeweza kunusuru kiasi cha

US$ 46,394,210

US$ 21,900,000

US$ 68,294,210 au TSh. Bilioni 85.4

Angalia Vielelezo vya bei kutoka kwa watengenezaji.[39]

[39] Kabrasha la bei za mtambo wa CNG tanks pamoja na GPB 180 generators

JEDWALI III

MAELEZO		KAMPUNI		
		RICHMOND/ DOWANS	**AGGREKO**	**ALSTOM**
1.	Capacity Charge (US$ kwa kW kwa siku)	34.60565	35.928	43.8
2.	Energy Charge (US$ kwa Kwh) ;	0.0499	0.0499	0.0608
3.	Fidia kwa kucheleweshaMkataba (delay damages) (US$)	10,000 kwa siku kwa muda wote wa kucheleweshaMkataba	• 20,000 kwa siku (kwa muda wa mwezi mmoja tu) au • 40,000 (kwa siku baada ya Mwezi mmoja.Hata akichelewesha vipi hatalipa zaidi ya dola 350,000	57,600 kwa siku, na hata akichelewesha vipi hatalipa zaidi ya dola 400,000
4.	Malipo ya Kodi	TANESCO	TANESCO	Hakuna
5.	Incentives	Hakuna	Hakuna	Hakuna
6.	Matengenezo ya mitambo	TANESCO	TANESCO	ALSTOM (Annex I)
7.	Aina ya Nishati	Gesi	Gesi	Dizeli
8.	Masharti ya kuvunja Mkataba	Kifungu 12.3	Kifungu 12.3	Kifungu 12.3
9.	Muda wa Mkataba	Miaka 2	Miaka 2	Mwaka 1
10.	Kiwango cha Umeme (MW)	105.6	40	40
11.	Bei ya Mkataba (US $)	87,704,565	34,874,110	21,900,000
12.	Barua ya Dhamana ya Benki	30,696,598	7,051,699	7,000,000

JEDWALI IV

MAELEZO		KAMPUNI	
		IPTL	**SONGAS**
1.	Capacity Charge (US $ kwa kW)	Not fixed	6,638,600
2.	Energy Charge(US $ kwa kW)	Not fixed	*Formula* imetolewa
3.	Fida kwa kuchelewesha Mkataba(delay damages)(US $)	*Formula* imetolewa	*Formula* imetolewa
4.	Malipo ya Kodi	TANESCO	TANESCO
5.	Incentives	Bonus, Kifungu 5.4(b) na 6.5b)	Bonus, Kifungu 99(a)
6.	Matengenezo ya mitambo	TANESCO	TANESCO
7.	Aina ya Nishati	Mafuta mazito	Gesi
8.	Masharti ya kuvunja Mkataba	Kifungu 16.3	Kifungu 4.4
9.	Muda wa Mkataba	Miaka 20	Miaka 20
10.	Kiwango cha Umeme (MW)	100	80
11.	Bei ya Mkataba (US $)	TANESCO inabeba gharama ya *capacity charge*: na gharama nyingine ambazo TANESCO haiwezi kuzidhibiti kama vile Matengenezo, Bima, Mikopo na riba zake, na consultation fees	*Formula* imetolewa
12	Barua ya Dhamana ya Benki	Hawana	Hawana

Katika Jedwali III hapo juu, kifungu 4 cha mkataba kinaonyesha kuwa Richmond Development Company LLC inalipa kidogo ukilinganisha na bei zinazoonekana kwa wenzake yaani Aggreko na Alstom. Lakini Richmond Development Company LLC itatakiwa

kulipa kiwango hicho kwa muda wote itakaochelewesha, wakati Aggreko itaonekana kuwa na *capacity charge* kubwa kwa siku jambo ambalo unaweza kudhani kuwa kilikuwa ni kifungu kizuri. Lakini kutokana na ujanja unaofanyika wakati wa majadiliano ya mkataba, wenye mitambo hao wanakuwa wameshajilinda kwa kuweka kifungu Na. 10.1[40] ambacho kinaweka ukomo wa kulipa gharama ambazo ukitathmini utagundua kuwa vifungu hivyo vinatoa na kutwaa upande wa pili. Vivyo hivyo ndivyo ilivyo katika Mkataba wa Alstom Power Rentals.

Kamati Teule imejifunza kuwa gharama za matengenezo ya mitambo kwa baadhi ya wamiliki hao zimebebeshwa TANESCO. Mikataba mingine kama IPTL ndiyo kiboko yetu maana hata vipuri, bima na riba zao nazo zinalipwa na TANESCO.

Wakati wengine wanahangaika kulinusuru Taifa hili kutoka kwenye wimbi la umaskini, watu wachache wanawarudisha nyuma kutokana na kutokuwa makini, kazi za zima moto *(emergency)* na kutotumia utaalam stahili.

Mikataba yote ukiiangalia utagundua kuwa inasababisha mzigo mkubwa kwa TANESCO kwani sehemu kubwa ya makusanyo ya Shirika hili yanatumika kulipia gharama za wawekezaji hao.

[40] Angalia Mkataba wa AGGREKO

Sambamba na mikataba ya kuzalisha umeme TANESCO imekuwa ikibebeshwa mizigo kutokana na maamuzi ya haraka kutoka Wizarani kwa mfano mkataba wa menejiment wa Net Group Solution (PTY) ambao kwa kiwango kikubwa umechangia hasara kubwa kwa Taifa kutokana na kampuni hiyo kujitahidi kubana matumizi ili ipate faida itakayowapelekea kupata *bonus*. Lakini pia katika mchakato huo Wizara imeonesha dhahiri kuwa haikuwa katika mawasiliano mazuri na kampuni hiyo ya Net Group Solution (PTY) hasa katika kipindi cha mchakato wa kumpata mzabuni wa umeme wa muda (2006). Net Group Solutions (PTY) iliingizwa nchini (kuiendesha TANESCO) na Serikali yenyewe tena kwa ulinzi mkali wa mtutu wa bunduki.

Kamati Teule ilipata taarifa kuwa hata gesi iliyopo haitoshelezi kuwasha mitambo yote kwa mara moja hivyo kuifanya kampuni ya sasa ya Dowans Holdings S.A kushindwa kuendesha mitambo yake yote kwa wakati wote. Swali la Kamati Teule ni kwa nini Wizara iliamua kuwekeza haraka kwenye mitambo yenye uwezo mkubwa wakati hakuna Gesi ya kutosha? Je huo sio uharibifu wa pesa ya Watanzania hata kama ilitokana na kupunguziwa madeni? Kama pesa hizo zingepona je zisingesaidia kufanya kazi nyingine?

3.7 Uzingatiaji wa mkataba huu katika kutekeleza sheria ya CRB na ERB

Kwa mujibu wa Sheria ya Usajili wa Wahandisi ya 1997 (Na. 15 ya Mwaka 1997) wahandisi wote wanaofanya kazi hapa nchini wawe ni Watanzania au kutoka nje wanatakiwa kusajiliwa na Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB). Kwa wale wanaotoka nje wanatakiwa kusajiliwa na Bodi wakiwa nje kabla ya kuingia nchini au mara tu wanapoingia nchini. Utafiti tulioufanya kutoka ERB kama inavyothibitishwa katika Hansard ya Kikao cha kwanza cha Kamati Teule cha tarehe 27 Novemba 2007 umebainisha kuwa ERB haikupokea maombi yeyote ya kusajili wahandisi kutoka Richmond Development Company LLC. Na wala ERB haijui kuwa kampuni hiyo ilikuwa *contractor* au *supplier*.

Vilevile kwa mujibu wa Sheria Bodi ya Usajili wa Makandarasi ya 1997 (Na.17 ya Mwaka 1997) iliyounda Bodi ya Usajili ya Makandarasi, Bodi hiyo imepewa majukumu yafuatayo:

- Kusajili Makandarasi wa aina zote,
- Kuratibu tabia na mwenendo wao, na
- Kuendeleza Makandarasi wa Tanzania.

Vilevile Bodi hiyo inasajili makandarasi wa kudumu na makandarasi wa muda. Sheria ya Ununuzi wa Umma[41] inaruhusu kampuni ya nje kupeleka zabuni yake na kupewa kazi kabla ya kusajiliwa. Aidha,

[41] Kifungu 46

sheria hiyo ina kipengele ambacho kinairuhusu Bodi kusajili kampuni hiyo kwa muda kwa ajili ya kutekeleza mradi mahsusi.

Kwa upande wake Richmond Development Company LLC ilipewa kazi kwa kutumia kipengele hicho. Bodi ilipogundua ilikwenda TANESCO kuonana na uongozi wa juu kuitaka kampuni hiyo isajiliwe ili kukamilisha taratibu za sheria zilizoainishwa katika Mkataba iliyousaini. Hata hivyo kampuni hiyo kupitia TANESCO ilidai kuwa Mkataba waliousaini unawatambua wao kama *"Supplier"* na siyo *"Contrator"*, jambo ambalo lilikuwa linakinzana na sheria ya CRB, 1997, inayosema kwamba mtu yeyote anaye-*supply* na ku-i*nstall* ni mkandarasi.[42]

Baada ya CRB kuandika barua ya kutaka kuipeleka mahakamani Richmond Development Company LLC, Maafisa kutoka Wizara ya Nishati na Madini na TANESCO walikwenda kwenye Ofisi ya Msajili wa Makandarasi kwa lengo la kuijengea kampuni hiyo utetezi ili ipewe muda zaidi.

Hadi Richmond Development Company LLC inahaulisha mkataba wake kwa Dowans Holdings (T) Limited ilikuwa haijasajiliwa na Bodi hiyo wala wahandisi wake kusajiliwa na ERB. Huku ni kutoheshimu sheria na taratibu za nchi.

[42] Taarifa rasmi za Bunge HANSARD tarehe 27/11/2007 - Majadiliano na Eng. Muhegi.

4.0 UTEKELEZAJI WA MKATABA

4.1 Barua ya Dhamana ya Benki (Letter of Credit)

Barua ya Dhamana ya Benki ni mpango wa usimamizi wa huduma za malipo kati ya Benki na Mteja wake katika biashara inayohusu uingizaji au usafirishaji wa mali au huduma kuingia au kutoka ndani au nje ya nchi. Barua ya Dhamana ya Benki inamlinda msafirishaji wa bidhaa au huduma kupata uhakika wa malipo yake na pia kumlinda mnunuzi au anayepokea huduma kupata mali anayokusudia kwa thamani ya fedha zake.

Katika Mkataba kati ya TANESCO na Richmond Development Company LLC, TANESCO ilihitaji huduma za uzalishaji umeme wa dharura kutoka kwa Richmond Development Company LLC kwa uzalishaji wa wastani wa MW 105.6 kwa mwezi kwa makubaliano kwamba Richmond Development Company LLC italeta nchini Tanzania mitambo mitano yenye uwezo wa kuzalisha umeme kwa wastani usiopungua MW 22 kila moja, na wakati huo huo Richmond Development Company LLC ilihitaji uthibitisho wa malipo ya gharama za kuwekeza mitambo hiyo *(capacity charge)* na gharama za matumizi halisi ya umeme utakaozalishwa na kuuzwa kwa TANESCO *(energy charge)*, kila mwezi, kwa kipindi cha miaka miwili. TANESCO pia ilitakiwa kulipia gharama za kuandaa na kusafirisha mitambo *(mobilization costs)* hadi eneo la kazi la TANESCO, Ubungo – Dar-es-Salaam, Tanzania.

Katika Mkataba huo masuala ya Barua ya Dhamana ya Benki yalizungumziwa katika Kifungu 4.5(c) kama ifuatavyo:-

Kifungu 4.5(c):

> *" . . . For the mobilization costs a Letter of Credit (LC) shall be established within seven days after signing of the contract. TANESCO, BOT, MoF and RDVECO shall jointly agree on the terms and conditions." (*Barua ya Dhamana ya Benki kulipia gharama za maandalizi na usafirishaji wa mitambo ya uzalishaji wa umeme itafunguliwa siku saba baada ya kutiwa saini kwa Mkataba, na kwamba TANESCO, Benki Kuu ya Tanzania, Wizara ya Fedha na Richmond Development Company LLC watakaa ili kukubaliana masharti ya Barua ya Dhamana ya Benki).

Kifungu 15.18

> *"This Agreement shall become effective on the date following the day TANESCO establishes a Letter of Credit as commitment for partial payment of mobilization arrangements. Terms and conditions of Letter of Credit shall be negotiated by the parties".* (Mkataba kati ya TANESCO na Richmond Development Company LLC utaanza rasmi siku ambayo TANESCO imefungua rasmi Barua ya Dhamana ya Benki

kama sehemu ya uwezeshaji wa taratibu za usafirishaji wa mitambo.)

Kifungu hiki kinaleta utata wa tarehe ya kuanza kwa Mkataba. Tarehe hiyo inaweza kuchukuliwa kuwa ni siku inayofuata baada ya TANESCO kufungua Barua ya Dhamana ya Benki au tarehe ambayo TANESCO na Richmond Development Company LLC watafikia makubaliano kuhusu masharti ya Barua ya Dhamana ya Benki.

Katika Kamati ya Serikali ya Majadiliano *(GNT)* ilikubalika kwamba:-

(i) Mitambo itasafirishwa kwa awamu mbili,
(ii) Malipo ya awali yatakayolipwa yatafidiwa kutoka katika malipo ya *capacity charge* kwa mafungu sawa ndani ya miezi 24 ya Mkataba.
(iii) Masharti ya Barua ya Dhamana ya Benki yatajadiliwa na wahusika *(parties)* wa Mkataba.[43]

Gharama zilizoainishwa hapo juu zitalipwa kwa fedha za mfuko maalum uliojulikana kama *Multilateral Debt Relief Initiative (MDRI)* kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ambayo ilitoa angalizo kuhusu masharti maalum kwa TANESCO ili kuiwezesha Benki inayosimamia malipo haya kulipwa chini ya utekelezaji wa Mkataba wa uzalishaji wa umeme wa dharura kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT). Katika

[43] Kumbukumbu za kikao cha Kamati ya Serikali ya Majadiliano (GNT) tarehe 8 – 15 Juni, 2006.

angalizo hilo Benki Kuu ya Tanzania iliagiza kwamba malipo stahili yafanyike kwa kufungua Barua ya Dhamana ya Benki kupitia Benki ya CRDB (Tanzania) Ltd au Citibank (Tanzania) Ltd kwa kuzingatia masharti yote chini ya utaratibu wa ufunguaji wa Barua ya Dhamana ya Benki wa Kimataifa *(Uniform Customs Practice – UCP* 500*)* kwa mfumo maalum wa *International Chamber of Commerce (ICC)*, na kwamba thamani ya Barua ya Dhamana ya Benki ni kiasi cha Dola za Kimarekani 30,696,598.00. Maana yake ni kwamba Richmond Development Company LLC inatengewa kulipwa fedha hizo kabla ya kuanza uzalishaji wa umeme wa dharura *(Advance Payment).*

Thamani hii ya Barua ya Dhamana ya Benki ni sawa na asilimia 35 ya thamani ya malipo ya Mkataba kwa kipindi cha miaka miwili. Aidha, hakuna mabadiliko yoyote yatakayoruhusiwa kufanywa katika Barua ya Dhamana ya Benki bila kutolewa idhini ya maandishi kutoka Benki ya CRDB (Tanzania) Ltd, TANESCO na Benki Kuu ya Tanzania.[44]

Kamati Teule imeona kwamba mojawapo ya masharti ya kufungua Barua ya Dhamana ya Benki ni kuwa TANESCO au Serikali ithibitishe kupitia Benki yake, CRDB Bank Limited, au Benki Kuu ya Tanzania kwamba katika akaunti maalum (Escrow) zipo fedha za kulipia gharama husika.

[44] *Letter of Undertaking* kati ya Benki Kuu ya Tanzania, Benki ya CRDB na TANESCO, iliyosainiwa tarehe 8 Septemba, 2006.

Mapendekezo ya ufunguaji wa Barua ya Dhamana ya Benki yalipitia katika mtiririko ufuatao:-

i. Maombi maalum ya kufunguliwa Barua ya Dhamana ya Benki kutoka Richmond Development Company LLC baada ya Mkataba kutiwa saini.
ii. Majadiliano na makubaliano ya kikao cha tarehe 7 Julai, 2006.
iii. Majadiliano na makubaliano ya kikao cha tarehe 27 Julai, 2006.
iv. Maombi ya kufanya marekebisho ya Barua ya Dhamana ya Benki toka kwa Richmond Development Company LLC kwenda TANESCO, Awamu ya kwanza hadi Awamu ya tatu.

4.2 Majadiliano na Makubaliano kuhusu Masharti ya Barua ya Dhamana ya Benki

4.2.1 Maombi ya Masharti ya Barua ya Dhamana ya Benki (Awamu ya Kwanza)

Ili kutekeleza masharti ya Kifungu 4.5(c) cha Mkataba, tarehe 3 Julai, 2006, Richmond Development Company LLC iliwasilisha TANESCO barua yenye mapendekezo ya masharti ya Barua ya

Dhamana ya Benki *(Awamu ya Kwanza)*[45] ikiambatanisha na Hati ya awali ya Madai (*Proforma Invoice)* ya Dola za Kimarekani milioni 30.7 (Tsh. 38.37 bilioni). Katika barua hiyo Richmond Development Company LLC ilipendekeza utaratibu wa malipo kuwa kama ifuatavyo:-

(i) Asilimia 35% ya mapato ya miaka miwili ya Mkataba kiasi cha Dola za Marekani milioni 30 (Ths. 37.5 bilioni) ilipwe kwa Richmond Development Company LLC kwa masharti yafuatayo:

(a) Kwanza ilipwe asilimia 50 ya thamani ya Barua ya Dhamana ya Benki kama malipo ya awali *(Advance Payment).*

(b) Kisha ilipwe asilimia 40 baada ya kuwasilisha hati za uthibitisho wa kusafirisha mitambo.

(c) Ilipwe asilimia 10 baada kutolewa hati ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ya uthibitisho wa kuwasili na kupakuliwa kwa mitambo *(Single Bill of Entry).*

(iii) Aidha, ilipendekeza kuwa Barua ya Dhamana ya Benki ifunguliwe katika Benki ya Citibank (Tanzania) ambayo kwa maelezo yao (Richmond Development Company LLC)

[45] Mapendekezo ya Barua ya Dhamana ya Benki kutoka Richmond Development Company LLC 3/7/2006

ni kuwa tayari wamekwishafanya majadiliano na Citibank wamekubali kutekeleza jukumu hilo.

Kwa msimamo huu ni kwamba Richmond Development Company inataka ilipwe malipo ya awali jumla ya Dola za Kimarekani milioni 15 kabla ya uthibitisho wa kuwepo hati za kusafirishia mitambo.

Majadiliano kuhusu mapendekezo haya yalifanyika tarehe 7 Julai 2006 kwa kuwashirikisha Wajumbe kutoka TANESCO, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania kulingana na masharti ya Kifungu 4.5(c) cha Mkataba. Kumbukumbu zinaonyesha kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali hakuhudhuria kikao hiki, wala mwakilishi wake.

Katika kikao hiki mapendekezo yaliyotolewa na Richmond Development Company LLC yalijadiliwa na kubadilishwa na kuwa asilimia 30 ya kiwango cha mapato ya miaka miwili ya Mkataba kwa wastani wa Dola za Kimarekani (US $30,000,000) milioni thelathini zilipwe kwa Richmond Development Company LLC kwa awamu na masharti yafuatayo:-

(i) Asilimia 12 ya thamani ya Mkataba italipwa kama malipo ya awali *(Advance Payment)* baada ya kuwasilishwa hati ya madai *(Invoice)* na hati ya Uthibitisho wa Udhamini wa Benki *(Bank Guarantee)* kwa TANESCO.

(ii) Asilimia 10 italipwa baada ya kuwasilishwa hati za kusafirisha mitambo kwa mpangilio wa awamu.

(iii) Asilimia 8 italipwa mara baada ya uzinduzi wa mitambo.

(iv) Ilikubalika pia kwamba ifunguliwe akaunti maalum itakayotengwa kuwezesha kupokea, kutunza na kulipa fedha kwa ajili ya malipo yote yanayohitajika *(Escrow)*.

Kikao hiki ambacho kiliongozwa na TANESCO kiliweza kuibana Richmond Development Company LLC isichukue fedha *(advance payment)* kabla ya uthibitisho wa kusafirisha mitambo kama ilivyo katika Mkataba. Jambo hili limethibitika wakati wa ziara ya Wajumbe wa Kamati Teule Houston, Texas ambapo mmiliki wa Richmond Development Company LLC Bwana Mohammed Gire alieleza kuwa hakupata malipo ya awali kwa wakati, tofauti na alivyoomba katika mapendekezo yake ya awali.

Katika kufanikisha malipo yote chini ya vifungu (i – iv) hapo juu, ilikubalika kuwa TANESCO itafungua Barua ya Dhamana ya Benki kwa ajili ya Richmond Development Company LLC kupitia benki ambayo Richmond Development Company LLC itachagua.

TANESCO iliiarifu Richmond Development Company LLC juu ya mapendekezo ya marekebisho hayo ya Barua ya Dhamana ya Benki na kuifahamisha pia Wizara ya Nishati na Madini.

4.2.2 Mapendekezo ya Richmond Development Company LLC kutaka masharti mengine mapya ya Barua ya Dhamana ya Benki (Awamu ya Pili).

Baada ya makubaliano ya marekebisho ya Barua ya Dhamana ya Benki, Richmond Development Company LLC ilirejea tarehe 10 Julai 2006 na kutoa mapendekezo mengine ya kutaka kubadilisha tena masharti ya Barua ya Dhamana ya Benki.

Mapendekezo yaliyowasilishwa katika awamu hii ya pili ni pamoja na:-

(i) Asilimia 17.5 ya jumla ya thamani ya Mkataba ilipwe kama malipo ya awali, na

(ii) Asilimia 17.5 ya thamani ya Mkataba ilipwe baada ya kupakiwa kwa mitambo.

Kimsingi TANESCO hawakuafiki mapendekezo hayo na sababu za msingi kwa TANESCO kutoafiki mapendekezo hayo ni pamoja na:

(i) Wasiwasi juu ya uwezo wa kifedha wa Richmond Development Company LLC, na

(ii) Kuweka kinga kwa kutoruhusu malipo ya awali kabla ya kupata uhakika wa usafirishaji wa mitambo.

Baada ya TANESCO na Richmond Development Company LLC kutofikia muafaka juu ya mapendekezo haya mapya, ndipo tarehe 27 Julai, 2007 Wizara ya Nishati na Madini ilipoingilia kati na kuitisha kikao kujadili maendeleo ya ufunguaji wa Barua ya Dhamana ya Benki ya Richmond Development Company LLC. Kikao hiki kilisimamiwa na Waziri wa Nishati na Madini wa wakati huo (Mhe. Dr. Ibrahim Msabaha, MB) akiwa Mwenyekiti, na kilihusisha Wajumbe kutoka Wizara ya Fedha, TANESCO, Benki Kuu ya Tanzania, Mwakilishi kutoka CTI na Richmond Development Company LLC. Kama ilivyokuwa kwa kikao cha tarehe 7 Julai, 2006 na hapa pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali hakuhudhuria, wala mwakilishi wake.

Kikao hiki kilitengua maamuzi ya kikao cha tarehe 7 Julai na kuafiki kuwa masharti ya Barua ya Dhamana ya Benki yarekebishwe na kuwa kama ilivyopendekezwa na Richmond Development Company LLC, yaani:-

(i) Asilimia 17.5 ya jumla ya thamani ya Mkataba ilipwe baada ya Benki ya Mteja (Richmond Development Company LLC) kupokea hati za usafirishaji wa mitambo *(shipping documents)*, hati ya bima, Orodha ya vifungashio *(packing list)*, hati za uasili wa bidhaa *(Certificate of origin),* hati za upangaji wa mizigo *(packing lists)*, pamoja na hati ya madai (*Invoice)* kwa mtambo wa MW 22.

(ii) Asilimia 17.5 ya jumla ya thamani ya Mkataba ilipwe baada ya TANESCO kutoa hati ya uthibitisho ya mitambo kuwasili eneo la kazi (Ubungo, Dar-es-Salaam).

Tofauti kati ya mapendekezo haya na yale yaliyowasilishwa na Richmond Development Company LLC ni lile la malipo kufanyika baada ya angalau kusafirishwa mtambo mmoja.

Masuala mengine yaliyokubaliwa katika kikao hiki cha tarehe 27 Julai ni kwamba:

(i) Mitambo inaweza kusafirishwa kwa awamu mbili ili mradi mtambo wa kwanza uwe na uwezo wa kuzalisha si chini ya MW 22 na inayofuata ikamilishe kiasi kinachobaki kutimiza jumla ya MW 105.6.

(ii) Malipo ya awali yatafidiwa kutoka katika madai ya *capacity charges* kwa viwango vilivyo sawa kwa miezi 24 kuanzia tarehe ya kuzinduliwa kwa mitambo *(Commercial Operating Date)* ambayo ni 2 Februari, 2006.

(iii) Barua ya Dhamana ya Benki ifunguliwe kupitia Citibank (Tanzania) na itolewe kwa uhai wa miezi minne.

(iv) Akaunti ya *Escrow* ifunguliwe yenye thamani ya kuwezesha kulipia gharama za mitambo (contract price) kwa miezi minne.

Baada ya makubaliano haya TANESCO ilianza kuandaa mchakato wa kufungua Barua ya Dhamana ya Benki.

4.2 Mchakato wa Kufungua Barua ya Dhamana ya Benki

TANESCO huendesha biashara yake kwa kutumia Benki za hapa nchini zikiwemo CRDB na Citibank. Benki hizi kiutendaji zinapaswa kuwa na mahusiano ya kiutendaji na Benki nyingine za Kimataifa nje ya nchi *(Correspondent Bank),* ili pale inapohitajika kumlipa mteja aliyeko nje ya nchi basi Barua ya Dhamana ya Benki ifunguliwe kwa ajili hiyo.

Ili kufungua Barua ya Dhamana ya Benki kwa ajili ya Richmond Development Company LLC kulingana na masharti ya Mkataba, tarehe 23 Agosti, 2006 TANESCO iliiomba Benki ya Citibank (Tanzania) kufungua Barua ya Dhamana ya Benki kwa ajili ya Richmond Development Company LLC yenye thamani ya Dola za Kimarekani 30,696,598.00 kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa[46].

Barua ya Dhamana ya Benki iliyowasilishwa Citibank (Tanzania) ilikuwa na masharti mahsusi yafuatayo:

[46] Barua ya Dhamana ya Benki iliyopelekwa Citibank (Tanzania)

SENDER:	CRDB Bank LTD Dar-es-Salaam
RECEIVER:	CITIBANK N.A NEW YORK NY US
LETTER OF CREDIT NO.	NR CRDB 061LC 092
DATE OF ISSUE:	06 07 25 – (25 July, 2006)
DATE AND PLACE OF EXPIRY:	06 11 23 – (23 Novemba, 2006)(TEXAS)
APPLICANT:	TANESCO
BENEFICIARY:	Richmond Development Company LLC 5825 Schumacher HOUSTON TEXAS
LETTER OF CREDIT:	USD 30,696,598.00
GOODS:	TM 2500 22 MV Gas Turbine (moja)
MASHARTI:	Thamani ya Barua ya Dhamana ya Benki ni sawa na asilimia 35 ya jumla ya thamani ya Mkataba.
MUDA WA KUWASILISHWA HATI:	Hati za usafirishaji **z**iwasilishwe ndani ya siku 21 baada ya mitambo kupakiwa mradi siku hizo ziwe ndani ya uhai wa Barua ya Dhamana ya Benki.

Pamoja na maombi haya TANESCO iliambatanisha hati ya madai Namba 100 ya tarehe 2 Agosti 2006 ya thamani ya Dola za Marekani 30,696,598.00 iliyowasilishwa na Richmond Development Company LLC.

Tarehe 23 Agosti 2006, Citibank (Tanzania) iliwajulisha TANESCO kwamba hawangeweza kufungua Barua ya Dhamana ya Benki kwa ajili ya Richmond Development Company LLC, kutokana na kile walichoeleza kuwa ni kutopata muda wa kutosha kuchunguza kwa kina uwezo wa mteja anayehusishwa na dhamana ya malipo hayo *(due diligence)*.[47]

Baada ya kukataliwa na Citibank, TANESCO waliiomba Benki ya CRDB kufungua Barua ya Dhamana ya Benki hiyo kwa masharti sawa na yale yaliyopelekwa Citibank (Tanzania).[48]

Tarehe 25 Agosti, 2006 kwa kuzingatia uharaka wa mahitaji ya umeme wa dharura nchini, Benki ya CRDB ilifanya mawasiliano kufungua Barua ya Dhamana ya Benki kupitia Benki ya Citibank (New York). Lakini tarehe 2 Septemba 2006, Citibank (New York) iliifahamisha Benki ya CRDB kuwa wao pia wasingeweza kushiriki katika kufungua Barua ya Dhamana ya Benki kwa Richmond Development Company LLC kutokana na mahitaji ya lazima ya

[47] Barua kutoka CITIBANK (T) LTD kutoweza kufungua Barua ya Dhamana ya Benki kwa Richmond Development Company LLC ya tarehe 23/8/2006
[48] Barua ya tarehe 23/8/2006 kutoka TANESCO kwenda CRDB Bank Limited

kuzingatiwa chini ya Kifungu Namba 7 cha Kanuni za UCP 500. Kifungu hicho ndicho kilichowafanya Citibank (Tanzania) kukataa kufungua Barua kama hiyo.

Kitendo cha kukataliwa kufunguliwa kwa Barua ya Dhamana ya Benki na Citibank (Tanzania) katika awamu ya kwanza na Benki ya Citibank (New York) katika awamu ya pili ni dalili zinazoleta hofu juu ya mahusiano kati ya Benki hiyo na Richmond Development Company LLC, iwapo kweli alikuwa mteja wao.

Tarehe hiyo hiyo, 2 Septemba 2006, kwa kuzingatia tena umuhimu na uharaka wa utekelezaji wa mradi wa umeme wa dharua, Benki ya CRDB ilifungua upya Barua ya Dhamana ya Benki kwa Richmond Development Company LLC kupitia Benki nyingine ya nje iitwayo HSBC Bank kwa masharti yale yale ambayo CRDB ilipokea kutoka TANESCO.

Katika kutimiza masharti ya Barua ya Dhamana ya Benki, Benki ya HSBC ilipaswa kukubali kuidhamini Barua ya Dhamana ya Benki, hivyo tarehe 2 Septemba 2006 Benki ya HSBC baada ya kuwasiliana na Richmond Development Company LLC ambayo iliomba ilipwe kama RDEVCO, HSBC ilifungua Barua ya Dhamana ya Benki ambayo ilithibitishwa (confirmed) tarehe 11 Septemba, 2006, na Richmond Development Company LLC ikafahamishwa.

4.3 Maombi ya Richmond Development Company LLC kubadilisha tena Masharti ya Barua ya Dhamana ya Benki (Awamu ya Tatu)

Baada ya Barua ya Dhamana ya Benki kufunguliwa na kuthibitishwa uwajibikaji kwa utekelezaji wa masharti ya Mkataba ulianza rasmi. Hata hivyo, tarehe 4 Oktoba 2006, Richmond Development Company LLC kwa mara nyingine tena iliipelekea TANESCO maombi ya kutaka kuifanyia marekebisho ya Barua ya Dhamana ya Benki[49], kwamba:-

(i) Barua ya Dhamana ya Benki iruhusu malipo ya awali *(Upfront Payment)* ya Dola za Kimarekani milioni 10.

(ii) Richmond Development Company LLC iruhusiwe kusafirisha mtambo wa kwanza kwa njia ya ndege kwa gharama ya Dola za Kimarekani 5,696,568.00.

(iii) Asilimia 50 ya Barua ya Dhamana ya Benki ilipwe baada ya uthibitisho kutoka TANESCO juu ya kupokelewa kwa mitambo nchini.

Tarehe hiyo hiyo, 4 Oktoba, 2006 Wizara ya Nishati na Madini iliitisha kikao kujadili maombi hayo. Kikao hiki kilihudhuriwa na wawakilishi kutoka Wizara ya Nishati na Madini, TANESCO, Benki ya CRDB na Richmond Development Company LLC. Aidha, kwa kuwa mwakilishi wa Richmond Development Company LLC hapa Tanzania

[49] Maombi ya marekebisho ya Barua ya Dhamana ya Benki toka Richmond Development Company LLC (Awamu ya Tatu).

alitaka ufafanuzi zaidi kutoka kwa mwanahisa mkuu aliyekuwepo, Texas, Marekani, hivyo mkutano kwa njia ya simu *(Teleconference)* ukafanyika kupata ushauri wa mwisho. Kikao hiki kilikubali maombi yote ya Richmond Development Company LLC, na kwamba hatua za utekelezaji zifuate mara moja.[50]

Pamoja na ukweli kwamba mchakato mzima ulitawaliwa na udharura, Kamati Teule haielewi ni vipi Wizara ya Nishati na Madini ilikuwa ikitekeleza kila pendekezo jipya linalotolewa na Richmond Development Company LLC, hata yale ambayo ni wazi yako kinyume na Mkataba.

Tarehe 6 Oktoba, 2006, TANESCO iliomba kibali rasmi kutoka Wizara ya Nishati na Madini ili kufanya marekebisho yaliyopitishwa na kikao cha tarehe 4 Oktoba, 2006. Hii ilikuwa baada ya kubaini kwamba mapendekezo hayo yako nje ya masharti ya Barua ya Dhamana ya Benki, yaliyoainishwa katika Mkataba wa malipo kati ya TANESCO, Benki Kuu ya Tanzania, Wizara ya Fedha na CRDB Bank, Mkataba ambao unaelekeza masharti ya fungu maalum la *Multilateral Debt Relief Initiative.*[51]

Wizara ya Nishati na Madini iliijulisha Wizara ya Fedha kuhusu maombi haya mapya kutoka Richmond Development Company LLC.[52] Katika barua hiyo, Wizara ya Nishati na Madini ilieleza kwamba

[50] Kumbukumbu za kikao cha marekebisho ya Barua ya Dhamana ya Benki tarehe 4 Oktoba 2006.
[51] Barua Kumb. Na. DF/C/O/28 ya tarehe 6/10/2006
[52] Barua Kumb. Na. CBD. 214/324/01 ya Tarehe 6/10/2006

katika Mkataba kati ya TANESCO na Richmond Development Company LLC, kipo Kifungu kinachoruhusu usafirishaji wa mitambo kwa njia ya ndege hivyo ombi la Richmond Development Company LLC la kuomba marekebisho katika Barua ya Dhamana ya Benki kuruhusu kulipwa kwa Dola za Marekani 5,696,568.00, halina madhara katika Mkataba uliopo.

Wizara ya Fedha haikuridhishwa na mapendekezo yaliyotolewa kwani malipo yoyote ya awali kutoka fungu maalum la *Multilateral Debt Relief Initiative* ni lazima yafanyike kwa uthibitisho wa kuridhisha. Sehemu ya barua hiyo inasomeka kama ifuatavyo:-

> *" . . . We note that, contrary to the information provided during Contract negotiation that the selected lease contractor (RDC) had the necessary equipment ready for delivery, it is now apparent that, this was not the case.*
>
> *As you know, payment in respect of the rental or procured power plants under the Emergency Power Project funded through the IMF MDRI Account are based on the negotiated and signed contract.*
>
> *I, therefore, wish to advise that any advance payment from the MDRI Account must be against satisfactory*

security from the lessor. This requirement seems not to be met under your proposed arrangement."[53]

Pamoja na maelekezo na ushauri huu wa Wizara ya Fedha, siku hiyo hiyo Wizara ya Nishati na Madini iliwaandikia barua TANESCO kuitaka itekeleze maombi ya Richmond Development Company LLC kubadilisha masharti ya malipo, kwamba:-

" . . . I wish to inform you that the proposed amendments to the existing Letter of Credit are acceptable and you are advised to liaise with CRDB Bank to effect the changes as soon as is practical. . . ."[54]

Kamati Teule imejiuliza bila kupata majibu: Ni nini kilifanyika hadi Wizara ya Nishati na Madini ikatoa kauli hii ambayo ni tofauti kabisa na ushauri walioupata kutoka Wizara ya Fedha?

Katika kutekeleza maagizo ya Wizara, tarehe 6 Oktoba, TANESCO iliiandikia barua Benki ya CRDB kuitaka kufanya mabadiliko yafuatayo:-[55]

(i) Barua ya Dhamana ya Benki iruhusu malipo ya awali ya malipo ya Dola za Kimarekani milioni 10 ili kuiwezesha Richmond

[53] Barua Kumb. TYC/E/60/1 ya tarehe 6/10/2006
[54] Barua Kumb Na. CBD.214/324/01 ya tarehe 6/10/2006
[55] Barua Kumb Na. DF/MF/BANK ya tarehe 6/10/2006.

Development Company LLC kumlipa mmiliki wa mtambo mmoja kabla ya kuusafirisha kwa ndege kuja nchini.

(ii) Salio la Dola za Kimarekani 5,696,598.00 kati ya asilimia 50 ya kwanza ya thamani ya Barua ya Dhamana ya Benki ilipwe wakati wa kuwasilishwa hati za kusafirishia mitambo.

(iii) Asilimia 50 iliyobaki ilipwe wakati wa kuwasilisha hati za uthibitisho wa kuwasili kwa mitambo katika eneo la kazi la TANESCO.

Tarehe 9 Oktoba, 2006 Benki ya CRDB iliijibu TANESCO na kuikumbusha kwamba Barua ya Dhamana ya Benki inasimamiwa na makubaliano ya pamoja chini ya uangalizi wa Benki Kuu ya Tanzania. Kwa msingi huo TANESCO ililazimika kuiomba Benki Kuu ya Tanzania kibali cha kufanya marekebisho katika Kifungu 1(a) cha Mkataba wa makubaliano ya taratibu za malipo ili kuwezesha maombi yaliyopendekezwa kufanyiwa kazi. Kwa msingi huo, Benki ya CRDB haikutekeleza ombi la TANESCO la kuifanyia marekebisho *Barua ya Dhamana ya Benki*.[56] Hii ikailazimu TANESCO kufuta maombi yake ya kutaka mabadiliko yafanywe katika Barua ya Dhamana ya Benki kama ilivyokuwa imeombwa katika barua ya tarehe 6 Oktoba, 2006.[57] Hivyo TANESCO ikawa imefunga mjadala wa maombi ya Richmond Development Company LLC kutaka mabadiliko ya ziada katika Barua ya Dhamana ya Benki.

[56] Barua Kumb. Na. CRDB06ILC092 ya tarehe 9/10/2006.
[57] Barua Kumb. Na. DF/MF/BANK ya tarehe 9/10/2006

Hadi Barua ya Dhamana ya Benki inakwisha muda wake (tarehe 30 Novemba, 2006) Richmond Development Company LLC haikuwa imetekeleza sharti hata moja na hivyo kushindwa kuchukua fedha kama ilivyokuwa imepangwa. Swali linalojitokeza ni, iwapo Benki ya CRDB ingekubali kubadilisha masharti ya Barua ya Dhamana ya Benki na kuipa Richmond Development Company LLC fedha ilizoomba bila kibali cha Benki Kuu ya Tanzania, na bila Mkataba kuruhusu, Je, Richmond Development Company LLC ingeleta nchini mitambo kama ilivyokusudiwa au ingekuwa ni hasara kwa Taifa?

Kwa upande mwingine, mchakato mzima wa Richmond Development Company LLC wa kutaka kufanya mabadiliko katika Barua ya Dhamana ya Benki mara kwa mara unadhihirisha nia yao ya kutaka kupata mtaji. Pia inadhihirisha kwamba Richmond Development Company LLC haikuwa na uwezo wa kifedha wa kutekeleza Mkataba huu kama ilivyoelezwa katika Sehemu "B" ya utambulisho wa pande zilizoingia Mkataba huu *(parties to the contract)*. Sehemu hii inasomeka kama ifuatavyo:-

> *"The Supplier has the equipment and the financial and technical capability to construct, install, commission, operate and maintain such a plant as required by TANESCO".*
> (Msambazaji *(supplier)* ana vifaa na uwezo wa kifedha na wa kitaalam kujenga, kusimika, kuiwasha, kuendesha na kuendeleza mtambo kama TANESCO inavyohitaji.)

Kwa msingi huo Kamati Teule ilijiuliza maswali yafuatayo:-

(i) Je, utafiti ulifanywa kufahamu gharama halisi za mitambo mipya kutoka kwa watengenezaji wenyewe bila ya kupitia kwa mawakala? Kamati Teule ilibaini kuwa zoezi hilo liliwahi kufanyika mwaka 1998 tu ambapo Wizara ya Nishati na Madini ilitoa kazi hiyo kwa wataalam wa sekta *(consultants)* na kufanikisha kugundua kuwa bei ya mitambo ya umeme ya IPTL (400 MW) ambayo ilitakiwa kuuzwa kwa Dola za Kimarekani milioni 150 (Tsh. 187.5 bilioni) wakati bei yake halisi ilikuwa ni Dola za Kimarekani milioni 85 (Tsh.106.2 bilioni) tu na hivyo kupata kigezo cha kukataa bei yao[58]. Hali kadhalika kutokana na uzoefu wa Wizara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na TANESCO walitakiwa kufuatilia bei hizo za mitambo na pia makadirio ya kazi za ujenzi ili kupata picha ya gharama halisi ya mradi jambo, ambalo halikufanyika.

Kitendo cha viongozi wa Wizara na TANESCO kushindwa kujua bei halisi ya mitambo kutoka kwa watengenezaji wenyewe kwa takribani miaka 10 huku wakisafiri kwenda nje ya nchi kila kukicha kwa mikutano, warsha, makongamano, n.k, na kwa Wizara kung'ang'ania kutumia mawakala badala ya watengenezaji wa mitambo, nchi yetu imegeuzwa gulio la wajanja kuikamua na

[58] Taarifa rasmi za Bunge HANSARD ya tarehe 19/12/2007 Mahojiano na Ndugu P.Rutabanzibwa

kuwabebesha wananchi mzigo wa kodi. Wakati ikiwa Marekani, Kamati Teule iliamua kufanya utafiti huo ili kuona kama Taifa lingenufaika iwapo maamuzi ya busara zaidi yangefanyika. Kamati Teule iliwatembelea baadhi ya watengenezaji wa mitambo ya uzalishaji wa umeme huko huko Houston Marekani kujua bei za mitambo yao. Mmoja wao, *Kawasaki Gas Turbines – Americas* anatengeneza na kuuza mtambo mpya aina ya GPB180 wenye uwezo wa kuzalisha MW 17.5 kwa Dola za Kimarekani 7.5 milioni (Tsh. 9.4 bilioni). Mawakala huwa wanatuletea mitambo ya aina hiyo hiyo kwa bei mara mbili ya bei halisi.

(ii) Iwapo TANESCO au Serikali iliweza kufungua Barua ya Dhamana ya Benki ya thamani ya Dola za Kimarekani 30,696,598, je, fedha hizo zisingeweza kutosheleza kununua mitambo mipya ya uzalishaji umeme, na mitambo hiyo kubakia mali ya TANESCO, badala ya kuingia katika Mikataba ya ghali ya kukodisha mitambo?

Aidha, taarifa za watendaji wa Wizara ya Nishati na Madini kwamba wakati wa kipindi cha mchakato wa zabuni ya umeme wa dharura kulikuwa na ugumu wa kupatikana mitambo ya umeme wa dharura zimethibitishwa na Kamati Teule kuwa sio za kweli.

Ni ukweli kwamba kulikuwa na ukame, lakini ukame huo haukuwa wa mitambo ya kuzalisha umeme kwani mitambo hiyo hutengenezwa muda wote na sio kwa kutegemea mvua. Aidha, utafiti wetu umebaini kuwa katika kipindi hicho cha matatizo ya umeme nchini, kampuni moja tu ya *Kawasaki* ilikuwa na mitambo 8 ya kisasa tena ile yenye kutumia gesi na dizeli (***dual fuel plant***). Mitambo hii ina uwezo wa kusukuma maji na kuzalisha umeme kwa wakati mmoja. Na hii bei ya Dola za Kimarekani milioni 7.5 kwa mtambo mmoja ni bei ya kuanzia tu kwani mteja anaweza kupunguziwa. Ushahidi wa hili ni kwamba Serikali ya Nigeria mwaka huo wa 2006 iliuziwa mitambo hiyo na Kampuni ya Kawasaki kwa Dola za Kimarekani 6.7 milioni au Tsh.8.4 bilioni kwa mtambo mmoja.[59]

Kwa thamani ya Barua ya Dhamana ya Benki iliyofunguliwa kwa Richmond Development Company LLC ya Dola za Kimarekani milioni 30.7 au Tsh 38.4 bilioni ingeweza kununuliwa mitambo mipya yote minne pamoja na kumudu kulipia gharama za kusafirisha kwa meli hadi Dar-es-Salaam. Hivyo ili zipatikane MW 105.6 zilizohitajiwa na TANESCO ingehitajika mitambo sita (6) ambayo ni sawa sawa Dola za Kimarekani milioni 45 au Tsh. 56.25 bilioni badala ya Dola za Kimarekani milioni 87 au Tsh. 108.7 bilioni tulizobebeshwa na Richmond Development Company LLC.

[59] Kabrasha *(brochure)* la Kawasaki Gas Turbines – Americas na picha za Karakana yao.

Je, si dhahiri kuwa hii ndio ilikuwa nia ya Richmond Development Company LLC, yaani kupata fedha za malipo ya awali *(advance payment)* ili ikanunulie mtambo mmoja na kuja kuukodisha kwa TANESCO hivyo kufaidika na *capacity charge* ya kila mwezi kwa Mkataba wa miaka miwili? Kwa mtambo mmoja wa MW 22 *capacity charge* ni Dola za Kimarekani takriban 730,871 au Tsh. Milioni 913.6 kwa mwezi, hivyo kwa miezi 24 ni wastani wa Dola za Kimarekani 17,540,912 au Tsh. Bilioni 21.9.

(iii) Kwa kuwa thamani ya Barua ya Dhamana ya Benki inalipwa kama malipo ya awali *(advance payment),* Je, hii si sawa na kutoa mkopo kwa Richmond Development Company LLC? Kwa nini tunatoa mkopo na kukubali mkopo huo urejeshwe kwa awamu sawa kwa miaka miwili bila riba? Kamati Teule inaona kwamba hiyo ni sawa na kutoa mkopo wa masharti nafuu kwa mfanyabiashara wa nje ili awe mwekezaji.

(iv) Kwa nini katika Mkataba wa Richmond Development Company LLC kifungu cha kufidia malipo ya awali *(advance payment)* ya Barua ya Dhamana ya Benki hakikuwekwa bayana ndani ya Mkataba tofauti na Mikataba mingine? Kamati Teule haioni sababu yeyote ya msingi mbali na wahusika kujiwekea fursa ya kukidhi maslahi yao binafsi.

(v) Serikali haioni kuwa utaratibu wa aina hii unaoelezwa katika swali namba (iv) inaweza kuwa kichocheo cha vitendo vya ufisadi?

4.4 Kushindwa kwa Richmond Development Company LLC kutimiza masharti ya Mkataba

Kabla ya Barua ya Dhamana ya Benki ya Richmond Development Company LLC kufikia ukomo wa kutumika (tarehe 30 Novemba, 2007) TANESCO ilichukua hatua kadhaa kuonyesha wasiwasi wake juu ya uwezo wa Richmond Development Company LLC katika kutelekeza Mkataba wa uzalishaji wa umeme wa dharura wa MW105.6 kwa mpango wa kukodisha.

Baadhi ya hatua zilizochukuliwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Tarehe 7 Oktoba 2006, TANESCO iliwaandikia barua Richmond Development Company LLC kuhusu wajibu na majukumu muhimu ndani ya Mkataba na viwango vya mitambo vinavyohitajiji kuzingatiwa. TANESCO pia ilisisitiza kwamba wakati wa majadiliano ya Mkataba katika Kamati ya Majadiliano ya Serikali, (GNT) Richmond Development Company LLC ilisema kwamba itatekeleza mradi wa uwekezaji wa mitambo ya umeme wa dharura pamoja na kampuni kubwa ya kimataifa ya Pratt & Whitney, na kwamba Mkataba wa makubaliano kati ya Richmond Development Company LLC na Pratt & Whitney

ungeambatanishwa kama sehemu ya Mkataba kati ya TANESCO na Richmond Development Company LLC. Nakala ya barua hiyo ilipelekwa Wizara ya Nishati na Madini.[60]

(ii) Aidha, Tarehe 27 Oktoba, 2006 TANESCO ilitoa tena taarifa ya tahadhari *(Default Notice)* kwa Richmond Development Company LLC kuwa wanakiuka masharti ya Mkataba chini ya Kifungu 12.3(a). Katika barua hiyo TANESCO iliorodhesha mapungufu makuu yafuatayo:-

(a) Hata baada ya Barua ya Dhamana ya Benki kufunguliwa tarehe 2 Septemba, 2006 hadi kufikia 27 Oktoba 2006, mtambo wa kwanza wa wastani wa unit 22 kW ulikuwa bado haujasafirishwa.

(b) Kuchelewa kuwasili kwa mtambo huo wa kwanza kunaashiria kushindwa kufika kwa wakati tarehe ya uzinduzi wa mitambo *(Commercial Operation Date)*. Mtambo wa kwanza ungepaswa kuwa tayari tarehe 25 Oktoba, 2006 iwapo ungesafirishwa kwa ndege au tarehe 25 Novemba, 2006 iwapo ungesafirishwa kwa meli.

(c) Mwakilishi wa Richmond Development Company LLC aliyepo Dar-es-Salaam amekuwa akishindwa kutoa taarifa za maendeleo ya utekelezaji mradi katika vikao

[60] Barua Kumb. Na. DP/EPP 100 MW Rentals Plant 7/10/ 2006

mbali mbali vya Wizara ya Nishati na Madini na TANESCO.

(d) Kumekuwa na shaka ya uwepo kihalali wa kampuni yenye jina la Richmond Development Company LLC huko Texas, Marekani, na kwamba hatua ndiyo zilikuwa zinaanza hapa Tanzania kuandikisha kampuni mpya inayoitwa Richmond Development Company (Tanzania) Ltd kupitia Msajili wa Makampuni pamoja na kupata *Certificate of Incentive* kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

(e) TANESCO imepata wasiwasi kama Richmond Development Company LLC ni kampuni yenye uwezo wa kitaalamu na kifedha kuweza kutekeleza Mkataba uliopo.

Hivyo, kwa kuwa Kifungu 12.3(a) cha Mkataba kinatoa nafasi ya kutoa taarifa ya tahadhari ya kukiukwa kwa masharti ya Mkataba, TANESCO iliwataka Richmond Development Company LLC kuanza majadiliano ya utetezi wao ndani ya siku 30. Wizara ya Nishati na Madini na Mwanasheria Mkuu wa Serikali walipewa nakala ya barua hiyo.[61]

(iii) Tarehe 17 Novemba, 2006 TANESCO iliwaandikia tena Richmond Development Company LLC, kuwakumbusha juu ya madokezo

[61] Barua Kumb. Na. MD/033 ya tarehe 27/10/2006.

yaliyotangulia katika barua za tarehe 7 Oktoba, 2006, 27 Oktoba, 2006 na majadiliano katika ngazi mbali mbali ikiwemo mkutano wa pamoja uliofanyika kwa Katibu Mkuu Kiongozi, Ikulu, tarehe 13 Oktoba, 2006 ambapo Mwakilishi wa Richmond Development Company LLC Bwana Naeem Gire alihudhuria.

Katika barua hiyo TANESCO iliwaarifu Richmond Development Company LLC kwamba imepata habari za kuaminika kwamba kwa muda mrefu kumekuwa hakuna mawasiliano kati ya Pratt & Whitney na Richmond Development Company LLC, na upo wasiwasi iwapo majukumu ya Pratt & Whitney yatatekelezwa! TANESCO ilisisitiza madai yao ya awali ya kupata nakala ya Mkataba wa makubalino kati ya Richmond Development Company LLC na Pratt & Whitney kama ilivyoainishwa katika majadiliano ya Mkataba.[62]

(iv) Tarehe 23 Novemba 2006 TANESCO waliwakumbusha Richmond Development Company LLC kuhusu taarifa ya tahadhari juu ya kukiukwa kwa Mkataba chini ya Kifungu 12.3(a) cha Mkataba ambayo TANESCO ilianza kutekeleza kwa barua iliyoandikwa kwao tarehe 27 Oktoba, 2006; kwamba siku 30 kwa ajili ya majadiliano ya pande mbili za Mkataba zinafikia ukomo tarehe 26 Novemba 2006. Hivyo TANESCO ilipendekeza Mkutano wa pande mbili za Mkataba ufanyike tarehe 30 Novemba, 2006 ili hoja zote

[62] Barua Kumb. Na.MD/033 ya tarehe 17/11/2006.

zilizoainishwa na ambazo hadi tarehe hiyo Richmond Development Company LLC haikuweza kuzitekeleza zijibiwe.[63]

Kamati Teule imeshangazwa kuona kwamba badala ya kuiunga mkono TANESCO katika jitihada zake za kuisisitizia Richmond Development Company LLC itekeleze wajibu wake kulingana na Mkataba, Wizara ya Nishati na Madini haikufurahishwa na taarifa hizi za tahadhari zilizokuwa zikitolewa na TANESCO kwenda kwa Richmond Development Company LLC.

Mshangao huu unatokana na mawasiliano kutoka Wizara ya Nishati na Madini yakimweleza Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO kwamba Waziri wa Nishati na Madini (sasa akiwa ni Mhe. Nazir Karamagi, Mb.) anataka maelezo kuhusiana na taarifa ya tahadhari iliyotumwa kwa Richmond Development Company LLC. Sehemu ya barua ya majibu ya Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO kwenda kwa Waziri wa Nishati na Madini inasomeka kama ifuatavyo:-

> *". . . As part of the contract administration it is considered prudent to maintain formal communication on all matters pertaining to the contract between TANESCO and RDC. As you may be aware, TANESCO has failed to obtain responses on matters concerning the*

[63] Barua Kumb. Na DP/100 MW Rentals ya tarehe 23/11/2006.

project which could consider that TANESCO has waived some of its rights under the Contract.

The purpose of the said letter is to facilitate a meeting between TANESCO and RDC in order to clear contractual issues that need to be sorted out in order to expedite the implementation of the project within the stipulated agreements. . . .[64]

Pamoja na jitihada za TANESCO kuiandikia Richmond Development Company LLC, Kampuni hiyo haikujibu wala kutekeleza masharti muhimu ya Mkataba.

4.6 Mwelekeo mpya wa Mkataba wa umeme wa dharura

Tarehe 28 Novemba 2006, Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO, Balozi Fulgence M. Kazaura, alimuandikia barua Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO kwamba, asubuhi ya siku hiyo amepigiwa simu na Waziri wa Nishati na Madini akiwa Jijini Calgary, Canada akimuarifu kwamba Richmond Development Company LLC inakusudia kuhamisha majukumu yao yaliyobaki katika Mkataba wa uletaji na uzalishaji umeme wa dharura kwa kampuni nyingine, na kwamba Mheshimiwa Waziri ameagiza TANESCO ifanye mambo yafuatayo:-

[64] Barua Kumb. Na. MD/003 ya tarehe 23/11/ 2006.

(i) Kutathmini kuona iwapo Mkataba kati ya TANESCO na Richmond Development Company LLC unaruhusu kukabidhi majukumu kwa kampuni nyingine.

(ii) Kuwasiliana na Richmond Development Company LLC kufahamu mitambo inayokusudiwa kuletwa kutoka Afrika Kusini iko sehemu gani.

(iii) TANESCO ipeleke timu ya wataalamu wa mitambo Afrika Kusini katika eneo linalosemekana kwamba mitambo hiyo ipo ili wathibitishe kuwepo kwa mitambo hiyo na uwezo wa mitambo kufuatana na viwango vya Mkataba.[65]

Tarehe hiyo hiyo 28 Novemba 2006 uongozi wa TANESCO ulimshauri Mwenyekiti wa Bodi kama ifuatavyo:-

(i) Mkataba kati ya Richmond Development Company LLC na TANESCO hauruhusu kukabidhi majukumu ya Mkataba kwa Kampuni nyingine isipokuwa kwa maafikiano ya pande mbili za Mkataba (Kifungu 15.12).

(ii) TANESCO ilipata taarifa kwamba mitambo miwili ya Pratt & Whitney aina ya FT4 haitapatikana, na badala yake Richmond Development Company LLC inakusudia kuleta mitambo minne aina ya GE TM 2500 kutoka Afrika Kusini. Hata hivyo, taarifa

[65] Barua Kumb. Na SEC. 216/C/RDC ya tarehe 28/11/2006

hiyo waliyoipata kutoka kwa mwakilishi wa Richmond Development Company LLC nchini haijathibitishwa kwa maandishi.

(iii) Mtambo huo wa GE TM 2500 unaweza kufikia viwango vya ubora uliotajwa katika Mkataba.

(iv) Mitambo ingeweza kufika Dar-es-Salaam tarehe 8 Januari, 2007 na kuanza uzalishaji tarehe 27 Januari 2007.

(v) Pamoja na Wizara ya Nishati na Madini kupendekeza kwamba TANESCO iunde timu ya Wataalam kwenda Afrika Kusini kukagua mitambo kwa kushirikiana na wawakilishi wa Richmond Development Company LLC. TANESCO inakabiliwa na tatizo la mawasiliano kati yake na Richmond Development Company LLC ili kuwezesha ukaguzi huo kufanyika haraka.[66]

Hata hivyo, Kamati Teule imefahamishwa kwamba timu ya wataalam iliteuliwa kwenda Afrika Kusini kufanya ukaguzi na walithibitisha kuwepo kwa mitambo iliyotajwa.[67]

Tarehe 4 Disemba 2006, TANESCO walipokea barua kutoka kwa Richmond Development Company LLC iliyoonyesha kwamba iliandikwa tangu tarehe 9 Novemba, 2006. Katika barua hiyo Richmond Development Company LLC ilieleza kwamba inakusudia

[66] Majibu ya Uongozi wa TANESCO kwa Mwenyekiti wa Bodi.
[67] Barua Kumb. Na CBD.286/397/01 ya tarehe 28/11/2006 na taarifa ya ukaguzi

kutumia haki yake chini ya Kifungu 15.12 cha Mkataba ili kuhamisha majukumu yake yote ndani ya Mkataba huo kwenda kwa DOWANS Holdings, S.A. Aidha, Richmond Development Company LLC ilieleza kwamba tarehe ambayo TANESCO itaridhia mapendekezo hayo iwe ndiyo tarehe rasmi ya kuhamisha mafao na majukumu yote kwa DOWANS Holdings, S.A na kwamba DOWANS Holdings, S.A itawasilisha vielelezo vya utambulisho wake kwa TANESCO.[68]

Siku hiyo hiyo TANESCO iliwajibu Richmond Development Company LLC kwamba kwa wakati huo haiko tayari kuridhia pendekezo hilo kwa sababu kuu tatu:

(i) Kifungu 15.12 cha Mkataba kinataka kuwepo kwa makubaliano ya pamoja ya kimaandishi *(written mutual agreement)* kutoka kwa wahusika wote wa Mkataba *(Parties)* kabla ya kufikiwa uamuzi wa kuhamisha Mkataba.

(ii) Richmond Development Company LLC haijatoa sababu zozote za msingi kwa pendekezo hilo la kuhamisha Mkataba.

(iii) TANESCO haifahamu historia, uzoefu wala uwezo wa kifedha wa hao wanaopendekezwa kuhamishiwa Mkataba.

[68] Barua ya Richmond Development Company LLC 9 Novemba , 2006

(iv) Aidha, TANESCO ilikumbushia barua zake nne ilizoiandikia Richmond Development Company LLC (tarehe 27 Oktoba, 17, 23 na 29 Novemba) kuhusu ukiukwaji wa masharti ya Mkataba unaofanywa na Richmond Development Company LLC pasipo Richmond Development Company LLC kujibu chochote kwa kipindi chote hicho.

Hivyo, TANESCO iliwafahamisha Richmond Development Company LLC kwamba hadi pale yote yaliyoelezwa yatakapotekelezwa haitaridhia pendekezo la kuhamisha Mkataba husika.[69]

Kwa upande mwingine, ili kujiandaa kwa dharura ya kusudio la kuhamisha majukumu ya Mkataba kwa DOWANS Holdings, S.A TANESCO iliiandikia barua Benki ya Citibank (Tanzania) ikiwaelezea pendekezo la Richmond Development Company LLC kuhamisha Mkataba kwa Dowans Holdings, S.A na kuiomba Citibank ifanye uchunguzi *(due diligence)* juu ya Dowans HOLDINGS, S.A kwani japokuwa masharti ya Mkataba yanaruhusu Mkataba kuhamishwa, TANESCO ingependa kufahamu hasa ni nani anayehamishiwa Mkataba huo.[70]

Kamati Teule haikufanikiwa kupata majibu ya Benki ya Citibank (Tanzania) ila ilipata taarifa za ndani ya Wizara na TANESCO kuwa viongozi wa Wizara kama kawaida yao waliishinikiza TANESCO kukubaliana na ombi la Richmond Development Company LLC la

[69] Barua Kumb. Na DP/100MW Rentals ya tarehe 9/12/2006.
[70] Barua Kumb. Na.DP/100 MU Rentals ya tarehe 8/12/2006

kuhamisha Mkataba. Hivyo tarehe 21 Disemba 2006 TANESCO iliiandikia barua Richmond Development Company LLC kukubali pendekezo la kuhamisha majukumu yake kwa Dowans Holdings, S.A[71]. Pamoja na ridhaa hiyo TANESCO ikaweka masharti kwamba ipate hati ya uthibitisho kutoka Dowans Holdings, S.A ya kuridhia uwajibikaji kamilifu katika kutekeleza Mkataba wa tarehe 23 Juni, 2006, kati ya TANESCO na Richmond Development Company LLC.

Tarehe 23 Disemba 2006, TANESCO na Dowans Holdings S.A ya S.L.P. 3614 Sheikh Zayed Road Dubai, United Arab Emirates zilitiliana saini makubaliano ya Dowans Holdings S.A kuridhia Mkataba kati ya TANESCO na Richmond Development Company LLC, na kuahidi kuutekeleza kikamilifu kuwezesha upatikanaji wa MW 105.6 za umeme wa dharura.[72]

Katika utekelezaji huo, Dowans Holdings, S.A ilitakiwa kuingiza nchini mitambo mitatu aina ya TM 2500 PE yenye namba za utambulisho wa watengenezaji 192503, 193539 na 198219, zenye jumla ya uwezo wa kuzalisha MW 64.5.

Tarehe hiyo 23 Disemba 2006, kitendo cha pande zote mbili (TANESCO na Dowans Holdings, S.A) kutia saini kinatoa tafsiri ifuatayo:-

1. Tarehe 23 Disemba 2006 ndiyo siku rasmi ambayo Richmond Development Company LLC imekabidhi rasmi majukumu yake

[71] Barua Kumb. Na. SEC. 388/12/206 ya tarehe 21/12/2006
[72] Mkataba baina ya TANESCO na Richmond Development Company LLC uliosainiwa tarehe 16/3/2006.

ya utekelezaji wa Mkataba kati yake na TANESCO kwa Dowans Holdings S.A

2. Dowans Holdings, S.A itatekeleza majukumu ya Mkataba uliotiwa saini kati ya TANESCO na Richmond Development Company tarehe 23 Juni, 2006 kwa masharti yote kama yalivyo katika Mkataba.

3. Malipo halisi na madeni ndani ya Mkataba kati ya TANESCO na Richmond Development Company LLC, sasa yatakwenda kwa Dowans Holdings, S.A kuanzia tarehe 23 Disemba, 2006.

4.7 Uhaulishaji wa Mkataba kati ya TANESCO, Richmond na Dowans

Tarehe 27 Disemba TANESCO iliingia Mkataba wa pamoja na Benki Kuu ya Tanzania na CRDB Bank Ltd kwa ajili ya kuwezesha Benki Kuu ya Tanzania kulipa Barua ya Dhamana ya Benki Dowans Holdings S.A ili kutekeleza Mradi wa Umeme wa dharura. Mkataba huu uliweka awamu mbili za malipo kama ifuatavyo:-

Awamu ya Kwanza, Dola za Kimarekani milioni 30,696,598.00 (Tsh. 38.4 bilioni) sawa na thamani ya Mkataba kama iliyokuwepo katika Mkataba wa Richmond Develoment Company LLC uliorithiwa na Dowans Holdings S.A.

Awamu ya Pili, Dola za Kimarekani milioni 57,007,967.00 ikiwa ni 65% ya thamani ya Mkataba kwa malipo yanayoendelea katika Mkataba wa Dowans Holdings S.A[73]

Tarehe 28 Disemba TANESCO iliwataka CRDB Bank Ltd kufungua Barua ya Dhamana ya Benki kwa niaba ya Dowans Holdings S.A yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 30,696,598.00 (Tsh. 38.4 bilioni) kwa masharti ya malipo kama ifuatavyo:-

(a) Asilimia 50 ilipwe kama malipo ya awali *(advance payment)* baada ya madai yao kuwasilishwa yakiambatana na ushahidi wa hati ya TANESCO kuthibitisha kwamba mtambo wa MW 22 umepokelewa. Kiasi hiki ni sawa na Dola za Kimarekani milioni 15.3 (Tsh. 19.2 bilioni).

(b) Asilimia 50% iliyobaki ilipwe baada ya mitambo iliyobaki kutimiza MW 105.6 kuthibitishwa kuwa imepokelewa. Hati za madai na hati za uthibitisho wa kupokelewa kwa mitambo ziwasilishwe CRDB Bank Ltd kwa uthibitisho wa watia sahihi wanaotambuliwa na Benki toka TANESCO. Kiasi hiki ni sawa na Dola za Kimarekani milioni 15,348,299.00.

[73] *Letter of Undertaking* kati ya TANESCO, Benki Kuu ya Tanzania na CRDB Bank Ltd za Benki kwa Dowans Holding S.A

Tarehe 28 Disemba, 2006 CRDB Bank Ltd ilifungua Barua ya Dhamana ya Benki yenye Namba CRDB 061L 151 kwa Dowans Holdings, S.A. ya thamani ya Dola za Kimarekani milioni 30,696,598.00 (Tsh. 38.4 bilioni) kwa masharti kama yalivyoelezwa hapo awali. Barua hiyo ya Dhamana ya Benki ilikuwa inaanza kutumika kuanzia tarehe 28 Disemba 2006 na kuishia tarehe 12 Julai, 2007.[74]

4.8 Mchakato wa malipo kwa Dowans Holdings S.A

Tarehe 30 Oktoba, 2006, Mtambo wa MW 22 uliwasili Uwanja wa Ndege Dar-es-Salaam, na viunganishi vyake viliwasili tarehe 14 Novemba 2006. Kwa kuwa Richmond Development Company LLC haikuweza kutimiza masharti ya Barua ya Dhamana iliyofunguliwa hadi muda wake ulipokwisha tarehe 30 Novemba, 2006 mrithi wake, Dowans Holdings S.A alikuwa na haki ya kudai malipo kutokana na Barua ya Dhamana ya Benki iliyofunguliwa kwa niaba ya Richmond Development Company LLC kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa.

Tarehe 28 Disemba 2006 mara baada ya CRDB Bank Ltd kufungua Barua ya Dhamana ya Benki kwa Dowans Holdings S.A, TANESCO ilitoa Barua ya uthibitisho wa kupokelewa kwa mtambo wa MW 22 kwa hati ya ukaguzi ya tarehe 3 Oktoba 2006 na kuruhusu Dowans Holdings S.A kulipwa 50% ya thamani ya Barua ya Dhamana ya Benki

[74] Barua Kumb. Na. DST/MP/P/63/103 ya tarehe 28/12/ 2006.

sawa na Dola za Kimarekani milioni 15,348,299.00.[75] Sehemu hii ya malipo inapaswa kujumuisha gharama za usafirishaji wa mtambo kwa ndege Hati Namba EFD 786675 ya Dola za Kimarekani milioni 4,865,000.00.[76]

Tarehe 4 Januari 2007 Dowans Holdings S.A iliwasilisha TANESCO madai ya usafirishaji wa mtambo mmoja kwa njia ya ndege kwa gharama ya US$ 4,865,000.00. Pamoja na madai hayo Dowans Holdings S.A iliambatanisha Hati ya Ukaguzi na Uthibitisho wa kupokelewa mtambo huo na TANESCO. TANESCO ilipeleka madai hayo Wizara ya Nishati na Madini tarehe 22 Januari, 2007 kwa utekelezaji.

Awamu ya pili ya malipo ya Barua ya Dhamana ya Benki ya Dowans Holdings S.A ilipaswa kulipwa baada ya uthibitisho kutoka TANESCO kwenda CRDB Bank Ltd baada ya mitambo yote kuwasili Dar-es-Salaam kutimiza MW 105.6. Tarehe 10 Machi 2007 Dowans Holdings S.A iliwaarifu TANESCO rasmi kwamba mitambo yote minne iliyobaki ilishawasili na kukaguliwa. Hivyo, tarehe 18 Mei, 2007 TANESCO iliwaarifu CRDB Bank Ltd kwamba mitambo mingine mitatu ilikwisha kupokelewa Dar es Salaam na kufanyiwa ukaguzi. Kwa uthibitisho huo TANESCO ilitoa idhini kwa CRDB Bank Ltd kuwalipa Dowans Holdings S.A US$ 13,813,469 ili kuhitimisha malipo ya asilimia 90 ya thamani ya Barua ya Dhamana ya Benki. Kiwango kilichobaki

[75] Barua Kumb. Na. DST/MP/PSO/P/63/102 ya tarehe 28/12/2006
[76] Barua Kumb. Na. DF/MF/PAMP/GAS ya tarehe 22/01/2007

US$1,534,850 kitalipwa baada ya uthibitisho wa kuwasili nchini kwa mtambo uliobakia.[77]

Tarehe 20 Juni, 2007 TANESCO ilitoa hati ya mwisho ya uthibitisho wa kuwasili kwa mtambo uliobaki na kuitaka CRDB Bank Ltd kuwalipa Dowans Holdings S.A salio la US $1,534,830.00 kutoka katika Barua ya Dhamana ya Benki.[78]

Jumla ya malipo yaliyothibitishwa na Benki Kuu ya Tanzania[79] kuwa yamelipwa kwa Dowans Holdings S.A ni kama ifuatavyo:-

Tarehe 2 Januari, 2007	USD 15,348,299.00
Tarehe 2 Februari, 2007	USD 4.865,000,00
Tarehe 25 Mei, 2007	USD 13,813,469.00
Tarehe 19 Juni, 2007	USD 1,534,830.00
Jumla	USD 35,561,598.00
	Tsh 44.5 bilioni

Kwa hali hii malipo hayo ni zaidi ya kiasi cha Barua ya Dhamana ya Benki cha USD 30,696,598.00 iliyofunguliwa kupitia CRDB Bank Ltd kwa niaba ya Richmond Development Company LLC, tarehe 11 Septemba, 2006. Kiasi hicho pia ni zaidi ya kiasi cha Barua ya Dhamana ya Benki iliyofunguliwa na CRDB Bank Ltd kwa Dowans

[77] Barua Kumb. Na. DST/MP/PSO/P/63/102 ya tarehe 18/05/2007

[78] Barua Kumb. Na. DST/MP/PSO/P/63/102 ya tarehe 20/06/2007

[79] Barua Kumb. Na 5659 ya tarehe 28/12/2007

Holdings Limited baada ya kuhuisha Mkataba wa Richmond Development Company LLC kwa Dowans Holdings S.A tarehe 28 Disemba, 2006, kwa thamani ya USD 30,696,598.00.

Fedha zilizolipwa zaidi nje ya Barua ya Dhamana ya Benki kwa Dowans Holdings S.A ni USD 4,865,000.00 (Tsh 6.1 bilioni). Mkurugenzi Mtendaji wa Dowans Holdings S.A Bwana Guy Picard na Mkurugenzi wake wa fedha Bwana Stanley Munayi waliiambia Kamati Teule kwamba hawajui kama Dowans Holdings S.A imelipwa ziada ya US$ 4,865,000.00. Taarifa hizo zinapishana na taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania inayoonyesha kwamba Dowans Holdings S.A wamelipwa kiasi hicho.

Kamati Teule imeshangaa ni vipi malipo hayo yafanyike nje ya Barua ya Dhamana ya Benki iliyofunguliwa kwa masharti ya kumwezesha Richmond Development Company LLC/sasa Dowans Holdings S.A kuweza kugharamia maandalizi ya usafirishaji wa mitambo *(Mobilization Cost)*.

Kifungu 4.5(c) cha Mkataba kati ya TANESCO na Richmond Development Company LLC, kinasema ifuatavyo:-

> *"For the Mobilization Costs a letter of credit (LC) shall be established within seven days after signing of the Contract. TANESCO, BoT, MoF, and RDVECO, shall 'jointly agree' on the terms and conditions"*

Moja kati ya gharama zinazojumuishwa katika *"Mobilization costs"* ni gharama za usafirishaji. Hii ilithibitishwa tarehe 3 Julai, 2006 wakati Richmond Develoment Company LLC ilipowasilisha maombi ya asilimia 35 ya gharama za Mkataba kuitaka TANESCO kufungua Barua ya Dhamana ya Benki na kuambatanisha Hati ya Madai ya Makadirio *(Proform Invoice)* ya USD 30,698,598.00 ili iweze kununua na kusafirishia mitambo. Kamati Teule haioni sababu za msingi Dowans Holdings S.A kulipwa USD 4,865,000.00 nje ya Thamani ya Barua ya Dhamana ya Benki na ni vipi fedha hizo zimeweza kutolewa katika Akaunti Maalum *(escrow)* zaidi ya USD 30,698,598 zilizoidhinishwa awali. Hadi kufikia tarehe 27 Disemba, 2007 Dowans Holdings S.A na CRDB Bank Ltd walithibitisha kwamba hapakuwa na Barua ya Dhamana ya Benki mpya iliyokwisha funguliwa kati ya TANESCO na Dowans Holdings S.A kuwezesha malipo ya ziada kufanyika.

4.9 Madai na malipo ya Dowans Holdings S.A ya *Capacity* na *Interim Energy* Januari 2006 hadi Oktoba, 2007

Kati ya Januari 2007 hadi Oktoba 2007, Dowans Holdings S.A imewasilisha TANESCO hati za madai kwa malipo ya uwekezaji na uzalishaji wa umeme kama inavyoneshwa katika mchanganuo ulioambatanishwa kwenye taarifa hii ambao unaonesha kuwa:

(a) Jumla ya madai ya uzalishaji na mauzo ya umeme ya kipindi cha Januari, 2007 hadi Oktoba 2007 ni US$ 16,487,495.46.

(b) Jumla ya madai ya uwekezaji wa mitambo, *(Capacit charge* – Oktoba, 2007) ni US$ 4,373,738.40.

Hadi kufikia Mwezi Disemba 2007 Dowans Holdings S.A inatamka kwamba TANESCO haijawalipa madai yao kuanzia Januari 2007 hadi Novemba 2007 na Benki ya CRDB Bank Ltd imethibitisha kwamba haijafungua Barua ya Dhamana ya Benki nyingine baada ya ile ya awali ya US$ 30,696,598.00 kuisha kutumika.

Tarehe 28 Novemba 2007 baada ya kupeleka Hati Namba 011 kutoka Dowans Holdings S.A, TANESCO ilimwandikia Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini kuhusu mchakato wa kufidia madeni ya gharama za ucheleweshaji wa umeme na marejesho ya malipo ya awali kwa Barua ya Dhamana ya Benki ya US$ 30,696,598.00 kama ifuatavyo:-

(i) Fidia ya gharama za ucheleweshaji wa uzalishaji umeme *(liquidated damages)* kufuatana na Kifungu 4.4 cha Mkataba kati ya TANESCO na Richmond Development Company LLC. (US$ 10,000.00) kwa siku 243 za ucheleweshaji, sawa na US$ 2,430,000.00.

(ii) Marejesho ya Malipo ya Awali *(Advance Payment)* US$ 1,279,026.00.

Thamani hizo (i) na (ii) zikatwe kutoka Hati ya Madai Namba 011 ya tarehe 5 Novemba, 2007, kutoka Dowans Holdings S.A.[80]

Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha, Benki Kuu ya Tanzania na TANESCO kwa pamoja wanawajibika kuhakiki na kuthibitisha kwamba malipo yote yanarejeshwa kama ilivyokubalika katika mikataba. Malipo yanaanza rasmi kuanzia tarehe 4 Oktoba, 2007, siku ambayo uzinduzi wa mitambo ulifanyika.

[80] Barua Kumb. Na. DF/MF/PAMP/GAS PLANT ya tarehe 28/11/2007

5.0 TAARIFA ZA TAKURU/PPRA

5.1 Chimbuko la Uchunguzi

Kupewa kwa Richmond Development Company LLC zabuni ya kuzalisha umeme wa dharura MW 105.6 na baadaye kuingia mkataba na TANESCO kulizua mjadala wa manung'uniko ya wananchi wa kada mbalimbali walioshuhudia kushindwa kwa Richmond Development Company LLC kutekeleza mradi huo kwa muda kama ilivyokuwa imekubalika kwenye mkataba. Umma wa Watanzania wa kawaida, Wanasiasa, wasomi, wanataaluma, wanahabari, na wadau mbalimbali hawakusita kulalamika kwa kuhisi uwezo mdogo wa kampuni hiyo. Hisia hizo zilijengeka kutokana na historia isiyoridhisha ya utendaji ya Richmond Development Company LLC nchini, dalili za mapema za kushindwa kutekeleza mradi huu, na taarifa za wadau mbalimbali kutoka Marekani wenye kufahamu shughuli ambazo kampuni hiyo inafanya ambazo hazihusiani kabisa na masuala ya umeme.

Kufuatia hali hiyo, baadhi ya Taasisi kwa kutumia mamlaka waliyonayo kwa mujibu wa sheria na taratibu zao za kazi zilifanya utafiti kuchunguza mchakato mzima wa zabuni ulivyofanyika.

Taasisi zilizofanya uchunguzi wa zabuni hiyo ni pamoja na:

- Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), na
- Taasisi ya Kuzuia Rushwa (TAKURU) ambayo sasa ni Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)

Pamoja na taasisi hizo kufanya uchunguzi bado mshangao wa kutolewa zabuni hiyo kwa Richmond Development Company LLC uliendelea hata kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Kamati yake ya Kudumu ya Uwekezaji na Biashara, na vyombo mbalimbali vya habari hususan magazeti. Kwa pamoja walionyesha mashaka ya mzabuni Richmond Development Company LLC kupewa kazi hiyo pasipo kuzingatia sheria, kanuni na taratibu.

Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara ambayo ni msimamizi wa shughuli za Serikali kwa upande wa Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko, ilipowasilisha taarifa yake ya utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa mwaka 2006[81] mwezi Novemba 2007, ilionyesha mashaka yake kuhusu namna Richmond Development Company LLC ilivyopewa kazi ya kufunga mitambo ya kuzalisha umeme wa megawati 100 na hadi ilivyoshindwa kutekeleza kazi hiyo. Kamati hiyo ya Bunge haikuridhishwa na utendaji kazi wa Richmond Development Company LLC na baadaye mrithi wake Dowans Holdings SA kushindwa kutekeleza kazi hiyo kwa muda kama ilivyokubaliwa katika mkataba.

Utata wa utekelezaji wa kazi hiyo ulionekana kwa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara mapema katika ziara zilizofanywa na Kamati hiyo katika kipindi cha mwezi Januari hadi Mei 2007 za kutembelea na kukagua mitambo ya kuzalisha umeme iliyopo

[81] Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara kuhusu Utekelezaji wa Shughuli za Kamati kwa mwaka 2006

TANESCO – Ubungo kwa nyakati tofauti na kuonyeshwa mtambo wenye uwezo wa kuzalisha MW 20 ulioletwa na Richmond Development Company LLC na mitambo mingine ya MW 40 iliyoletwa na Kampuni ya Dowans Holdings SA, ambayo ilikuwa imefungwa kwa kipindi hicho.

Katika taarifa yake, Kamati ya Uwekezaji na Biashara ilitaka kupata majibu ya maswali mbalimbali ambayo katika hali ya kawaida majibu yake hayakuweza kupatikana mara moja kwa kipindi hicho. Maswali hayo ya msingi yanayohusu miiko, maadili na taratibu za kazi za Serikali, uadilifu, umakini na uwajibikaji katika utendaji kazi, ambayo hayakuangaliwa na yanadai majibu ya uhakika ni haya yafuatayo:

(i) Je, ni sababu zipi za msingi zilizosababisha Serikali kuacha kuifanyia uchunguzi wa awali *(due deligence)* Kampuni hiyo ya Richmond ili kujua uwezo wa kampuni hiyo kifedha, kitaalamu na kiutendaji?

(ii) Je, Serikali ilipata fursa ya kuikagua kwa dhati tovuti ya kampuni hiyo?

(iii) Je, ni sababu zipi za msingi zilizoisukuma Serikali kufumbia macho udhaifu wa Richmond uliojidhihirisha awali kwenye mradi mwingine mkubwa kitaifa, yaani mradi wa Bomba la Mafuta (Dar es Salaam – Mwanza)?

(iv) Je, Serikali ilipewa ushahidi wowote wa kimaandishi kuhusu uhusiano wa kisheria wa kampuni hizo mbili? Je, kwa nini basi mkataba wa mwisho wa kuzalisha umeme wa dharura nchini, haukutajwa wala kuihusisha kwa namna yoyote ile kampuni ya Pratt & whitney?

(v) Je, ni sababu zipi zilizoifanya Serikali iruhusu kufunguliwa *Letter of Credit* ya uingizaji wa mitambo ya Kampuni ya Richmond?

(vi) Ni kiasi gani cha hasara nchi imepata kwa mradi huu kutokamilika ndani ya muda wa dharura ya umeme?

Maswali haya yakashindwa kupata majibu ya kuridhisha kutokana na msimamo wa Serikali kwamba mikataba ya kibiashara kati ya Serikali na makampuni ya nje ni siri hata kwa Bunge lenye mamlaka kikatiba kusimamia shughuli za Serikali.

Miezi miwili tu baada ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara kuwasilisha kwa Spika taarifa yake ya mwaka 2006, iliyolalamikia kushindwa kupata majibu hayo, na hivyo kupendekeza kuundwa kwa Kamati Teule, Bunge lilipewa majibu rasmi na Serikali kupitia kwa Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji Mhe. Gaudence Kayombo, (Mb) wakati akijibu Swali Na. 102 lililoulizwa

na Mhe. Masolwa C. Masolwa, (Mb) tarehe 19 Aprili 2007 aliyetaka Serikali kuruhusu Kamati za Bunge kupitia mikataba ya kibiashara iliyoingiwa na Serikali na taasisi zake isiyo na tija kwa nchi. Naibu Waziri alisema:

> *"Serikali haiko tayari kuzipa Kamati za Bunge mikataba ya aina hii maana ni ya utendaji na kibiashara kati ya mwekezaji na Serikali. Best practice kote duniani ni kutoitangaza aina hii ya mikataba".*

Baada ya jibu hili kuzua swali la nyongeza kutoka kwa Mbunge wa Karatu Mhe. Dk. Wilbrod Slaa (Mb.) lililosisitiza kuwa dhana ya kusimamia ni pamoja na kuona mikataba, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji Dk. Juma Ngasongwa (Mb.), alisimama Bungeni na kutamka kuwa:

> *"Mikataba hii ni siri; na best practice duniani kote ni kwamba mikataba hii inashughulikiwa na Serikali na wafanyabiashara. Bunge jukumu lake ni kuihoji Serikali; na mimi nafikiri kuhoji tunahojiwa sana na moja ya kazi ya kuhoji ni hii tunayotoa maelezo hapa. Kwa hiyo, mimi nafikiri suala la mipaka tulizingatie na best practice tulizingatie."* [82]

Ni kutokana na msimamo huu wa Serikali, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara ikatoa hoja ya kuundwa kwa

[82] Taarifa Rasmi za Bunge HANSARD ya tarehe 19/04/07

Kamati Teule itakayokuwa na uwezo kisheria wa kuchunguza mchakato wa zabuni hiyo na Mkataba kati ya TANESCO na Richmond Development Company LLC, na kwamba Kamati Teule ingefanya kazi kwa vigezo vipana zaidi kuliko vile vilivyofanywa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

5.2 Taarifa ya Mamlaka ya Udhibiti na Ununuzi wa Umma (PPRA)

Kwa ujumla taarifa ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) iliangalia kama Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma zilifuatwa. Taarifa hiyo imebainisha wazi kuwa pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kutaka kuiokoa nchi kutokana na hali mbaya ya umeme mchakato mzima wa zabuni ulikiuka Sheria ya mwaka 2004 na Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2005. Mambo yaliyobainika na kuelezwa katika taarifa ya PPRA yamechambuliwa kwa kina katika Sehemu ya 2.0 ya taarifa hii. Kwa mfano kupunguzwa kwa siku za kutangaza zabuni kutoka 45 hadi 10, na TANESCO kwa kushinikizwa na Wizara ya Nishati na Madini kutozingatia ushauri uliotolewa na PPRA na badala yake kutangaza zabuni hiyo tarehe 27/2/2007.

Mara baada ya kutangazwa kwa zabuni hiyo, vyombo vya habari vilitoa taarifa kuhusiana na ukiukwaji wa taratibu za ununuzi, hali iliyopelekea PPRA kuchukua jukumu la kufuatilia kwa kina taarifa hizo kwa kuomba nyaraka zote zilizohusu zabuni hiyo.

Katika uchunguzi uliofanywa na PPRA mambo mbalimbali yalibainishwa, kwa mfano, kukiukwa kwa Kifungu 38 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2004, kinachozuia taasisi moja kuingilia ununuzi wa taasisi nyingine. Kila taasisi inatakiwa kufanya ununuzi kwa kutangaza zabuni, kuchambua na kumchagua mzabuni wake ili kuwajibika na uamuzi utakaofanywa na taasisi husika.

Aidha, PPRA ilibaini kuwa Kifungu 42 (a) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ambacho kinatoa maelekezo kuhusu matumizi ya *emergency procurements* hakikutumika ipasavyo na Kifungu 59 (1) cha Sheria hiyo kinachotamka kufanyika kwa zabuni ya ushindani *(International Competitive Tendering)* pia kilikiukwa.

TANESCO pia ilikiuka Kanuni ya 65 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma GN No.97 ya mwaka 2005 kwa kutangaza zabuni kwa siku 10 badala ya siku 45 kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni ambayo inahitaji zabuni kwa njia ya ushindani wa Kimataifa kutangazwa kwa siku zisizopungua 45.

Vilevile, taarifa ya PPRA ilieleza kuwa Kanuni nyingine ambayo haikuzingatiwa ni Kanuni ya 68 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma. Kanuni hii inafafanua utaratibu wa kutumia njia ya *"International Shopping Procurement"* kwa kualika makampuni yanayojulikana kuwa yanatengeneza mitambo ya umeme na kuyaomba kuleta bei zao kwa *"quotations"* njia ambayo inahitaji siku 14 tu kutangaza na kufungua *"quotations".*

Katika kupitia taarifa ya PPRA, Kamati Teule imebaini kuwa kulikuwa na mapungufu kwa upande wa Wizara ya Nishati na Madini kwa kutoifanyia uchunguzi wa kina "*due diligence"* Richmond Development Company LLC ili kuthibitisha uwezo wake kifedha, kiutendaji, kiutaalam na uzoefu wa kazi na hali kadhalika uadilifu wake katika utendaji kama ilivyooneshwa katika *"Company Profile"* yake.

Uamuzi wa Wizara ya Nishati na Madini kuunda kamati ya wataalam ambayo iliwekwa kufanya kazi kama bodi ya zabuni ya TANESCO na Wizara ya Nishati na Madini kuiamuru TANESCO kusaini mkataba ambao haikuujadili kupitia vyombo vyake kisheria ni kitendo cha unyanyasaji.

Kwa kuwa Wizara ilikuwa ndio mnunuzi ilitakiwa kusaini mkataba huo na kuiachia TANESCO kazi ya utekelezaji wa mkataba. Hivyo Kamati Teule imeona kuwa haikuwa sahihi kwa Wizara kuiamuru TANESCO kusaini mkataba husika wakati ununuzi umefanywa na Wizara ambayo ni taasisi tofauti.

Hata hivyo, Kamati Teule inapenda kujua kama Bodi ya Zabuni ya TANESCO ilikiuka taratibu kiasi cha kuifanya Wizara kuchukua uamuzi huo yenyewe je, Bodi hiyo imeshughulikiwa kwa kiasi gani?

Pia inaaminika kwamba mkataba baina ya TANESCO na Richmond Development Company LLC ulisainiwa katika mazingira ya utata

(usiku) Wizara ya Nishati na Madini bila ya kuwepo na muda wa kutosha kwa TANESCO kuupitia kwa makini mkataba huo[83]. Uthibitisho kwamba TANESCO ililazimishwa na Wizara ya Nishati na Madini kusaini mkataba huo bila kuupitia kwa makini umeonekana kwenye barua ya aliyekuwa Mkurugenzi wa TANESCO kwa wakati huo, Bwana Johannes Lottering iliyoandikwa tarehe 26 Juni, 2006.[84] Kitendo cha Mkurugenzi huyo kupewa muda wa saa moja tu kusaini mkataba huo na kuelekezwa kuzingatia maamuzi ya Kamati ambayo hakuhusika nayo ni kudhalilishana.

Kwa ujumla Kamati Teule imeridhishwa na taarifa ya PPRA ambayo imeandikwa kitaalamu ikiwa na vielelezo vya wazi ambavyo Mamlaka imevitumia. Kama ilivyoelezwa hapo awali, mtiririko wa maelezo ya uchunguzi wa mchakato huo kwenye taarifa hiyo pamoja na viambatisho vyake, umeweza kuainisha wazi mambo ambayo yalikwenda kinyume cha Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2004/2005.

Pamoja na Serikali kuwa inaimiliki TANESCO kwa asilimia mia moja na imekuwa mtekelezaji wa miradi ya dharura na ilikuwa ndio mlipaji wa gharama za mpango wa ufungaji wa mashine za kuzalisha umeme wa dharura kupitia fedha za msamaha wa madeni (IMF), Kamati Teule imeona kuwa haikuwa sahihi kwa Serikali kuingilia kati maamuzi ya Bodi ya Zabuni ya TANESCO, kama yalivyoelezwa

[83] Taarifa ya Wakaguzi wa Zabuni kutoka Kilimanjaro International Corporation
[84] Angalia Na. 31

kwenye taarifa ya tathimini (*evaluation report)* ya zabuni iliyofanywa na wataalamu wa TANESCO.

Kamati Teule imebaini pia kuwa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 haijatoa ufafanuzi wowote wa neno *"emergency"*. Hivyo Kamati Teule inashauri kuwa neno hilo lifafanuliwe vizuri katika sheria kwa kueleza wazi ni wakati gani hasa Serikali ifanye jambo fulani kwa dharura ili kuwe na *checks and balances* ambazo zitasaidia kuhakikisha kuwa taratibu za udhibiti na ununuzi wa umma zinafuatwa na kuzingatiwa kama ilivyokusudiwa. Ili kuweka maana hiyo wazi Sheria hiyo iangaliwe upya na kuweka bayana maeneo yote yenye utata na kuyarekebisha kwa ajili ya kuepuka matatizo kama haya kwa siku zijazo.

Aidha, Kamati Teule imeona kuwa Sheria ya Ununuzi wa Umma haina nguvu ya kisheria (meno) ya kutosha kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha kwamba ununuzi wa umma unaboreshwa zaidi kwa kuongeza ushindani wa ukweli na uwazi na hivyo kuipa Serikali thamani halisi ya pesa yake. Kwa mujibu wa sheria iliyopo PPRA imekuwa ikitumia njia ya kutoa ushauri kuhusu taratibu za ununuzi jambo ambalo Kamati Teule imeona kuwa ni vema Mamlaka hii ikapewa nguvu za kisheria pamoja na kuhamishiwa Ofisi ya Rais ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

5.3 **Taarifa ya TAKURU**

TAKURU (sasa TAKUKURU) iliamua kufanya uchunguzi wa zabuni iliyoipa ushindi Richmond Development Company LLC baada ya mchakato huo kulalamikiwa na wananchi na vyombo vya habari kuwa uligubikwa na rushwa.

Kwa ujumla uchunguzi uliofanywa na TAKURU ulijikita katika kuthibitisha tuhuma zilizoainishwa, kama vile:-

- Kufahamu wamiliki wa Kampuni ya Richmond,
- Kufahamu iwapo utaratibu wa zabuni ulifuatwa na iwapo kulikuwa na upendeleo,
- Kufahamu kiasi cha fedha kilicholipwa kwa kampuni ya Richmond baada ya mkataba hadi Kampuni hiyo ilipokabidhi shughuli zake kwa Kampuni ya Dowans Holdings S.A,
- Kufahamu uhusiano uliopo kati ya Richmond na Dowans na sababu zilizofanya Richmond kujiondoa,
- Kufahamu hasara iliyopatikana kutokana na Kampuni ya Richmond kushindwa kuzalisha umeme,
- Kuchunguza kama Kamati ya Wataalam ilifanya uzembe katika kusimamia mchakato husika, na
- Kuchunguza iwapo kulikuwa na kamisheni iliyotolewa kwa Watendaji wakuu Serikalini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na TAKURU ambayo imeeleza kwamba uchunguzi huo ulifanywa kwa “kina na wenye umakini wa hali ya juu’’ yafuatayo yalibainika:-

- Mchakato wa kumpata mzabuni ulikuwa wa wazi na shindanishi,
- Hakuna ushahidi wowote uliopatikana kuthibitisha vitendo vya rushwa, uzembe na hata kupokea kamisheni. Pia hakuna ushahidi uliopatikana wa Afisa yeyote Serikalini kumiliki hisa au kuwa na madaraka Richmond Development Company LLC,
- Kamati maalum iliyoundwa haikupata muda wa kutosha kuifanyia uchambuzi wa kina Richmond Development Company LLC ili kufahamu uwezo wake kiufundi na kifedha na badala yake ilitegemea uwezo wa Kampuni ya Pratt & Whitney kama kigezo cha kuipatia Richmond zabuni,
- Utafiti wa kina haukufanywa kutambua uwezo wa Kampuni ambayo ingepaswa kusimamia shughuli za Richmond Development Company LLC yaani Richmond Development Company (T) Ltd, na
- Uchunguzi wa TAKURU ulithibitisha kwamba mapungufu yalikuwepo, lakini mapungufu hayo ni ya kawaida kiutendaji na hayakuhusisha rushwa au manufaa ya aina yeyote ile kwa watendaji wa Serikali na wala hakuna hasara iliyosababishwa na mapungufu hayo.

Katika kubainisha yaliyoelezwa kwenye taarifa ya TAKURU Kamati Teule imetoa maoni katika uchunguzi huo kwa kuzingatia masuala yafuatayo:-

(i) Mchakato ambao TAKURU imeeleza kuwa ulikuwa wa wazi na shindanishi uliendeshwa na Wizara ya Nishati na Madini bila kuzingatia taratibu za sheria na kanuni za ununuzi wa umma. Kamati Teule imeshindwa kuelewa ni mbinu zipi taasisi hii ilitumia katika kueleza kuwa mchakato wa zabuni ulifanywa kwa uwazi na kuwa shindanishi. Imeonekana wazi kuwa Wizara ilisitisha zabuni kwa kuielekeza TANESCO kuacha kuendelea na zabuni hiyo kwa kuwa tayari timu maalum ilikuwa imeundwa kwa maelekezo ya Waziri Mkuu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mzabuni anapatikana. Je, TAKURU hawakuona kuwa kitendo hicho kilikiuka Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma?

Aidha, Kamati Teule imeona kuwa hakuna ukweli juu ya uwazi na ushindanishi wa mchakato huo kutokana na kubaini kwamba barua pepe[85] za kutaka kufutwa kwa zabuni zilitumwa kwa wazabuni tarehe 19 Juni 2006 wakati Kamati ya Serikali ya Majadiliano (GNT) ilikuwa imeshakaa tarehe 8 – 15 Juni 2006 kwa ajili ya kufanya majadiliano na Richmond Development Company LLC. Pia, vigezo vilivyotumika hadi kuipa ushindi Richmond Development Company LLC viliwekwa kwa ajili ya kuiwezesha kampuni hiyo ishinde na si vinginevyo.

[85] Barua pepe zilizotumwa kwa wazabuni

(ii) Kuhusu usimamizi wa mchakato wa zabuni, taarifa ya TAKURU imeeleza kuwa kulikuwa na mapungufu katika kusimamia utekelezaji wa mchakato huo na kuyaelezea mapungufu hayo kuwa ni ya kawaida ambayo hayajengi makosa ya jinai. Kamati Teule imeona kuwa kupatikana kwa Richmond Development Company LLC kulisababisha Wizara ya Nishati na Madini kuilazimisha TANESCO kusaini mkataba na Kampuni hiyo ambayo imekuwa ikibadili majina kwa nyakati tofauti kama vile kujiita Richmond, RDC, Richmond Development Company LLC na RDEVCO[86]. Je, TAKURU haioni kuwa kubadilisha badilisha majina bila kuzingatia taratibu za sheria ili ipate manufaa kwa kuficha ukweli wa mambo sio kosa kisheria?

(iii) Taarifa ya TAKURU imeeleza kwamba Richmond Development Company LLC ilikuwa ifunguliwe *Letter of Credit* yenye thamani ya Dola za Kimarekani 30,696,598.00. Uchambuzi wa Kamati Teule umebaini kwamba majaribio ya kutaka kufunguliwa kwa LC yalifanyika mara tatu; mara ya kwanza yalifanyika kupitia Citibank (T) Ltd kwenda Citibank New York na kukataliwa kutokana na kutokidhi vigezo; mara ya pili ilifanyika kupitia CRDB (T) Ltd kwenda Citibank New York na ilikataliwa tena kutokana na kutokuwa na utambulisho, tathmini na uwezo wa kutosha kwa Kampuni hiyo na mara ya

[86] Articles of Association of RDEVCO, Mkataba baina ya Richmond Development Company LLC na TANESCO

tatu ilifanikiwa kupitia HSBC Bank kwenda Citibank New York. Je? TAKURU hawakuona kwamba mchakato wa ufunguzi wa *LC* hiyo ulikuwa umetawaliwa na ujanja ambao Richmond Development Company LLC iliutumia ili kuendeleza mradi wakati haikuwa na fedha?

(iv) Kuhusu hasara ambayo nchi imepata kutokana na mradi huo, Kamati Teule imeona kuwa Taarifa ya TAKURU imeshindwa kueleza wazi hasara ambayo nchi imepata kutokana na kuchelewa kufungwa kwa mitambo hiyo licha ya kuelezwa kwamba Richmond Development Company LLC ilikuwa iilipe TANESCO kiasi cha Dola za Kimarekani 10,000 kwa siku kama fidia ya ucheleweshaji wa kuzalisha umeme. Kiasi hicho cha pesa ni kidogo mno na ni hasara kwa Taifa kama tulivyojadili kwenye sehemu ya 4.0 ya taarifa hii.

Pamoja na kuwepo kwa hisia za mashaka ya wingu la rushwa, kubebwa au kuipendelea Richmond Development Company LLC bado taarifa ya TAKURU imeshindwa kubaini mianya ya rushwa katika hatua zote za mchakato kwa kile ilichodai kuwa ni kutokana na kukosekana kwa ushahidi wowote uliowahusisha vigogo na watendaji wakuu wa Serikali ambao kwa namna moja au nyingine walishiriki katika mchakato huo. Ingawa uchunguzi huo ulifanywa kwa kuchelewa ni wazi kuwa kuchelewa huko kusingeiwezesha taasisi hii kuona moto wala

moshi, lakini, ilikuwaje hata ishindwe kubaini uwepo wa majivu?

(v) Taarifa ya TAKURU imeendelea kubainisha kwamba hakukuwa na uzembe katika mchakato huo. Kamati Teule imeona kuwa kitendo cha kampuni hii kuchaguliwa kwa kuwa ilionesha kwamba itashirikiana na kampuni kubwa ya kimataifa ya Pratt and Whitney baada ya kuithibitishia Kamati ya Serikali ya Majadiliano kupitia kigezo cha kuonyeshwa Business Card, kufanyiwa *power point presentation*, mkutano kwa njia ya simu (*Teleconference)* na kuwasilisha *proprietary information agreement* havitoshi kumfanya mtu aamini juu ya mahusiano bila ya kuwa na mkataba baina ya pande hizo mbili *"consortium agreement"*. Kwa mantiki hiyo, ilikuwa rahisi kwa Pratt & Whitney kuiacha Richmond Development Company LLC bila maelezo yeyote. Kamati Teule imeona kuwa kushindwa kwa GNT kudai uthibitisho halisi wa mahusiano ya kisheria ya pande hizo mbili na kutokuifanyia *(post qualification)* Richmond Development Company LLC ni uzembe tosha. Je, TAKURU hawakuliona hilo?

(vii) Kuhusu taarifa hiyo kueleza juu ya kutokuwepo kwa upendeleo wa aina yeyote, Kamati Teule imeshindwa kuafiki juu ya hilo kutokana na kubaini kuwepo kwa dalili hiyo pale ambapo upendeleo umebainika baada ya vigezo vilivyowekwa na TANESCO kupunguzwa mara tatu na katika hatua zote hizo

Richmond Development Company LLC haikufikia. Je, TAKURU haikuona kuwa huo ulikuwa upendeleo?

(viii) Richmond Development Company LLC ilipewa maelekezo/masharti ya kujisajili katika Bodi ya Usajili wa Makandarasi, Bodi ya Usajili wa Wahandisi, Baraza la Usimamizi wa Mazingira (EIA), n.k lakini cha kushangaza mpaka mkataba unasainiwa baina yake na TANESCO maelekezo hayo hayakuwa yametekelezwa na Kampuni hiyo. Licha ya kwamba maelekezo /masharti hayo yalitolewa bila ya kuwepo na muda maalum wa kutekelezwa *"time frame"*, Richmond Development Company LLC hawakusajiliwa katika maeneo hayo na walipotaka kuchukuliwa hatua Kamishna wa Nishati Ndugu Bashir Mrindoko alizuia. Je, huo haukuwa upendeleo?

(ix) Richmond Development Company LLC pamoja na kukosa vigezo vya msingi vya kupewa *Certificate of Incentives* kwa mfano kuonyesha, kupitia *business plan* yao, kuwa ina fedha ya kutosha kutekeleza mradi, na iliweza kusajiliwa bila ushahidi huo.

Ikizingatiwa kuwa TAKURU ni Taasisi nyeti Kitaifa ambayo ina uwezo wa kutosha kielimu, kiuchumi, kiufundi na kitaalamu katika kufuatilia masuala ya kiuchunguzi, Kamati Teule haijaridhishwa

kabisa na taarifa yake ya uchunguzi kutokana na taarifa hiyo kutokuwa ya wazi huku ikificha uhalisia wa mchakato.

Taarifa hiyo ilibaini kuwa yapo mapungufu katika mchakato wa zabuni husika lakini ikayaelezea mapungufu hayo kuwa ni ya kawaida ambayo hayajengi makosa ya jinai kwa kuwa mapungufu hayo yalitokana na msukumo wa hali ya dharura ya kutafuta ufumbuzi wa tatizo la umeme lililoikumba nchi. Kwa upande wake Kamati Teule imeona kwamba kitendo cha Richmond Development Company LLC kushindwa kutekeleza kazi yake kwa muda uliokubalika kwenye Mkataba ni mapungufu ambayo yameitia nchi hasara kubwa.

Pia Kamati ya Serikali ya Majadiliano iliyoundwa haikuifanyia uchambuzi wa kina Richmond Development Company LLC ili kufahamu uwezo wake kiufundi na kifedha na badala yake Kamati hiyo kutegemea uwezo wa Kampuni ya Pratt & Whitney (ambayo ina sifa na umahiri wa eneo hili duniani) kama kigezo cha kuipatia Richmond Development Company LLC zabuni. Kamati Teule imeona kuwa upungufu huo ungeweza kuepukwa kwa kuifanyia uchunguzi wa kina Kampuni hiyo licha ya kwamba kulikuwa na udharura.

Mkurugenzi wa Upelelezi na Makosa ya Jinai wa TAKURU ndugu Alex Mfungo aliitetea Taasisi yake mbele ya Kamati Teule kuwa ilifanya uchunguzi kwa mujibu wa sheria ya mwaka 1971 iliyokuwa na

mapungufu mengi na kwamba ilikuwa vigumu sana kuthibitisha madai ya rushwa yaliyokuwa yanalalamikiwa na wananchi[87].

Pamoja na utetezi huo, Kamati Teule imeona kuwa taarifa ya TAKURU haikuwatendea haki Watanzania kwa kuutatiza zaidi utata kuliko kuutatua. TAKURU inasema kwamba mapungufu iliyoyabaini katika mchakato huo yalikuwa ya kawaida. Je, ni kigezo gani walitumia kupima kwamba mapungufu hayo yalikuwa ya kawaida? Ingekuwa busara kwa taarifa kutoka taasisi nyeti kama hii kuwa ya wazi na kweli ikionesha dhahiri wapi kosa lilitendeka na kama ni kutoa ushauri itoe ushauri ipasavyo kwa manufaa ya wananchi na viongozi wote waliohusika kwa namna moja au nyingine kwenye mchakato huo. Kutokana na maelezo hayo taarifa hiyo imeonekana kujikanganya na kuficha ukweli (*white wash)* wa mambo bila ya kuelewa nini inataka kuueleza umma wa Watanzania.

5.4 Vyombo vya Habari – Magazeti

Vyombo vya habari hususan magazeti vilitoa habari za kutoridhishwa na jinsi mchakato wa zabuni ya kukodi majenereta ya kuzalisha umeme wa dharura ilivyoendeshwa. Habari hizo zilianza kutolewa baada ya Richmond Development Company LLC kushinda zabuni na kuingia mkataba na TANESCO.

[87] Taarifa rasmi za Bunge HANSARD tarehe 27/12/2007 mahojiano na Ndg. Alex Mfungo

Vyombo hivyo vilishambulia taratibu na namna mzabuni huyo alivyoshinda pasipo Serikali kufanya utafiti wa kina juu ya uwezo wake kifedha, kitaalam na uzoefu, wala usahihi wa taarifa zilizotolewa na Richmond Development Company LLC hali iliyoashiria upendeleo wa kubebwa na baadhi ya vigogo Serikalini.

Kamati Teule imepitia baadhi ya magazeti yaliyoripoti juu ya Richmond Development Company LLC kwenye makala, tahariri na hata habari zilizowekwa kurasa za juu za magazeti na kuamsha shauku ya wananchi kuhusu suala hili.[88]

Usiri mkubwa wa mikataba na Serikali kushindwa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati kukakuza shauku ya wananchi ambayo ilimalizwa na vyombo vya habari kwa "habari za kuaminika". Kamati Teule pamoja na kuikubali kazi kubwa ya vyombo vya habari katika kuhabarisha, kutonya na kukosoa mambo yasiyoenda vizuri katika jamii, na pamoja na kuthamini mchango wake katika uchunguzi wa suala hili, ilishindwa kuzitumia kikamilifu baadhi ya taarifa kutokana na kukosa uchunguzi wa kina.

Hata hivyo, Kamati Teule inavipongeza vyombo vya habari kwa kupiga kelele sana kuhusu sakata la Richmond Development Company LLC ingawa hawakuwa na takwimu wala taarifa nyingi muhimu ambazo zingeweza kufichua ukweli halisi wa jambo hili.

[88] Daily News, Mwananchi, This Day, The Citizen, The African, Majira, Sunday Citizen, Rai, Kulikoni, The Express na Mwanahalisi.

Udadisi na uzalendo umeisaidia sana jamii kuelewa na kutaka kujua hatma na mchakato mzima ulivyoendeshwa. Ufuatiliaji wa vyombo vya habari kuhusu suala hili ulikuwa moja ya sababu kubwa kwa Richmond Development Company LLC kujitoa mapema na wapambe wao ndani ya Serikali kuingiwa na woga wa kuwajibishwa.

Mmiliki wa Kampuni hiyo Bwana Mohammed A. Gire alikiri mbele ya Ujumbe wa Kamati Teule uliotembelea Kampuni yake Houston-Texas Marekani kuwa moja ya sababu zilizoifanya kampuni yake kusitisha shughuli zake ni kutokana na kuandamwa kwa kuandikwa na vyombo vya habari.[89] Kuandikwa huku kulimlazimu kuipa kazi Kampuni ya *G&S Media Consultancy* kwa lengo la kupunguza makali ya maumivu aliyokuwa anayapata.[90]

Kamati Teule inakumbushia ahadi ya Serikali ya kuanzisha mafunzo maalum kwa ajili ya kuwawezesha wanahabari kuongeza ujuzi na kujenga uzoefu wa kuhoji na kuandika habari za uchunguzi wenye kina stahili, shughuli ambayo ni sehemu muhimu ya kuimarisha demokrasia na utawala bora nchini.

[89] Taarifa ya ziara ya Ujumbe wa Kamati Teule Houston, Texas - Marekani 10 – 15 Desemba 2007
[90] Taarifa Rasmi za Bunge HANSARD ya tarehe 18 na 19/12/2007 Mahojianao na Ndugu S. Rweyemamu na Dk. Gideon Shoo

6.0 RICHMOND DEVELOPMENT COMPANY LLC NI KINA NANI?

6.1 Utambulisho wake Kisheria

Mshindi wa zabuni ya kuzalisha umeme wa dharura nchini, Richmond Development Company LLC anatambulishwa kwa kina na ufasaha mkubwa katika mkataba kati yake na TANESCO uliosainiwa tarehe 23 Juni, 2006 jijini Dar es Salaam. Mkataba huo katika Utangulizi unaielezea Richmond Development Company LLC kuwa ni kampuni iliyosajiliwa chini ya sheria za Jimbo la Texas, Marekani na yenye anuani ifuatayo: 5825 Schumacher, Houston Texas 77057, Marekani. Aidha, kifungu cha 5.1 (a) cha Mkataba huo kinatoa maelezo ya ziada kuhusu Richmond Development Company LLC kuwa ni kampuni yenye ukomo wa hisa (*limited by shares*) ambayo uwepo wake Tanzania haukinzani na sheria za nchi. Kifungu hicho kidogo kinamalizia kwa kutamka bayana kuwa kampuni hiyo ina nguvu na mamlaka yote stahili ya kikampuni (*all requisite corporate power and authority*) ya kumiliki au kukodisha na kutumia mali zake na kuendesha biashara zake kama ilivyokusudiwa nchini Tanzania.[91]

Hiyo ndiyo sura ya Richmond Development Company LLC kama ilivyoainishwa katika Mkataba huo wa kisheria uliotiwa saini kwa upande wa TANESCO na aliyekuwa Kaimu Mkurugenzi Mwendeshaji wa TANESCO, Johannes G. Lottering na kushuhudiwa na aliyekuwa Kaimu Katibu (*Ag. Company Secretary*) wa TANESCO, Godson Makia

[91] Mkataba baina ya Richmond Development Company LLC na TANESCO wa mwaka 2006

na kwa upande wa Richmond Development Company LLC na Meneja wake, Mohamed Gire na kushuhudiwa na wakili maarufu nchini, Dr. Ringo Tenga ambaye alijitambulisha katika mkataba huo kama Katibu wa Richmond Development Company LLC.

6.2 Hadhi ya Richmond kisheria/kikampuni Marekani

Uchunguzi wa kina uliofanywa na Kamati Teule ndani na nje ya nchi na kwa msaada mkubwa wa Ubalozi wa Tanzania Washington D.C na Wizara yetu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, umetoa picha tofauti kabisa na ile iliyomo kwenye mkataba huo. Kamati Teule imejiridhisha kuwa hakuna kampuni yenye jina la Richmond Development Company LLC iliyokuwa imesajiliwa Jimbo la Texas wakati wa kusaini mkataba huo au iliyosajiliwa baada ya mkataba huo hadi tunapowasilisha ripoti hii kwa Mhe. Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 31 Disemba, 2007.

Hitimisho tulilofikia linashabihiana kwa vigezo vyote na ushauri wa kitaalamu uliotolewa na kampuni mashuhuri ya mawakili ya Virginia, Marekani inayoitwa Hunton & Williams LLP kwa Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO mwezi Oktoba 2006. Katika ripoti yake yenye jumla ya kurasa 19, kampuni hiyo ya mawakili imetamka bayana kuwa hakuna kampuni yenye jina la Richmond Development Company LLC kwenye masijala ya Katibu wa Jimbo la Texas ambaye moja ya majukumu yake ni sawa na ya Msajili wa Makampuni wa Tanzania.

Hunton & Williams LLP wameituhumu Richmond Development Company LLC kwa upotoshaji wa hadhi yake kikampuni (*misrepresentation of its corporate status*) na kutoa tamko lisilo sahihi (*incorrect statement*) kuhusu hadhi yake chini ya sheria za Texas. Ukaguzi wa kumbukumbu za Katibu wa Jimbo la Texas uliofanywa na kampuni hiyo ya mawakili Oktoba 2006, ulionesha kuwa hakuna kampuni yenye jina la "Richmond Development Company LLC" iliyokuwa imeanzishwa na kuendesha shughuli zake jimboni Texas wakati huo.[92]

Aidha, tarehe 10 Oktoba, 2006 gazeti la kila siku la Kiingereza linalochapishwa hapa nchini, *The Citizen,* lilimkariri afisa mmoja katika Jimbo la Texas, Bw. William Pate, akisema makampuni yote yanayofanya biashara halali jimboni humo yana kumbukumbu zake katika ofisi ya Katibu wa Jimbo la Texas. Kwamba, ofisi hiyo haina taarifa au kumbukumbu zozote kuhusu kampuni hiyo inayojiita Richmond Development Company LLC.[93]

Wajumbe wa Kamati Teule waliotembelea Marekani kati ya tarehe 10 na 16 Disemba, 2007 waliambiwa na Bwana Mohamed Gire, mmiliki wa kampuni hiyo iliyoshinda zabuni ya umeme Tanzania, kuwa Richmond Development Company LLC ni jina mbadala la biashara la kampuni yake iitwayo RDEVCO LLC. Bwana Gire ambaye aliamua mkutano wake na Wajumbe wa Kamati Teule ufanyike

[92] Memorandum for the TANESCO Board of Directors, Hunton & Williams LLP,2006
[93] Nakala ya Gazeti la The Citizen la tarehe 10/10/2006

ofisini kwa wanasheria wake, Duane Morris LLP waliopo 3200 Southwest Freeway, suite 3150, jijini Houston, alisisitiza kuwa sheria za Texas zinawaruhusu wafanyabiashara na makampuni kutumia majina mbadala au tofauti na yale yaliyopo kisheria kwa sababu za kibiashara. Kamati Teule iliyazingatia maelezo ya Bwana Gire kwa lengo la kuyafanyia kazi.

Ni kweli kabisa kuwa majimbo mengi nchini Marekani, likiwemo la Texas, yanaruhusu matumizi ya majina mbadala katika biashara au huduma. Kwa Kiingereza majina hayo yanaitwa "*assumed names*" au "*dba*", kwa kirefu: "*doing business as*". Katika nchi nyingine nyingi kama vile Tanzania, Uingereza, Ireland, Australia na baadhi ya majimbo ya Marekani na sehemu za Kanada, neno linalotumika zaidi ni "*t/a*", yaani "*trading as*".

Katika nchi zote hizo, sheria zinaweka taratibu za kuzingatia ili kuepusha vitendo vya kitapeli katika matumizi ya majina mbadala ya kibiashara. Nchini Tanzania na nchi zingine za Jumuiya ya Madola, zipo sheria maalum za usajili wa majina ya biashara tu ambapo kampuni au mfanyabiashara au mtu yeyote yule ambaye kwa sababu za kibiashara au vinginevyo, asingependa kutumia jina lake halali katika biashara fulani, anaweza kusajili jina mbadala kwa biashara hiyo bila kulazimika kuunda kampuni tofauti. Majina mbadala ya kibiashara hapa kwetu Tanzania yanasajiliwa chini ya

Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara (Business Names (Registration) Ordinance) Sura ya 213.

Nchini Marekani vilevile, huwezi ukakurupuka tu na kuanza kutumia jina mbadala la biashara bila kupitia usajili maalum ambao unawawezesha watu wengine kukagua jalada la majina hayo mbadala kwa lengo la kupata utambulisho kamili wa wanayoyatumia. Vilevile, sheria zinalazimu majina hayo kuchapishwa magazetini kwa lengo la kuutaarifu umma. Lengo, kama tulivyodokeza awali, ni kulinda raia wema dhidi ya vitendo vya udanganyifu. Katika Jimbo la Texas ambako Bwana Gire anaishi, ni kosa la jinai kutumia jina mbadala bila kulisajili. Usajili wa jina mbadala unadumu kwa miaka mitano ambapo mtumiaji lazima asajili jina hilo upya kati ya tarehe 1 Januari na 31 Disemba ya mwaka wa tano.

Sasa je, ni kweli kwamba jina la Richmond Development Company LLC ni jina mbadala la kampuni ya Bwana Gire iitwayo RDEVCO LLC? Je, jina hilo lilisajiliwa ipasavyo? Katika kujibu maswali hayo mbele ya mawakili wake wawili, Bwana Gire aliwakabidhi Wajumbe wa Kamati Teule hati ya uthibitisho ya Harris County, Texas ambayo kwa maoni yake, ilikuwa inathibitisha kuwa Richmond Development Company LLC ni jina mbadala la biashara![94]

[94] Certificate of Operation under Assumed Name. August 28, 2003

Kamati Teule imeikagua hati hiyo kwa kina na kuona kuwa badala ya kumsaidia Bwana Gire, inazidi kuthibitisha kuwa si mfanyabiashara mwadilifu ila tapeli kwa sababu kuu mbili:

(a) Mbali na kwamba hati hiyo ya Bwana Gire ni kivuli tu au nakala ya "hati" halisi (kama ipo), nakala ambayo haina uthibitisho wowote wa uhalali na uhalisia wake, ilikuwa ina saini ya afisa mmoja tu badala ya wawili walioainishwa katika hati hiyo;

(b) Badala ya hati hiyo kutamka kuwa RDEVCO LLC imesajili jina la Richmond Development Company LLC kama Bwana Gire alivyotaka Kamati Teule ielewe, hadithi mpya kabisa inaanzishwa kuwa Richmond Development Company ni jina mbadala lililosajiliwa na Richmond Development Company LLC! La kushangaza ni kuwa katika baadhi ya barua zake alizoiandikia TANESCO na Wizara ya Nishati na Madini, Bw. Gire anatamka kuwa Richmond Development Company ni jina mbadala la biashara la RDEVCO LLC.[95]

Unaweza kudanganyika ukafikiri kuwa kiwango hiki cha ubabaishaji hakithibitishi utapeli pekee, bali vilevile elimu duni ya mmiliki wa kampuni hizo, Bwana Gire, inayomfanya asione hatari kubwa anayojitwalia ya hata kumfikisha jela kwa udanganyifu huu. Lakini kwa mfanyabiashara mzoefu aliyejizungushia mawakili wa kumtetea mambo yakimwendea mrama, anajua analolifanya. Hivyo basi, Richmond Development Company LLC ni kampuni ya kimakusudi, ya

[95] Barua ya Richmond Development Company ya Novemba 9,2006

kimkakati ambayo haikamatiki, haishitakiki, haipigiki faini na haiadhibiki kwa lolote lile itakalolifanya kwani haina uhai wa kikampuni (*corporate personality*).

Pamoja na Bwana Gire kuamua kufanyia mkutano wake na Wajumbe wa Kamati Teule ofisini kwa wanasheria wake na si ofisini kwake mwenyewe, Wajumbe walihakikisha kuwa wanatembelea mtaa unaotajwa kwenye mkataba kuwa ofisi za Richmond Development Company LLC, yaani 5825 Schumacher, Houston Texas, 77057, USA. Anuani hiyo ikawafikisha kwenye jengo lenye jina la Richmond Printing LLC, jina walilothibitisha kuwa la kampuni iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Kampuni yenye Ukomo wa Hisa ya Texas (*Texas Limited Liability Company Act*) tarehe 1 Agosti, 1994 kwa madhumuni ya kuendesha biashara ya uchapishaji na biashara zingine zinazoruhusiwa na sheria kwa kampuni ya aina hiyo.[96] Kampuni hiyo ilianzishwa ikiwa na mwanahisa na meneja mmoja tu kwa jina Mohamed Gire.

Aidha, Wajumbe wa Kamati Teule wakatambua kuwa jengo hilo la Richmond Printing LLC linatumiwa vilevile kama ofisi za RDEVCO LLC, kampuni ambayo ilisajiliwa chini ya sheria hiyo hiyo ya Texas tarehe 11 Septemba, 2003 ikiwa na madhumuni mapana ya kujishughulisha na "biashara yoyote halali".[97] Kampuni hiyo vilevile ilianzishwa ikiwa na mwanahisa na meneja mmoja tu kwa jina

[96] Articles of Organisation of Richmond Printing LLC, of 01/08/ 1994
[97] Articles of Organisation of RDEVCO

Mohamed Gire. Tunalazimika kusema kuwa jengo hilo vilevile ni "makao makuu" ya kampuni hewa ya Richmond Development Company LLC. Licha ya kutumia jengo moja, kampuni zote hizo zinamhusu mtu mmoja, Mohamed Gire, na zinatumia anuani moja. Kutokana na uchambuzi huu, ni wazi kuwa maelezo yaliyomo kwenye utangulizi wa Mkataba kati ya Richmond Development Company LLC na TANESCO kuwa chombo hicho cha biashara cha Bw. Gire ni "kampuni iliyosajiliwa chini ya sheria za Jimbo la Texas", si sahihi hata kidogo.

6.3 Hadhi ya Richmond kisheria/ kikampuni Tanzania

Richmond Development Company LLC si jina geni nchini Tanzania. Jina hili lilianza kusikika nchini kwa mara ya kwanza mwaka 2003 na kwa kishindo likihusishwa na mradi mkubwa wa takriban shilingi bilioni 400 wa ujenzi wa bomba la mafuta la urefu wa kilometa 1,150 kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza.

Katika barua yake ya kujitambulisha iliyotumwa kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) tarehe 28 Mei, 2003, Richmond Development Company wakati huo ikijiita kwa kifupi RDC, ikajitambulisha kuwa kampuni yenye uzoefu wa zaidi ya miaka 25 katika miradi ya nishati na kwamba imekamilisha miradi mbalimbali ya aina hiyo kwa zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 500 katika nchi

zinazoendelea. Kutokana na wasifu huo, TPDC ikawapa RDC nakala ya ripoti ya upembuzi yakinifu iliyofanywa na kampuni ya COWIconsult (Tanzania) Consulting Engineers and Planners Ltd mwaka 1997 ili kupata taarifa za awali kuhusu mradi huo. Aidha Wizara ya Nishati na Madini ikairuhusu RDC kuleta mapendekezo ya awali kuhusu mradi huo.

Mapema mwezi Oktoba, 2003 Wizara ikapokea mapendekezo ya awali ya mradi kutoka RDC ambayo yalipitiwa na wataalamu wa Wizara na TPDC na kukutwa na mapungufu mengi yakiwemo: kukosekana kwa tathmini za kifedha na za kiuchumi za mradi, kukosekana kwa tathmini za mazingira, na kukosekana kwa mpango wa kuwapa makazi waathirika katika njia ya bomba. Kutokana na mapungufu hayo, Wizara ikasita kuipa RDC mradi huo muhimu na kuitaka kampuni hiyo kwanza irekebishe mapungufu yote yaliyojitokeza. RDC nayo ikaweka sharti la kupewa upendeleo wa kutoruhusu kampuni nyingine kwenye mradi huo kwa kipindi maalum (*exclusivity period*) ili kukamilisha kazi hiyo bila wasiwasi wa kunyang'anywa mradi.

Tarehe 30 Juni, 2004 Mhe. Daniel Yona, wakati huo Waziri wa Nishati na Madini na Bwana Mohamed Gire, wakati huo akijiita Mwenyekiti wa RDC, wakasaini mkataba wa awali (*Memorandum of Understanding*) ulioipa RDC *exclusivity period* ya miezi 18 kufanya upembuzi yakinifu wa kina. Mkataba huo, pamoja na mambo mengine, uliitaka RDC kuipa Wizara ripoti za maendeleo ya

utekelezaji wa mradi kila baada ya miezi sita na uliipa Wizara jukumu la kuhakikisha kuwa mradi huo unatekelezwa na RDC mara baada ya zoezi la upembuzi yakinifu wa kina kufanikishwa.[98]

Tangu mkataba huo usainiwe, RDC haikuonekana tena ikijishughulisha na utekelezaji wa sehemu yake ya mkataba. Kumbukumbu za mawasiliano kati ya Wizara na kampuni hiyo, zimetawaliwa na malalamiko ya watendaji wa Wizara kuhusu ubabaishaji wa RDC. Hatimaye, tarehe 9 Januari 2006 Ndugu Bashir J. Mrindoko, kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, akaiandikia barua RDC kuitaarifu kuwa mkataba kati yake na Wizara kuhusu bomba la mafuta ulikoma tarehe 30 Disemba, 2005 na wawekezaji wengine sasa wanapewa fursa kuendelea na mradi huo.

Sehemu ya barua ya Katibu Mkuu inasomeka hivi: "*The Ministry of Energy and Minineral (sic) notes with regret that throughout the 18 month exclusivity period, in spite of several reminders, the Richmond Development Company failed to honor its obligations as provided for in Art.2.1 and 2.2 of the Memorandum*". (Wizara inasikitika kuwa kwa kipindi chote cha miezi 18 ya upendeleo, Richmond Development Company, pamoja na kukumbushwa mara

[98] Memorandum of Understanding between Richmond Development Company na Ministry of Energy and Minerals, 2004

kwa mara, ilishindwa kuheshimu wajibu wake kama ulivyoainishwa katika Ibara ya 2.1 na 2.2 ya Mkataba).[99]

Turejee kwenye hoja ya awali ya kupima ukweli uliomo kwenye kifungu cha 5.1 (a) cha Mkataba kati ya TANESCO na kampuni hiyo ya Richmond tulichokinukuu awali kinachosema Richmond Development Company LLC ni kampuni yenye ukomo wa hisa ambayo uwepo wake Tanzania haukinzani na sheria za nchi na kwamba kampuni hiyo ina nguvu na mamlaka yote stahili ya kikampuni ya kumiliki au kukodisha na kutumia mali zake na kuendesha biashara zake nchini.

Katika kupima ukweli wa kauli hizo ndani ya mkataba, kikwazo kikubwa cha mwanzo ambacho Kamati Teule ilikipata kilikuwa ni msingi wa kuichunguza Richmond Development Company LLC kama kampuni wakati uhalali wake kama kampuni huko ilikotoka unabishaniwa au kwa lugha iliyonyooka, haupo. Richmond Development Company LLC, kwa maneno mengine, si kampuni ya mchana bali ya usiku, kampuni ya mfukoni au ya sanduku la barua (*mail box company*)! Hiyo ndiyo kampuni ambayo shirika la umma, TANESCO, iliingia nayo mkataba wa mabilioni ya fedha za walipa kodi wa Tanzania.

Kampuni ya wanasheria ya Kimarekani ya Hunton & Wiliams LLP iliyopewa kazi na Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO kuichunguza

[99] Barua Kumb. Na. CBC. 105/229/02 ya 09/01/2006

Richmond Development Company LLC, kama tulivyoeleza hapo awali, inathibitisha kuwa tarehe 23 Juni, 2006 siku ambayo mkataba huo ulisainiwa, Richmond Development Company LLC haikuwa na nguvu za kisheria wala mamlaka yoyote ya kikampuni kuiwezesha kuendesha shughuli zake Tanzania.

Kamati inaamini kuwa wamiliki au waendeshaji wa kampuni hiyo wanaotambulishwa kwenye tovuti ya kampuni hiyo (www.rdevco.com), Bwana Mohamed A. Gire na Dk. Mohammed S. Huque, waliliona tatizo hilo na kuamua siku 19 tu baada ya kusainiwa kwa Mkataba huo kusajili kampuni mpya kwa jina la Richmond Development Company (T) Limited yenye makao yake makuu jijini Dar es Salaam. Kampuni hiyo mpya ilisajiliwa tarehe 12 Julai, 2006 na kupewa Hati ya Usajili nambari 57014 ikiwa na wanahisa wawili, kwa majina:

1. Richmond Development Company LLC yenye anuani ya 5825 Schumecher (*tunadhani ni Schumacher*), Houston – Texas 778057, USA (hisa 750,000), na
2. Naeem Gire wa S.L.P. 1998, Dar es Salaam (hisa 250,000).

Kwa kusajili kampuni hiyo mpya, ni dhahiri kuwa wamiliki wa kampuni hiyo walitaka wasibanwe na Kifungu cha 434 cha Sheria ya Makampuni ya Tanzania (Na. 12 ya 2002) kinachotamka wazi kuwa kampuni zote za nje ambazo zinaanzisha ndani ya nchi mahali pa biashara (*a place of business*), zinawajibika kuwasilisha kwa Msajili

wa Makampuni taarifa mbalimbali za kampuni ndani ya siku 30 toka zianzishe mahali pa biashara, kama vile: sheria au mkataba unaoelezea muundo wa kampuni (*charter, statutes or memorandum and articles of association*); orodha ya wakurugenzi na katibu wa kampuni; anuani kamili ya ofisi kuu ya kampuni; na nakala ya taarifa ya mahesabu ya kampuni na shughuli za kampuni.

Kwa kutekeleza masharti yote chini ya kifungu cha 434 cha Sheria ya Makampuni ya 2002, kampuni ya nje itathibitishwa na Msajili wa Makampuni kuwa imetimiza masharti. Uthibitisho huo utakuwa ushahidi kamili wa usajili wa kampuni hiyo ya kigeni nchini ambao utaipa kampuni hiyo haki sawa na kampuni iliyosajiliwa Tanzania katika kumiliki ardhi. Ni dhahiri kuwa taarifa zinazodaiwa chini ya kifungu hicho cha sheria zisingeweza kutolewa na Richmond, kwa sababu kampuni hiyo isiyo na usajili stahili Marekani haiwezi kuwa nazo.

Pamoja na juhudi hizo za wamiliki wa kampuni ya Richmond Development Company LLC, Kamati Teule ilibaini kutokana na ushauri mbalimbali iliopata wa kisheria, kuwa tatizo la uhalali wa Richmond ya Tanzania lilikuwa palepale kwani kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Makampuni kinataka watu wawili au zaidi kuwa na uwezo wa kufungua kampuni. Kwa kuwa mmoja wa wanahisa waliofungua kampuni hiyo ya Richmond ya Tanzania ni Richmond Development Company LLC ya Marekani (yenye asilimia 75 ya hisa zote za

kampuni hiyo iliyosajiliwa Tanzania) na kwa kuwa kampuni hiyo ya kimarekani haijasajiliwa Marekani wala hapa Tanzania kwa mujibu wa kifungu cha 434 cha Sheria ya Makampuni na kwa kuwa, kutokana na hiyo sababu, kampuni hiyo ya kimarekani haina nguvu wala mamlaka stahili ya kikampuni, Richmond Development Company (T) Limited ina mwanahisa mmoja tu kwa jina Naeem Gire, hali ambayo haikubaliki kisheria.

Ni wazi kuwa picha iliyojengwa kwenye mkataba tunaouongelea hapa kuhusu hadhi na uhalali wa Richmond Development Company LLC nchini Tanzania ilikuwa ya kisanii, ya uongo na isiyo na msingi wowote kisheria.

Kinachosikitisha hapa ni kuwa mwezi Februari, 2006, yaani mwezi moja tu baada ya Wizara ya Nishati na Madini kuiandikia barua Richmond Development Company LLC kuwa haina imani nayo, "kampuni" hiyo ya Bwana Gire, ikajitosa kwenye zabuni nyingine ya Wizara hiyohiyo ya Nishati na Madini, zabuni ya kuingiza nchini jenereta za kuzalishia umeme wa dharura wa Megawati 100.

6.4 Uwezo wa Richmond Kifedha, Kitaalamu, Kiutendaji

Tumeeleza kuwa Richmond Development Company LLC iliweza kuaminiwa na Serikali kufanya upembuzi yakinifu wa kina wa mradi wa bomba la mafuta la Dar es Salaam hadi Mwanza kwa kujitambulisha kuwa:

(a) Kampuni hiyo ina uzoefu mkubwa wa zaidi ya miaka 25 katika kuendeleza miradi ya nishati;

(b) Kampuni hiyo inaaminiwa na taasisi mbalimbali za biashara na fedha za Marekani na ina mahusiano ya karibu na Serikali ya Marekani;

(c) Kampuni hiyo imekamilisha miradi mikubwa ifuatayo duniani: kituo cha umeme cha MW 130 cha Gaziantep, Uturuki (gharama za mradi $117 milioni) na utafutaji wa mafuta na gesi kusini mashariki mwa Ulaya ($150 million).[100]

Serikali ingejaribu kuzichunguza sifa hizo za rejareja za Richmond Development Company LLC hata kwa kuuandikia Ubalozi wa Marekani Dar es Salaam au kukagua tovuti yake (www.rdevco.com), ukweli ungelidhihirika kuwa "kampuni" hiyo si chochote wala lolote. Tovuti yake yenyewe imesheheni makosa madogo madogo ya Kiingereza na kupambwa na taarifa za juu juu za miradi ambayo "kampuni" hiyo inadai kuitekeleza, hivyo kuzua maswali mengi na hali inayoashiria upeo mdogo kielimu wa wamiliki wa kampuni hiyo.[101]

Kwa mfano ukurasa wa kwanza wa tovuti hiyo iliyoandaliwa mwaka 2004 unabeba dhamira mbili za "kampuni", lakini dhamira ya kwanza haieleweki, inahitaji mpangilio mpya wa sentensi kwa Kiingereza sanifu. Mbali na makosa madogo madogo ya kisarufi na

[100] Barua ya Richmond Development Company ya tarehe 28/05/2003
[101] Angalia Na. 24

mpangilio, ambayo yamepamba kurasa zote 11 za tovuti hiyo, ukurasa wa 7 unaorodhesha miradi mbalimbali ambayo "kampuni" hiyo ilikuwa inatekeleza: ujenzi wa uwanja wa kisasa wa michezo unaoweza kuchukua watazamani 65,000; ujenzi wa bomba la mafuta la kilometa 1,150 na ukarabati wa viwanja mbalimbali vya ndege nchini Tanzania. Miradi yote hiyo ilikuwa porojo tupu ambazo watendaji wetu Serikalini hawakustahili kuzifumbia macho.

Kama ilivyotarajiwa, "kampuni" hiyo ikashindwa kutekeleza sehemu yake ya mkataba. Mashahidi kadhaa walioongea na Kamati Teule wakati wa uchunguzi, walisema ingelikuwa maajabu kwa "kampuni" ya aina hiyo iliyokuwa haina uwezo kifedha hata wa kuwasafirisha wawakilishi wao kwenda Afrika ya Kusini kwa mazungumzo ya kutafuta fedha za mradi, kampuni iliyokuwa haina uelewa stahili wa masuala ya nishati na iliyokosa rekodi nzuri ya utendaji, kufanikisha mradi huo.[102]

Kwa hali ya kawaida, kampuni yoyote inayoshindwa kutekeleza masharti ya mkataba na Serikali, inalazimika kukaa pembeni kwa muda kusubiri angalau mapungufu yake yasahaulike kidogo. Aidha muda ambao kampuni hiyo itakuwa imekaa pembeni utachukuliwa na waungwana kuwa wa kujisahihisha, wa kurekebisha mapungufu na kuweza kuaminiwa tena. Lakini si kawaida kwa kampuni iliyoshindwa kutekeleza kazi moja ya mteja kurejea muda mfupi

[102] Taarifa rasmi za Bunge HANSARD tarehe 17 na 19/12/2007 Mahojiano na Ndugu E. Chuwa, E. Muro na Ndugu Chaggama

baadaye kutafuta kazi nyingine tena yenye unyeti mkubwa kwa mteja huyohuyo bila kigugumizi wala soni.

Hivyo basi kwa Richmond Development Company LLC kuingia kwenye mchakato wa zabuni nyingine ya Wizara ya Nishati na Madini hata kabla wino kwenye barua iliyoandikiwa na Wizara ikilalamikia utendaji kazi wake haujakauka sawasawa, na kwa Wizara kufumbia macho ubabaishaji bayana wa “kampuni” hiyo na kuiruhusu kushiriki kwenye zabuni ya umeme wa dharura inayohitaji uzoefu maalum bila wasiwasi wa madhara ambayo yangeweza kutokea kwa Taifa, hisia za maslahi binafsi ya baadhi ya viongozi wa Serikali hazikwepeki.

7.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

7.1 Hitimisho

Kamati Teule imeuchambua kwa kina mchakato mzima wa zabuni ya uzalishaji umeme wa dharura ulioipa ushindi Richmond Development Company LLC ya Houston, Texas, Marekani mapema mwaka 2006 ili kuzitolea majibu yaliyokamilika hadidu rejea zote sita ambazo Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samuel J. Sitta(Mb), aliipa Kamati Teule tarehe 15 Novemba, 2007 mjini Dodoma.

Kurasa zote 165 za Taarifa ya Uchunguzi ya Kamati Teule ambayo inatokana na kazi kubwa ya kuwahoji jumla ya mashahidi 75, kuwauliza maswali 2,717 na kupitia nyaraka 104, zimebeba ushahidi usio na mashaka yoyote kwamba Wizara ya Nishati na Madini, iliibeba Richmond Development Company LLC kutoka mwanzo wa mchakato wa zabuni hadi mwisho. Kwa kufanya hivyo Wizara, kwa kutokufuata misingi ya utawala bora, ikachangia kwa kiasi kikubwa urefushaji wa mgao wa umeme ulioathiri shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii nchini. Kamati Teule imeridhika kuwa ukiukwaji huo unaweza kuwa ulichangiwa na hoja ya kukidhi maslahi binafsi. Pengine ndiyo sababu ya Wizara hii kuonesha tabia ambayo haikuoneshwa na Wizara zingine ya kukataa katakata kuiruhusu Kamati Teule kuona majalada ya Wizara hiyo yenye mawasiliano kuhusu zabuni hiyo.

Kwa muhtasari tu, tumeonesha katika Sehemu ya Pili ya Taarifa hii jinsi Wizara ya Nishati na Madini ilivyopindisha maamuzi ya Baraza la Mawaziri kwa kusitisha mpango uliokuwa umekaribia utekelezaji wa kuzalisha umeme kupitia mitambo ya kukodi ya kampuni ya CDC Globeleq bila kuufikisha ujumbe wa Serikali kwa kampuni hiyo wa kurekebisha masharti yao ili mradi huo utekelezwe. Hayo yamefanyika siku ileile Baraza la Mawaziri limetoa maagizo na siku nne baada ya kuanza mgao wa umeme kwa mikoa yote ya Tanzania Bara inayounganishwa na Gridi na Taifa.

Tumeonesha vilevile maamuzi yenye jeuri na kiburi ya kukiuka kwa makusudi Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005, licha ya Baraza la Mawaziri kusisitiza kwamba Sheria ya Ununuzi wa Umma na kanuni zake izingatiwe. Kama vile Wizara hiyo haihusiki kabisa na utawala wa sheria na utawala bora, ikailazimisha TANESCO isiheshimu ushauri wa kitaalamu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) na kuingilia mchakato wa zabuni wa *procurement entity* nyingine kwa kuiweka pembeni Bodi ya Zabuni ya TANESCO, kuiagiza TANESCO ivunje sheria kwa kuwabadilisha wajumbe wa Bodi yake ya Zabuni na Wizara kufanya maamuzi ya ununuzi kwa niaba ya TANESCO na kuulazimisha uongozi wake kusaini mkataba na kampuni ambayo TANESCO waliikataa mara tatu kwa vigezo vya kitaalamu kuwa haifai kwa kazi hiyo. Huo ulikuwa udhalilishaji mkubwa wa viongozi na watendaji ndani ya TANESCO.

Tumebainisha kuwa mwezi mmoja tu kabla ya hiyo zabuni ya kuzalisha umeme wa dharura, Wizara ya Nishati na Madini ilikuwa imeiandikia Richmond Development Company LLC kuitaarifu kuwa imeshindwa kutekeleza mkataba baina yake na Wizara kuhusu mradi wa bomba la mafuta. Kimya cha Wizara kuhusu udhaifu wa Richmond Development Company LLC, kuliipa Kamati Teule mashaka kuhusu uadilifu wa viongozi wa Wizara.

Tumeonesha vilevile kuwa Richmond Development Company LLC ilikingiwa kifua na kufunguliwa kila mlango na Wizara: majaribio ya Richmond Development Company LLC kubadilisha masharti ya Barua ya Dhamana ya Benki (LC) yaliungwa mkono na Wizara ya Nishati na Madini kwa hamasa kubwa kiasi cha kupuuza maelekezo ya Wizara ya Fedha kwa kulazimisha kufanya mabadiliko katika LC hiyo nje ya mkataba wa makubaliano wa fedha kwenye akaunti ya *escrow.*(Tumenukuu na kuambatanisha kwenye Taarifa hii barua mbili zilizoandikwa na Wizara hizi mbili tarehe 6 Oktoba, 2006 zikionesha hamasa iliyoigubika Wizara ya Nishati na Madini kuisadia Richmond bila hata kujali maslahi ya Taifa). Tumeonesha hata jinsi Richmond Development Company LLC ilivyoanza kazi bila kujiandikisha Bodi ya Usajili ya Makandarasi na wahandisi wake kuacha kujiandikisha Bodi ya Usajili ya Wahandisi na jinsi Wizara ya Nishati na Madini ilivyokuwa wima kuitetea kampuni hiyo ya Kimarekani. Aidha, Kamati Teule imejionea jinsi Richmond

Development Company (T) Ltd, kampuni tanzu ya Richmond Development Company LLC, ilivyopata *Cetificate of Incentives* kutoka Tanzania Investment Centre bila kukidhi masharti ya msingi kama vile ushahidi wa mtaji wa kutosha kutekeleza mradi.

Hatimaye, TANESCO walipotaka kuuvunja mkataba kati yao na Richmond Development Company LLC kwa kampuni hiyo ya Kimarekani kushindwa kutekeleza sehemu yake ya mkataba na kwa kutoa taarifa za uongo kuhusu hadhi ya kampuni hiyo, ni Wizara ya Nishati na Madini iliyoingilia kati na, bila aibu, "kuwezesha" mkataba huo urithiwe na kampuni nyingine katika kipindi ambacho nchi ilikuwa haihitaji kabisa umeme wa ziada licha ya kuwepo fursa za wazi kisheria kwa TANESCO kuvunja mkataba huo bila ya athari za hasara zozote.

Ubebwaji wa Richmond Development Company LLC na Wizara ya Nishati na Madini ulichangiwa na kurahisishwa zaidi na ukosefu wa umakini wa maafisa ndani ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambao, badala ya kuwa washauri wa sheria wa Serikali, wanageuka kuwa wasindikazaji! Taarifa hii imesheheni mifano ya matukio mbalimbali ya majadiliano ambayo Mwanasheria wa Serikali au wawakilishi wake hawafiki, hivyo kukosa uelewa mpana wa michakato mbalimbali. Hata wakifika, mchango wao wa kuilinda nchi dhidi ya vifungu vya sheria vya kutumaliza, hauonekani.

Katika suala hili la Richmond Development Company LLC, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilichangia sana kulea ubabaishaji kwa kutohudhuria vikao vya majadiliano na kufumbia macho dosari bayana au pengine kutojali. Mahojiano ya Kamati Teule na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mwakilishi wake kwenye majadiliano ya mikataba, yanajieleza yenyewe katika Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) za tarehe 30 Novemba, 2006 na tarehe 5 Disemba, 2007. Ulikuwa wajibu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kugundua kuwa Richmond Development Company LLC si kampuni yenye ukomo wa hisa; ulikuwa wajibu wa Ofisi ya Mwansheria Mkuu wa Serikali kuieleza Wizara ya Nishati na Madini kuwa Sheria ya Ununuzi wa Umma inataka kampuni inayoshinda kwa kigezo cha bei ya chini kufanyiwa *post qualification*, uchunguzi wa kina baada ya kuteuliwa; ulikuwa wajibu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuishauri Serikali kuwa *business card* na karatasi walizoonesha Richmond Development Company LLC haviwezi kuwa mbadala wa *consortium agreement* kati yake na Pratt & Whitney ya utekelezaji wa mradi huo wa umeme.

Utetezi mkuu uliotolewa na viongozi wa Wizara ya Nishati na Madini ni kwamba nchi ilikuwa katika dharura, hivyo ilibidi Wizara ichukue hatua ilizochukua na kwamba kanuni ya 42 ya *Public Procurement (Goods, Works, Non-consultant Services and Disposal of Public Assets by Tender) Regulations, 2005* inairuhusu Wizara kuingilia kati mchakato kwenye taasisi yake. Kamati Teule iliyakataa maelezo

haya kwani yanapotosha maana halisi ya *emergency procurement* chini ya Kanuni ya 42. Ni kweli kuwa kanuni hiyo inatoa mwanya na uhuru mpana zaidi wa maamuzi, lakini uhuru huo ni kwa taasisi yenyewe. Ni makosa kwa taasisi moja ya ununuzi (*procurement entity)* kuingilia maamuzi ya *procurement entity* nyingine kwa kisingizio cha dharura kama Wizara ya Nishati na Madini ilivyofanya. Ikiwa Wizara ilitaka ifanye kazi hiyo yenyewe, kwa nini basi isisaini mkataba na Richmond Development Company LLC yenyewe *as a procurement entity*, badala yake kuibambikizia TANESCO mzigo ambao haukuwa wake?

Kamati Teule sasa inaelewa chimbuko la tabia mbaya iliyoenea nchini ya ajali ikitokea watu kukimbilia kusaidia. Lakini si wote wenye dhamira ya kusaidia, kuokoa. Baadhi yao lengo kuu ni kuiba, kupora! Viongozi tunaobuni miradi kutokana na majanga ya kitaifa, hatuna tofauti na watu wanaokimbilia ajali kama waokoaji kumbe wezi. Ukame nchini ulitabirika, lakini hatukuchukua hatua mapema pengine kwa kusubiri janga kubwa litokee ili kupata fursa ya miradi ya akina Richmond.

Kamati Teule iliyaona mawasiliano ya karibu kati ya Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati na Madini katika hatua mbalimbali za zabuni hiyo. Kwa kuwa Waziri wa Nishati na Madini aliyekuwepo awali, Mhe.Dk. Ibrahim Msabaha(Mb) na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ndugu Arthur Mwakapugi, hawakukiri kutumwa au kuagizwa kuibeba kampuni hiyo

ya Kimarekani, kwa mfumo wa uongozi na utawala bora wanawajibika wenyewe.

Ifikapo mwaka 2025, Tanzania inatakiwa iwe imeondoka kwenye kundi la **nchi za kipato cha chini** *(low-income countries)* na kuingia katika kundi la **nchi za kipato cha kati** *(middle-income countries).* Kipato cha Watanzania kinategemewa kupanda kutoka Dola za Kimarekani 210 kwa mwaka kilichopo sasa hadi Dola za Kimarekani 3,420 kwa mwaka. Kwa fedha ya Tanzania ni kutoka sh. 262,500/= hadi sh. 4,275,000/= kwa mwaka. Kama Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anavyosema: maisha bora kwa kila Mtanzania yanawezekana, kila mtu atimize wajibu wake.

Moja ya sifa kuu za nchi za kipato cha kati ni kilimo cha kisasa na maendeleo ya kati ya viwanda, shughuli ambazo haziendi bila nishati ya kutosha na ya bei nafuu. Msingi wa kujenga uwezo wa kutosha wa nishati ili kuendeshea viwanda, unatakiwa uanze kujengwa sasa na si baadaye. Kamati Teule inakubaliana na ushauri uliotolewa na Kamati ya Uwekezaji na Biashara katika Taarifa yake kwa Bunge kwa mwaka 2006 kuwa Serikali sasa iandae mpango madhubuti wa muda wa kati na muda mrefu (*power system master plan*) ukionesha ni namna gani nchi itatekeleza na kukabiliana na tatizo la mfumo mzima wa uzalishaji na usambazaji wa umeme.
Mpango wa aina hii utaipunguzia Serikali gharama ya kuingia mikataba ya dharura mara kwa mara kila kukitokea ukame. Aidha

mpango huo ujumuishe pamoja miradi kama ya Stieglers George ya kuzalisha umeme wa MW 2100 na zaidi, makaa ya mawe ya Mchuchuma, umeme wa nishati ya gesi asilia, upepo, jua, taka n.k. Hapo tutakuwa tumejijengea msingi mzuri wa kupokea changamoto za maendeleo ya nchi za kipato cha kati.

7.2 **Mapendekezo ya Kamati Teule**

Kutokana na uchunguzi wa kina tuliouainisha katika taarifa hii, Kamati Teule imejiridhisha na hivyo inatamka bayana mbele ya Bunge Tukufu kuwa mchakato wa zabuni ya kuzalisha umeme wa dharura wa MW 100, uliopelekea Richmond Development Company LLC kuteuliwa na hivyo kusaini mkataba na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) tarehe 23 Juni 2006 na baadaye kurithiwa na Dowans Holdings S.A tarehe 23 Desemba 2006, uligubikwa na vitendo vya ukiukwaji taratibu, kanuni na sheria za nchi na hivyo kujenga kiwingu cha mashaka ya upendeleo, ubadhirifu na rushwa ambavyo vimechangia kumuongezea mwananchi mzigo wa gharama za umeme. Aidha, Kamati Teule imethibitisha bila ya shaka lolote kuwa uteuzi wa Kampuni dhaifu kifedha, kiufundi na kiuzoefu na ambayo haina usajili Marekani wala Tanzania kama kampuni yenye ukomo wa hisa, yaani Richmond Development Company LLC, ulitokana na kubebwa bila woga wala aibu na viongozi waandamizi wa Serikali. Kutokana na msingi huo Kamati Teule inapendekeza yafuatayo:

(1) Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2004 *(Public Procurement Act, 2004)* haina nguvu ya kutosha ya kuiwezesha Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha kwamba Ununuzi wa Umma unaboreshwa kwa kuongeza ushindani wa ukweli na uwazi na hivyo kuipa Serikali thamani halisi ya pesa zake. Kamati Teule inapendekeza kwamba sheria hii ipitiwe upya ili kuiboresha kwa kuipa Mamlaka nguvu zaidi za udhibiti na uwezo wa kuchukua hatua pale Sheria na Kanuni zinapokiukwa, badala ya kutoa ushauri tu kama ilivyo sasa.

(2) Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma isiwajibike Wizara ya Fedha ambayo nayo ni taasisi ya ununuzi (*procurement entity*) badala yake iwe chombo huru kinachowajibika Ofisi ya Rais na taarifa zake kuwasilishwa Bungeni.

(3) Mkataba kati ya TANESCO na Richmond Development Company LLC na sasa Dowans Holdings S.A, kama ilivyo mikataba kati ya TANESCO na IPTL, SONGAS, AGGREKO na Alstom Power Rentals inatoa unafuu usiostahili kwa makampuni hayo ya umeme na kuiumiza TANESCO na hatimaye watumiaji na walipa kodi kimapato, k.m mikataba hiyo kuwa na vipengele vya kuibana TANESCO kuyalipia makampuni hayo kodi zinazohusika na uendeshaji *(operations),* matengenezo/marekebisho ya mara kwa mara

ya mitambo *(maintenance)* gharama za bima, ada za mawakili na washauri elekezi *(consultants)* gharama za mafuta na gesi ya kuendeshea mitambo, gharama za ukodishaji mitambo *(capacity charges)* ambazo TANESCO hulipa kila mwezi si chini ya wastani wa shilingi bilioni 2 kwa kila kampuni, izalishe au isizalishe umeme. Kamati Teule inatoa rai kwa Serikali kuwa mikataba yote hii ipitiwe upya mapema iwezekanavyo kama ambavyo mikataba ya madini inavyopitiwa upya sasa na Serikali. Bila kufanya hivyo, mzigo mkubwa wa gharama za umeme utawaelemea wananchi na kushindwa kufikia azma ya Serikali ya maisha bora kwa kila Mtanzania.

(4) Mkataba kati ya TANESCO na Richmond Development Company LLC ulikuwa wa uzalishaji umeme wa dharura kipindi ambacho nchi ilikuwa katika hali ngumu ya ukame uliokausha mabwawa yote ya kuzalishia umeme. Kamati Teule inaitaka Serikali kutathmini upya uhalali wa kuwepo na kuendelea kuwepo na mkataba huo kutokana na udanganyifu bayana uliofanywa na Richmond Development Company LLC kuhusu uwezo wake kifedha, kiufundi, na uzoefu wake katika masuala ya uzalishaji umeme; usajili na uwepo wake kisheria kama kampuni halali yenye ukomo wa hisa nchini Marekani na Tanzania; uhusiano wake kisheria na Kampuni kubwa ya Kimataifa ya Pratt & Whitney na utambulisho wa Mzungu

mmoja kwa jina la John Perun kama mwakilishi wa Pratt & Whitney, mambo ambayo Kampuni hiyo kubwa ya Kimataifa imeyakanusha vikali.

(5) Mkataba kati ya TANESCO na Richmond Development Company LLC na sasa Dowans Holdings S.A umesheheni makosa mengi ya kisheria yanayoashiria udhaifu mkubwa wa kitaalamu katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali au ukosefu wa umakini ama ubinafsi katika kuiwakilisha Serikali. Kwa mfano, kushindwa kutambua ukosefu wa sifa za kikampuni za Richmond Development Company LLC; kushindwa kuishauri Serikali kuifanyia kampuni hiyo ukaguzi wa awali *(due deligence)* au ukaguzi baada ya uteuzi (post qualification); kushindwa kutambua tofauti kati ya *consortium agreement* na *proprietary information agreement;* kushindwa kuona dosari kisheria za *proprietary information agreement;* kushindwa kuona tofauti kisheria kati ya Richmond Development Company LLC, RDEVCO,RDVECO na RDC, majina ambayo wamiliki wa Richmond Development Company LLC walikuwa wanayatumia kwa kubadilisha badilisha *(interchangerbly)* kwa makusudi; kushindwa kuwashauri Wajumbe wa GNT kwamba *business card* si mbadala wa hati mahsusi kisheria; kushindwa kuishauri Serikali kuhakikisha kuwa muhtasari wa majadiliano kati ya Kamati ya Serikali ya Majadiliano (GNT)

na Richmond Development Company LLC ambao ulizingatia baadhi ya maslahi ya nchi, uwe sehemu ya Mkataba kati ya TANESCO na Richmond Development Company LLC; kushindwa kuishauri Serikali kutumia fursa iliyokuwepo wazi ya kuvunja Mkataba baada ya Richmond Development Company LLC kushindwa kutekeleza sehemu yake ya Mkataba; kushindwa kuhudhuria idadi kubwa ya vikao muhimu vya majadiliano;n.k. Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye katika majadiliano yake na Kamati Teule alionyesha kutokuelewa kabisa kilichokuwa kinatendeka na wasaidizi wake, na mwakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Wakili wa Serikali Donald Chidowu, ambaye ushiriki wake katika GNT haukuwa na tija yeyote, wawajibishwe na Mamlaka ya juu ya nchi kwa kuchangia kuiingiza nchi katika mkataba wa aibu.

(6) Katika mikataba yote na makampuni ya nje Serikali ihakikishe kuwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) inatumika kikamilifu katika kupata taarifa kamili za kampuni hizo, kama vile wanahisa, mitaji na anwani. Aidha, Ofisi zetu za Ubalozi zilizo sehemu mbalimbali duniani zihusishwe katika majadiliano na makampuni yanayotoka nje ya nchi kwa lengo la kupata taarifa zao za msingi na kuboresha nguvu ya hoja ya Serikali.

(7) Madhumuni ya Mkataba kati ya TANESCO na Richmond Development Company LLC yalikuwa kuzalisha umeme wa dharura kwa kipindi cha miezi kumi na mbili (12) tu. Muda huo ungeweza kuongezwa baada ya kutathmini hali ya ongezeko la maji katika mabwawa ya kuzalishia umeme nchini. Kabla ya muda wa tathmini hiyo haujafikiwa, wakati majadiliano yakiendelea GNT ikaongezea Richmond Development Company LLC muda wa kukodi mitambo hiyo kuwa miaka miwili (2). Kamati Teule haikuona vielelezo vyovyote vilivyojenga uhalali kwa GNT kuongeza muda huo. Uamuzi huo umeliongezea Taifa mzigo mkubwa wa gharama zisizokuwa za lazima. Mathalan, kwa upande wa *capacity charges* tu, TANESCO itailipa Dowans Holdings S.A jumla ya shilingi bilioni 54.8 kwa kipindi kilichongezwa cha mwaka mmoja. Aidha, GNT ilishindwa kutambua ulaghai wa Richmond Development Company LLC kuhusu mwakilishi wa Pratt & Whitney na hivyo kuamini karatasi ambayo ilikuwa haijathibitishwa na mawakili na diskette zenye picha za mitambo ya Pratt & Whitney, vielelezo ambavyo Kamati Teule imegundua na kuthibitisha kuwa vilikuwa vya kugushi. Vilevile, bila kujali kwamba TANESCO ingelazimika kuilipa Richmond Development Company LLC shilingi milioni 152 kwa siku kama gharama ya kuweka vifaa vyao nchini, GNT ikakubali kilegelege kuitoza Richmond Development Company LLC shilingi milioni 12 tu kwa siku kama fidia kwa

ucheleweshaji wa kuanza kuzalisha umeme kulingana na tarehe iliyokubalika kwenye mkataba. Kamati Teule inapendekeza kuwa Wajumbe wote wa GNT ambao ni maafisa waandamizi wa Serikali wawajibishwe mara moja kwa kushindwa kutumia elimu na ujuzi wao kulinda maslahi ya Taifa.

(8) Pamoja na Uongozi wa TANESCO kubainisha mapungufu ya Richmond Development Company LLC na kutoa notisi tarehe 27 Octoba 2006 ya kusitisha Mkataba tena kwa ushauri mahsusi kutoka Kampuni ya Kimataifa ya Mawakili, Wizara ya Nishati na Madini haikuupenda mwelekeo huo hivyo tarehe 28 Novemba 2006 baadaye Waziri wa Nishati na Madini Mhe. Nazir Karamagi, Mb akiwa nje ya nchi Calgary, Canada alimuagiza Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO Balozi Kazaura kuangalia uwezekano wa kuhaulisha Mkataba wa Richmond kwa kampuni nyingine. Siku tano baada ya mawasiliano hayo, yaani tarehe 4 Desemba 2006, TANESCO ikapokea barua kutoka Richmond Development Company LLC ikielezea nia ya kampuni hiyo kutumia haki yake chini ya kifungu 15.12 cha mkataba ili kuhamisha majukumu yake ndani ya mkataba kwenda kwa kampuni mpya ya Dowans Holdings S.A. Kamati Teule ilipata taarifa za ndani ya Wizara na TANESCO kuwa viongozi wa Wizara kama kawaida yao waliishinikiza TANESCO kuridhia ombi hilo la Richmond Development

Company LLC kuhaulisha mkataba kwa Dowans Holdings S.A. TANESCO ikalazimika kuridhia uhaulishaji wa mkataba huu badala ya kutumia fursa iliyokuwepo ya kusitisha mkataba baada ya kutoa notisi ya siku thelathini. Kamati Teule inaamini kwamba uamuzi wa Wizara ya Nishati na Madini kuizuia TANESCO isitumie fursa ya kusitisha mkataba huo, unaashiria jinsi viongozi wetu wanavyojali zaidi faida na maslahi ya makampuni ya nje kuliko maslahi mapana ya Taifa. Tarehe 3 Desemba TANESCO kama ilivyoagizwa ikaridhia uhaulishwaji wa mkataba huo lakini kipindi ambacho hali ya maji katika mabwawa yetu ya kuzalishia umeme ilishaanza kurejea kuwa ya kawaida. Uamuzi huo umeliingizia Taifa hasara kubwa. Hivyo basi Kamati Teule inapendekeza kwamba Waziri wa Nishati na Madini Mhe. Nazir Karamagi, Mb aliyeshabikia sana uhaulishaji huo, awajibishwe.

(9) Matokeo ya uchunguzi ya Kamati Teule kama yalivyoainishwa hapo juu yanadhihirisha wazi jinsi Taifa lilivyotumbukizwa kwenye hasara kubwa kutokana na mkataba huo wa Richmond Development Company LLC na Dowans Holdings S.A, kinyume na taarifa iliyotolewa na TAKUKURU (wakati huo TAKURU) kwamba Taifa halikupata hasara yoyote. Taarifa ya TAKUKURU ililenga kuficha ukweli *(white wash)* hivyo ikaishia kujikanganya kwa kukiri kuwepo kwa

mapungufu lakini yasiyokuwa na athari. Taarifa hiyo imemong'oa kwa kiasi kiasi kikubwa hadhi na heshima ya chombo hiki muhimu cha kitaifa kilichopewa dhamana na rushwa na sio kuipamba ili kurejesha heshima ya umma katika taasisi hiyo, Kamati teule inapendekeza mabadiliko ya haraka ya uongozi wa taasisi hiyo.

(10) Taratibu za malipo ya madai ya mkataba wa umeme wa dharura zinafanywa kupitia Barua ya Dhamana ya Benki iliyofunguliwa kati ya TANESCO na benki ya CRDB ya dola za Kimarekani milioni 30,696,598 iliyofunguliwa tarehe 27 Desemba 2006. Kamati Teule imethibitisha kwamba hadi kufikia tarehe 19 Juni 2007 malipo yaliyolipwa na Benki Kuu yamefikia Dola za Kimarekani 35,561,598 kiasi hicho ni zaidi ya Barua ya Dhamana ya Benki kwa dola za kimarekani milioni 4,565,000 wastani wa shilingi bilioni 5.7. Kamati Teule inashangaa ni vipi Benki Kuu iidhinishe malipo hayo nje ya Barua ya Dhamana ya Benki iliyofunguliwa kati ya TANESCO, CRDB Bank na Dowans Holdings S.A. Kwa kuwa Benki Kuu ndio msimamizi mkuu wa akaunti maalum *(Escrow Account),* Gavana wa Benki Kuu pamoja na Bodi ya Wakurugenzi wachunguze kwa makini uhalali wa malipo hayo na kuhakikisha kwamba udhaifu wa namna hii haujitokezi tena hapo baadaye.

(11) Wakati umefika sasa kwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 1995 *(Public Leadership Code of Ethics Act)* ifanyiwe marekebisho makubwa ili kudhibiti utaratibu unaonekana wa kawaida sasa wa viongozi waandamizi wenye dhamana kisiasa kuendelea na biashara zao wakiwa madarakani, hivyo kuwaweka kwenye mtihani mkubwa wa mgongano wa kimaslahi katika maamuzi yao. Tufike mahali ambapo sheria iwalazimu kuchagua kati ya Utumishi wa Umma au biashara binafsi. Viongozi waandamizi wenye dhamana kisiasa (mawaziri na kuendelea) kuendelea na biashara zao wakiwa madarakani hivyo kuwaweka kwenye mtihani mguu wa mgongano wa kimaslahi.

(12) Serikali iondokane kabisa na utaratibu wa kutumia mawakala katika ununuzi wa mitambo ya kuzalisha umeme nchini na kuhakikisha kuwa Wizara husika ina taarifa za bei halisi ya mitambo kila wakati ili kujiepusha na mchezo wa kawaida wa mawakala kupandisha bei mara mbili au zaidi ya bei halisi. Kamati Teule ilishuhudia bei za mitambo hiyo jijini Houston, Texas Marekani kwa watengenezaji kiwandani ikiwemo kampuni ya Kawasaki Gas Turbines – Americas ambayo iko chini ikilinganishwa na bei zinazotolewa na mawakala hao, jambo ambalo lingeiwezesha Serikali kununua na kumiliki badala ya kukodi kwa muda mfupi na kwa gharama kubwa. Mathalan, MW 105 zingepatikana kwa

kununua mitambo sita ya MW 17,5 kila mmoja kwa gharama ya shilingi bilioni 56.25 badala ya shilingi bilioni 108.7 tulizotandikwa na Richmond Development Company LLC mitambo hiyo ikibaki mali ya wakodishaji. Kwa kumalizia Kamati Teule ilithibitisha kwamba kauli iliyokuwa inatolewa mara kwa mara na baadhi ya viongozi wote tuliowahoji kwamba kipindi hicho cha ukame haikuwa rahisi kupata mitambo hiyo na ilikuwa ikigombaniwa na nchi nyingi kauli hiyo ilikuwa sio ya ukweli na upotoshaji mkubwa.

(13) Utaratibu tuliourithi kutoka kwa wakoloni na kuuzoea wa kuiona mikataba ya kibiashara kuwa ni siri hata kwa walipa kodi wenyewe na kuwa uwanja wa pekee wa watendaji, ambao Waziri wa Mipango Uchumi na Uwezeshaji Mhe. Dk Juma Ngasongwa (Mb) aliusifia bungeni tarehe 19 Aprili 2007 kuwa *best practice* wakati akijibu swali la Mhe. Masolwa C. Masolwa (Mb) Mbunge wa Bububu, umepitwa na wakati na unakiuka misingi ya demokrasia na uwajibikaji. Matokeo ya utaratibu huu ni kuwepo kwa mikataba mibovu inayoficha vipengele vinavyoibebesha Taifa mizigo mikubwa ya gharama zisizokuwa za lazima kama tulivyoainisha katika pendekezo namba 3 hapo juu. Kamati Teule inatoa wito kwa Serikali kuondokana na utaratibu huu usio na tija kwa kuzihusisha Kamati za Kudumu za Bunge kwenye hatua za awali za maandalizi ya mikataba hiyo. Aidha, Kamati Teule inatoa

wito kwa Kamati zote za Bunge zihakikishe kuwa zinapitia mikataba mikubwa nay a muda mrefu ya kibiashara chini ya sekta zao ili kuliondolea Taifa mizigo isiyo ya lazima. Pale ambapo upatikanaji wa mikataba hiyo unakwamishwa kwa urasimu usio wa lazima Kamati zitumie utaratibu uliotumiwa na Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara ya kuunda Kamati Teule yenye ufunguo wa mikataba iliyofichika.

(14) Pamoja na dharura iliyokuwa inalikabili Taifa, Serikali haiwezi kuwa kinara wa uvunjaji wa taratibu, kanuni na sheria za nchi kwa makusudi. Kamati Teule imeanisha katika taarifa hii vitendo vya ubabe, ujeuri na kiburi vilivyofanywa na viongozi wa Wizara ya Nishati na Madini alimradi kampuni waliyoitaka iteuliwe kiasi cha kupindisha hata maamuzi ya Baraza la Mawaziri bila wasiwasi wowote, kukaidi ushauri wa kitaalamu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma mara tatu mfululizo na kinyume na maagizo ya Baraza la Mawaziri lililotaka Sheria ya Ununuzi wa Umma izingatiwe, kukiuka sheria kwa makusudi kwa kuingilia mchakato wa zabuni wa taasisi nyingine ya ununuzi, kuvipuuza vyombo vya ndani vya maamuzi vya TANESCO (Bodi ya Wakurugenzi, Bodi ya Zabuni n.k), kuilazimisha Bodi na Menejimenti ya TANESCO kuridhia maamuzi yaliyofanywa na Wizara ya kuibeba Richmond Development Company LLC kinyume cha sheria na taratibu n.k. Wizara hiyo katika kuibeba Richmond

Development Company LLC ilifikia hatua ya kupotosha kwa makusudi ushauri wa Wizara ya Fedha uliozuia malipo ya awali ya Dola za Kimarekani Milioni 10 katika Barua ya Dhamana ya Benki ya Richmond Development company LLC tarehe 6 Octoba 2006. Kamati Teule inapendekeza kwamba Waziri wa Nishati na Madini wa wakati huo Mhe. Dk. Ibrahim Msabaha (Mb) na Katibu Mkuu Ndugu Arthur Mwakapugi wachukuliwe hatua kali za kinidhamu kwa kuliingiza Taifa kwa makusudi kwenye mkataba na kampuni ya mfukoni ambao umesababisha hasara kubwa kwa nchi. Aidha Kamishna wa Nishati Ndugu Bashir Mrindoko naye achukuliwe hatua za kinidhamu kwa kushindwa kumshauri Katibu Mkuu mpya wa Wizara kuhusu udhaifu wa Richmond Development Company LLC ambao ulijulikana dhahiri na Wizara toka mwaka 2004 kwenye mkataba wa Bomba la Mafuta. Ndugu Mrindoko ndiye aliyeiandikia barua kampuni hiyo kusitisha mkataba wake na Serikali mwezi mmoja tu kabla ya mchakato wa zabuni ya umeme wa dharura haujaanza.

(15) Utaratibu wa kuteua wakurugenzi na makamishna katika Wizara kuwa wajumbe wa bodi za wakurugenzi za mashirika yaliyo chini ya Wizara, unazua mgongano wa kimaslahi, kudhoofisha usimamizi na uwajibikaji, hivyo Serikali iupige marufuku mara moja. Mfano Kamishna wa Nishati ni Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO ambaye alishiriki

kwenye kikao kilichowakataa wazabuni wote kuwa hawafai na kuishauri Serikali vilivyo, aliporejea Wizarani alishiriki katika kutengua maamuzi ya Bodi ya TANESCO.

(16) Uhuru mkubwa ambao viongozi wa Wizara ya Nishati na Madini waliutumia bila wasiwasi katika kuhakikisha kwamba kampuni waliyoitaka, Richmond Development Company LLC, inapewa zabuni ya umeme wa dharura; maelekezo ya mara kwa mara ya Waziri Mkuu kwa Wizara katika kila hatua ya mchakato huo; upendeleo wa dhahiri ambao Richmond Development Company LLC iliupata kutoka taasisi mbalimbali za Serikali k.m Kituo cha uwekezaji (TIC) ambacho kilifikia hatua ya kufumbia macho baadhi ya taratibu zake za msingi ili kuipa kampuni tanzu ya Richmond Development Company LLC cheti cha uwekezaji haraka iwezekanavyo; kutotimiza masharti ya Bodi za Makandarasi na Wahandisi na Wizara ya Nishati na Madini kuikingia kifua kampuni hiyo isichukuliwe hatua za kisheria; uteuzi wa mwisho wa Richmond Development Company LLC kuwa mkandarasi kufanywa na Waziri Mkuu mwenyewe tarehe 21 Juni 2006[103]; uamuzi wa kuiteua Richmond Development Company LLC kuwa mkandarasi kusafishwa na TAKURU (sasa TAKUKURU) kuwa ulikuwa wa wazi na wa haki; uamuzi wa Serikali kuizuia TANESCO isivunje mkataba na kampuni hiyo

[103] Barua Kumb. Na. 1/CEA 136/444/01

Iicha ya sababu zote kisheria kuwepo, ni baadhi tu ya viashiria vya nguvu kubwa iliyo juu ya Wizara ya Nishati na Madini kutumika katika suala hili na Kamati Teule kutokana na ushahidi wa kimaandishi, kimazingira na wa mdomo, inaiona nguvu hiyo kuwa ni Waziri Mkuu.

Ibara ya 52 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inatamka wazi kuwa Waziri Mkuu ndiye mwenye madaraka ya juu ya udhibiti, usimamiaji, utekelezaji wa siku hadi siku wa kazi na shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano na ndiye Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni. Kamati Teule haikufurahishwa hata kidogo na taarifa zinazomgusa moja kwa moja Mhe. Waziri Mkuu katika kuipendelea Richmond Development Company LLC. Hata hivyo Kamati Teule imetimiza wajibu wake kwa uwazi na ukweli kama ilivyoagizwa na Bunge letu Tukufu. Kwa kuzingatia umuhimu wa nafasi aliyonayo Mhe. Waziri Mkuu katika uendeshaji wa shughuli za Serikali na uongozi wa nchi kwa ujumla, ni wajibu wake yeye mwenyewe kupima uzito wa matokeo ya uchunguzi huu na wajibu wake kikatiba ndani na nje ya Bunge. Vile vile ni wajibu wa Bunge ambalo linathibitisha uteuzi wake kwa mujibu wa Ibara ya 51 inayothibitisha uteuzi wake kuangalia ikiwa matokeo ya uchunguzi huu hayajaathiri hadhi na uzito wake ndani ya Bunge.

7.0 SHUKRANI

Napenda kuchukua fursa hii kulishukuru na kulipongeza Bunge letu Tukufu kwa kukubali kwa kauli moja kuunda Kamati hii Teule. Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kutupa heshima hii kubwa ya kututeua kuwa Wajumbe wa Kamati hii.

Pia napenda kuishukuru Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa ushirikiano wake mzuri ambao uliiwezesha Kamati hii kupata taarifa mbalimbali. Vilevile naushukuru Ubalozi wa Tanzania wa Washington D.C, Marekani kwa kuwawezesha baadhi ya Wajumbe wa Kamati hii waliosafiri kwenda Marekani kufanya kazi yao kwa ufanisi. Nakishukuru Chama cha Uwekezaji cha Watanzania waishio Marekani *(Tanzanian American Investment Forum- TAIF)* chini ya Mwenyekiti wake Dk. Lenard Tenende kwa mapokezi mazuri ya Wajumbe wa Kamati Teule walipozuru Houston, Texas - Marekani.

Shukrani za pekee na pongezi ziwaendee waandishi wa habari na vyombo vyao walioweka maslahi binafsi pembeni na kupiga kelele kwa nguvu zao zote kuhusu mwenendo uliokuwa hauridhishi wa mchakato wa zabuni ya umeme wa dharura.

Vilevile shukrani zetu ziende kwa Watanzania na watu wote wenye nia njema na nchi hii waliotuunga mkono kwa kutupa taarifa mbalimbali, maoni kwa njia ya barua pepe, simu n.k.

Kwa kumalizia namshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Damian S.L Foka kwa kuisadia Kamati hii kufanya kazi vizuri. Aidha, shukrani za pekee zinatolewa kwa Katibu wa Kamati hii Ndg. Anselm Mrema na wasaidizi wake Ndugu Emmanuel Mpanda, Ndugu Lina Kitosi na Ndugu Nenelwa Mwihambi kwa umakini mkubwa waliouonyesha hali iliyosaidia Kamati Teule kufanikisha kumaliza kazi yake kwa ufanisi.